Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao Cha Thelathini na Tatu - Tarehe 28 Julai, 2003**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilisha na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2003/2004.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Katika Mwaka Uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2003/2004.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 319

**Majibu ya Maswali Bungeni**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa maswali yanayoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, katika Bunge hili yana msingi wa kuelezea kero zilizopo na kushawishi Serikali kuchukuwa hatua zipasazo kuzikabili kero hizo; na kwa kuwa mara nyingine majibu ya Serikali huwa ya mkato tu au kuitupia Wizara nyingine mpira na hivyo kufanya majibu yatolewayo yasikidhi haja, mfano swali langu Na. 330 lililojibiwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge, chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Swali Na. 56 lililojibiwa katika Mkutano wa Sita wa Bunge, chini ya Wizara ya Ujenzi:-

(a) Je, isingekuwa vema kwa Wizara mbalimbali chini ya uongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, zikawasiliana na kutoa jibu sahihi kama Serikali badala ya kurudisha mpira kwa Wabunge na kuwataka Wabunge wafuatilie Wizarani au Taasisi nyingine?

(b) Je, ni sawa kuyapeleka maswali ya msingi na ya kihimili yanayohusu Serikali Kuu na yenye gharama kubwa kama Usalama wa Rais na Usalama wa Taifa kwa Halmashauri ya Wilaya?

(c) Je, Waheshimiwa Wabunge, wanashauriwa wafanye nini wanapopewa majibu ya msingi na ya nyongeza yasiyoridhisha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Tano wa Bunge hili, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, aliuliza maswali mawili, la kwanza lilikuwa Swali Na. 24 lililoelekezwa Wizara ya Viwanda na Biashara na la pili lilikuwa Na. 132 lililoelekezwa Wizara ya Ujenzi. Swali Na. 330 chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, hakuliuliza katika Mkutano wa Tano kama alivyosema, bali aliliuliza katika Mkutano wa Nane. Aidha, katika Mkutano wa Sita wa Bunge hili Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, aliuliza swali moja Na. 57 aliloliekeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Kwa hiyo, swali Na. 56 chini ya Wizara ya Ujenzi hakuliuliza Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro kama alivyosema, ila liliuzwa na Mheshimiwa Harobu Said Masoud na liliekezwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa uthibitisho huo hapa ninazo *Hansard* ambazo zinathibitisha ukweli wa maelezo niliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara inapopata swali kutoka kwa Mbunge, huwa inafanya mawasiliano na Wizara nyingine ikiwa ni pamoja na Taasisi zenye mahusiano na Wizara yenye dhamana ya swali katika kuandaa majibu yanayokidhi matakwa ya swali hilo. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, inao utaratibu wa kuratibu maswali na majibu ya maswali yanayoelekezwa katika Wizara mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, majukumu ya Serikali za Mitaa ni pamoja na kuangalia usalama wa raia katika Halmashauri na ujumla wake unafanya Usalama wa Taifa nchini ambao ni chombo cha Serikali Kuu. Hivyo hakuna ubaya endapo swali linalohusu usalama wa raia na usalama wa Taifa litashughulikiwa katika Halmashauri ya Wilaya, kama liko ndani ya uwezo wake kimamlaka na kisheria.

(c) Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa usahihi na ufasaha kulingana na hoja iliyotolewa na muuliza swali. Hiyo, ni kazi inayotekelezwa na Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuzingatia Kanuni za Bunge hili.

Aidha, ni utaratibu uliwekwa wazi kwamba, Mheshimiwa Mbunge ambaye ataona haridhiki na jibu au majibu yaliyoendelea kutolewa na Serikali, anaweza kuuliza tena kwa idhini ya Spika na Serikali inaowajibu wa kujibu kwa kutoa majibu ya ufafanuzi zaidi ili kukidhi hoja husika. Kwa mantiki hii, namshauri Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu waitumie fursa hiyo na Serikali itajitahidi kutekeleza wajibu wake.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo yana nahau nyingi napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa jukumu la ulinzi ni jukumu la Serikali Kuu, maswali niliyouliza yalikuwa yanahusiana na Serikali Kuu, moja niliuliza habari ya ukosefu wa vifaa vya ulinzi katika Jimbo la Mkinga, ambalo liko mpakani na lina mstari mrefu wa bahari. Vyombo hivi vilihusu boti, magari, vyombo vya mawasiliano pamoja na ofisi na nyumba.

(i) Je, huo siyo wajibu wa Serikali Kuu, kushughulikia masuala haya badala ya kutupia Serikali? *(Makofi)*

(ii) Niliuliza Wizara ya Ujenzi kuhusu barabara ya mpakani nikaelezwa kwamba nchi jirani na ya kwetu wana barabara ambazo wanazitumia kwa ulinzi. Wizara ya Ujenzi ilisema kwamba barabara hiyo haipo na ukweli ni kwamba ipo. Je, Wizara hiyo, itakuwa tayari kufuatana na mimi nikawaonyeshe barabara hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sikumbuki kama aliuliza juu ya *specifics* hizi juu ya vifaa vya ulinzi katika Wilaya. Lakini ninachotaka kusema ni ukweli ulio wazi kwamba Wilaya inahusika sana na ulinzi na usalama wa raia ndani ya Wilaya, ndiyo maana msimamizi wa shughuli za Serikali ndani ya Wilaya ikiwa ni pamoja na shughuli za Halmashauri ni Mkuu wa Wilaya ambaye ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Kwa hiyo, kwa vyovyote vile Wilaya ndiyo inapaswa kusimamia. Huu ndiyo ukweli. Sasa yako matatizo fulani fulani yanajitokeza yanayohusu sekta fulani ndani ya Wilaya, Wilaya inachofanya ni ku-*coordinate* na kuwasiliana na Wizara inayohusika ili kuyatatua. Kama haya matatizo ya upungufu wa vifaa vya mawasilano na ulinzi, Wilaya inaweza ikaratibu na kuwasiliana na Wizara inayohusika ili kuyatatua. La pili, juu ya barabara bahati mbaya hata mimi sijui, lakini pengine nitashauriana na wenzangu wanaosimamia barabara hii wapate fursa waje kuiangalia il iwaweze kupata maelezo katika eneo linalohusika.

**MHE. SEMINDU. K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa jibu la namba (c) linahusu maswali ya Kanuni na alijibu kwamba swali kama Mbunge hakuridhika anaweza akauliza tena, kwa ajili ya kupunguza utitiri wa maswali yanayorudiwa rudiwa na maswali mengine mara nyingi yanakuwa yameshamalizwa tayari, lakini mengine yana msingi wa hali ya Serikali.

Je, Waziri anakubaliana na wazo hili kwamba ayachukue maswali haya yakijibiwa na sekta, katika Sekta za Kamati za Bunge au yakashughulikiwa na Kamati Maalum, tuunde Kamati moja maalum ya kufuatilia ahadi za Serikali ili kumaliza maswali ya utitiri wa kujirudia rudia? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, yote aliyosema yanaweza kufanyika na yanaweza kutekelezeka, huo ni ushauri lakini kama anavyojua mambo yote ambayo huwekwa kwenye Kanuni huanzia mahali fulani. Kwa hiyo, nafikiri Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge amesikia. *(Makofi)*

Na. 320

**Bima kwa Jengo la Ukumbi wa Bunge**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo tarehe 4 Novemba, 2002 Mji wa Dodoma ulikumbwa na balaa la Tetemeko la Ardhi na kwa kuwa tetemeko hilo liliwaletea Waheshimiwa Wabunge waliokuwa ndani ya Ukumbi wa Bunge hofu kubwa:-

(a) Je, Jengo la Ukumbi wa Bunge Dodoma lina Bima ya kiasi gani?

(b) Je, kila Mheshimiwa Mbunge, amewekewa kinga ya Bima ya kiasi gani?

(c) Je, isingekuwa vyema kukaanzishwa kinga ya bima ya vikundi *(Group Personal Accident)?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Jengo la Ukumbi wa Bunge ni la Serikali. Majengo yote ya Serikali pamoja na vifaa vingine yakiwemo magari na mitambo mingine huwa haviwekewi bima.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Jengo la Ukumbi wa Bunge Dodoma halina Bima, kwa kuwa ni mali ya Serikali.

(b) Waheshimiwa Wabunge nao hawana kinga ya Bima wakati wakiwa kwenye vikao vya Bunge ndani ya Jengo la Mikutano ya Bunge kwa vile utaratibu huo haujaanzishwa.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa kuwa na kinga ya Bima ya vikundi ilimradi tu jambo lenyewe tulizungumze sote kwa pamoja kupitia Tume yetu na wadau wengine ili kupata muafaka.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, binafsi labda niseme sina uhakika wa taratibu za Mabunge ya Jumuiya ya Madola, kama yana utaratibu huu. Lakini mimi nina amini kila Mbunge, ana mipango yake ya kujiwekea Bima. Lakini ndani ya chombo kikubwa kama hiki mimi nadhani suala hilo lingetiliwa mkazo kwa sababu kama balaa lililotaka kutokea siku ile kama baadhi ya viongozi mlikuwa mnakimbia huko mbele ingeweza kuumiza watu. ? *(Makofi/Kicheko)*

Sasa je, Mheshimiwa Waziri atafanya utaratibu huo na labda kama atahitaji ushauri wa kibima tuweze kumsaidia? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Chubi, kama ifuatavyo: -

Mimi nakubali kabisa ushauri aliotoa Mheshimiwa Omar Chubi. Hata nilivyokuwa nasema hapa nilisikia mnaguna kwa maana ya kwamba wote mnaungana na Mheshimiwa Omar Chubi, hata mimi ningependa kuwa na Bima. Sasa kama nilivyosema kwa masuala yanayotuhusu Wabunge lazima tuyaanzishe sisi wenyewe hakuna mtu mwingine wa kutuanzishia. Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema tuzungumze basi, humu ndani tuko Wajumbe wa Tume, Mwenyekiti, nayo yuko hapa hapa tuzungumze nini tunakata. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa wakati huu ambapo jengo hili halina Bima, ikitokea bahati mbaya dhahama ikatokea na Wabunge wakaumia vibaya au pengine kufariki wakiwa kazini, je, ni utaratibu gani utakaoweza kutumika kuweza kuwalipa au kulipa familia zao kwa njia mbalimbali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

Ikitokea ambapo tunaomba Mwenyezi Mungu isitokee na naomba aendelee kutulinda hivi hivi isitokee, lakini kama kweli itatokea, basi sheria zipo *Work-manship Compesation* ipo inayohusika na fidia za wafanyakazi, lakini pia ziko Kanuni ambazo zimeandaliwa na Tume ya Haki za Bunge, ambazo zinashughulikia mambo haya.

Endapo Mheshimiwa Mbunge ataumia, atatibiwa kwa mujibu wa masharti ya kazi ya Mheshimiwa Mbunge, ambayo yameandikwa, kama itabidi atibiwe ndani ya nchi, atibiwe kwenye hospitali ya Serikali, au ikishindikana apelekwe nje ya nchi kwa matibabu zaidi. Hayo yote yako wazi kwa mujibu wa taratibu zetu za kazi za Ubunge. *(Makofi)*

Na. 321

**Madini ya Aina Mbalimbali - Kalalani Korogwe**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu eneo la Kalalani katika Mto Umba Kata ya Mashewa Wilayani Korogwe yamegundulika kuwa na madini mengi sana aina ya vito kama vile *Red and Green Tomarine, Peter Stones, Blue Sapphire* na kadhalika na kwa kuwa eneo hilo Mererani, Geita, Kahama na kadhalika ambako Serikali imetafuta wawekezaji wa kuchimba madini hayo kwa ufanisi mkubwa na kuliongezea pata mapato na kuwawezesha kiuchumi wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vinavyowasaidia kwenye uchimbaji wa kisasa hivyo kujiongezea kipato:-

(a) Je, eneo la Kalalani lina wawekezaji wakubwa wangapi wanaochimba madini hayo kisasa na kitaalam ili kuliongezea Taifa letu mapato makubwa?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kutafuta wawekezaji wakubwa na wa uhakika kwenye eneo hilo ili wakishinikizwa na wachimbaji wadogo wadogo waweze kuchimba madini hayo kwa wingi kwa lengo la kuwakwamua wananchi wa Kalalani kutoka kwenye umaskini uliokithiri na kuinua Pato la Taifa?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kutimiza ahadi yake ya kuwakwamua wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwawezesha kiuchumi, kuwapatia vifaa vya kisasa vitakavyowasaidia katika uchimbaji wa kisasa na kuinua kipato chao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, madini ya vito yanayopatikana Kalalani ni pamoja na *Rhodolite, Green Tourmaline, Malaya Garnets, Green Garnets, Blue Sapphire, Almandine* na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, pengine hatuyajui madini yanayoitwa *Peter Stones.* Jina hilo limepachikwa tu katika suala la madini kutokana heshima pengine kutokana na mmoja wa wachimbaji maarufu na wa miaka mingi Kalalani, Bwana Alfred Peter. Madini ya vito ili yawe ni madini ya vito yenye thamani hapana budi yawe na sifa mbili kubwa mosi, yawe ni mazuri yaani ukiangalia tu yaonekane ni mazuri na pili uadimu. Madini ya vito yanayozalishwa kwa wingi yanaweza kuifanya bei iporomoke inategemea na umahiri wa madini yenyewe.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa eneo la Kalalani lina Kampuni moja tu ya mwekezaji mkubwa nayo ni kampuni ya ubia kati ya Watanzania na Wathai inayoitwa ya kampuni ya madini ya vito Afrika, *(Asia Precious and Mining Limited).* Aidha, ipo kampuni ya Watanzania inayojulikana kama *Amazon Trading Limited* yenye leseni kubwa ya utafutaji wa vito katika eneo hilo. Kampuni hiyo bado iko kwenye ngazi ya utafiti, haijaanza kuchimba.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madini ya vito ili yaendelee kuwa na thamani ni vizuri yakachimbwa kidogo kidogo na kwa kuwa uchimbaji wa madini hayo ni chanzo kikubwa cha ajira makampuni ya kigeni hayapendi kujihusisha mara nyingi na utafutaji wa uchimbaji wa madini ya vito kwani madini haya pia yanaweza kutengenezwa katika maabara *(production of synthetic gemstones).* Hali hiyo inafanya bei ya madini ya vito katika soko la dunia kuwa isiyotabirika kwa urahisi jambo ambalo wawekezaji hawalipendi.

(c) Mheshimiwa Spika, mikakati iliyopo ni pamoja ni kama kupitia Ofisi za Kanda za Madini kama moja iliyopo mjini Tanga, tunahamasisha wachimbaji wadogo kukata hati za uchimbaji ili wahalalishe shughuli zao na wajulikane, tunawataka waunde ushirika katika maeneo yao kurahisisha kupata mikopo na misaada ya fedha ya kununulia vifaa na tunawahamasisha kutafuta ubia na watu wenye uwezo wa kifedha kama ilivyofanyika hivi karibuni kati ya Bwana Alfred Peter na Bwana Reginald Mengi mwanzoni mwaka huu.

Pia kuimarisha soko la ushindani kwa kutoa leseni za biashara za madini ya vito kwa wanunuzi mbalimbali na mwisho, kuhamasisha ukataji wa madini ya vito hapa nchini ambapo wanaofanya hivyo wana uwezo wa kununua madini ya vito kutoka kwa wachimbaji wadogo kwa bei nzuri.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa kwa muda mrefu wanaochimba madini kule Kalalani wameomba wapatiwe eneo katika eneo la Daboetesi ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumza kwamba mwekezaji huyu ni wa muda mrefu na kazi yake inasuasua na wachimbaji wadogo wadogo hawana eneo, wameomba kwa muda mrefu lakini mpaka leo bado wananyimwa.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo wadogo angalau wapate eneo kwenye maeneo haya ambayo ndiyo yenye madini, lakini hawapati nafasi ya kuchimba au kupewa ruhusa ya kuchimba? *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusu Mzee Peter na Mzee amesema hawamtambui, lakini katika soko la nje Jiwe la *Peter Stone* linatambuliwa kwa maana ya huyu mzee Peter akiwa ni mwanzilishi na mgunduzi wa hilo jiwe. Je Serikali haioni kwamba ni heshima kwanza kwa Mtanzania huyu kuwa na jiwe linaloitwa *Peter Stone* na wakamsaidia ili angalau waweze kupata unafuu wa kuchimba zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Joel Bendera kama ifuatavyo:-

Kwanza hili suala la wachimbaji wadogo wadogo kwamba wamekuwa wakiomba kwa muda mrefu bila mafanikio, lazima nikiri kwamba mimi ndiyo nalisikia sasa hivi. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitakuwa tayari nionane naye baada ya Bunge hili la leo ili yeye pamoja na mimi tushughulikie suala hili, tuone namna gani wananchi hawa ambao wanaomba eneo hilo na kama liko wazi wanaweza wakapewa ili waweze kuchimba. *(Makofi)*

Pili, kuhusu Bwana *Peter Stone,* pia napenda kusema kwamba, nakubaliana naye Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna Mtanzania amegundua na hili jiwe linajukulikana katika baadhi ya sehemu kwa jina lake, ni vizuri akatambulika vizuri na mimi nakubaliana naye Mheshimiwa Mbunge, kwamba baada ya kupitia kwa kina zaidi taarifa zake, basi tunaweza tukatafuta utaratibu ambao huyu Bwana Peter anaweza akajulikana kwamba pia na yeye ni mmoja wa watu maarufu katika suala la madini. Lakini nilikuwa nikijibu hapa lilikuwa ni suala la jina rasmi la yale mawe. Si kwamba hatambuliki kama mchimbaji hapana, nilikuwa nazungumzia suala la jina mahsusi. Lakini nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba pale panapotokea Mtanzania amejitokeza na kugundua basi ni vizuri akapewa heshima yake kama kweli yeye ndiyo mgunduzi wa suala hilo. *(Makofi)*

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Waziri atakubaliana nami kwamba ingawa ni kweli kwamba kuna watu wanaotengeneza madini haya ya *Gemestones* ambazo siyo maliasili halisi wanayauza. Lakini anakubaliana na mimi kwamba wanunuzi na wakataji dunia nzima na watumiaji bado wanatambua madini ambayo ni halisi na siyo yale ya bandia viwandani na kwamba bado wanapata bei nzuri, kwa hiyo hakuna sababu ya kuacha kuchimba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hakulipata sawa sawa swali Mheshimiwa Naibu Waziri, ni ruksa kulirudia.

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Ningependa kurudia kusema hivi, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna watu au kuna utalaam wa kutengeneza madini bandia, siyo yale halisi, je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba wakataji na wauzaji na watumiaji yaani wanaovaa madini haya bado wanatambua madini halisi na bado ndiyo yanayopendwa kuliko ya bandia na kwa hiyo, Serikali yetu ingeendelea kuhimiza uchimbaji wa madini haya?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kabisa Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kwamba Serikali yetu iendelee kuhimiza uchimbaji wa madini na kwamba pamoja na kwamba zipo jitihada na kuna baadhi ya madini yanayotengenezwa bandia, madini halisi ndiyo bado yanapendwa zaidi. Lakini na hii haiko katika madini tu hata ukija kwenye mazao mengine kama Mkonge, kuna wakati Mkonge watu walikuwa wanatengeneza *Synthetic Fibre* lakini sasa hivi watu wanaona kwamba kwa kweli mkonge halisi ni bora zaidi kuliko *Synthetic Fibre.* Kwa hiyo, hii inapita katika awamu za mambo haya wakati fulani. Lakini nakubaliana naye mia kwa mia kwamba ni muhimu tukaendelea na uchimbaji huo. *(Makofi)*

Na. 322

**Utafiti wa Madini**

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa mingi ilifanyiwa utafiti na kuonekana na madini ya aina mbalimbali ambayo mengi yamepata wawekezaji na wananchi kupata ajira katika migodi hiyo:-

(a) Je, Mkoa wa Dodoma ulishafanyiwa utafiti wa madini?

(b) Je, kama umefanyiwa utafiti ni aina gani ya madini yaliyopo na yako wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma ulishafanyiwa utafiti wa madini kuanzia mwaka 1935 hadi 1996. Utafiti uliofanyika ni wa hatua za awali ambapo uliwezesha uchoraji wa ramani za kijiolojia za mkoa mzima zinazoonyesha aina za miamba na sehemu zenye dalili za madini.

Mheshimiwa Spika, aina ya madini na mahali yalipo ni Dhahabu ipo katika maeneo ya Nzunguni, Simbanguru na Chikuyu, Shaba *(copper)* maeneo ya Tambi, Winza, Mlali na Mlima wa Mautya, Jasi *(Gypsum)* iko maeneo ya Msagali, kuna madini yanaitwa *Diatomaceous Earth* maeneo ya Ilindi, *Magnesite* maeneo ya Kikombo na vilima vya Mwahanza, Iyobo na Mnakura, *Phosphate* maeneo ya milima ya chali, Chokaa *(limestone)* maeneo ya Iringa - Mvumi, Iduo - Mlali, Chamwino, Mbwanga na Goima, Tale *(Soapstone)* vilima vya Kikaza na Mahoma Makulu, chumvi maeneo ya Kigwe na Bahi, Madini ya vito kama *(Soaplite, Moonstone, Peridot, Garnet, Ruby, Opal* na *Chrysoprase)* maeneo mbalimbali ya Wilaya za Mpwapwa, Kondoa na Kongwa, yakiwepo Itiso na Haneti, *Uranium* maeneo ya Bonde la Bahi na kadhalika.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Sasa kumbe Dodoma vile vile tuna madini tena ya aina nyingi sana. Sasa naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Serikali itaweka mikakati ya kuhakikisha maeneo hayo yanapata wafadhili na madini hayo yanachimbwa ili kuiletea nchi mapato ya fedha? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kusema kwamba kwa hivi sasa yako baadhi ya makampuni yamejitokeza kutafiti madini na kutaka kuchimba madini haya. Tumeshatoa leseni sasa hivi kama 20 za utafutaji na uchimbaji wa madini hapa na miongoni mwake ni *Madinga Mining Enterprises, Shantac Mining Company, Centre Mining Company, Tentac Development Company* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hawa zipo pia leseni ndogo ndogo. Labda ningekuja kwenye swali moja kwa moja kwamba kwa ushahidi huu na pia kutokana na hatua ambayo Serikali imechukua ya kufungua Ofisi ya Madini hapa Dodoma baki ya kwamba Ofisi ya kanda iko Singida, lakini pia tumefungua ofisi ya madini hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi katika kuhakikisha kwamba inatangaza madini haya, inahamasisha wawekezaji ili waweze kuingia katika maeneo haya. Lakini kama tunavyofahamu hatimaye uamuzi wa mwisho kwa kweli unakuwa ni wa wale wawekezaji wenyewe. Kazi ya Serikali ni kutoa vivutio na kutoa uhamasishaji ili waweze kuingia katika maeneo hayo ya uchimbaji. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Naibu Waziri swali moja.

Je, anafahamu kwamba hawa wachimbaji ambao wako tayari katika Mkoa huu wanaondoa madini bila udhibiti wowote? Je, anafahamu hilo na kama anafahamu anachukua hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimewahi kusema katika Bunge lako Tukufu mara nyingi, ni kwamba Serikali kupitia kwa utaratibu uliopo imeweka Maafisa wa Madini katika maeneo mbalimbali na inatumia taratibu mbalimbali za kuhakikisha kwamba kuna udhibiti katika suala zima la utafutaji na uchimbaji wa madini. Lakini kama Mheshimiwa Mbunge yeye anazo taarifa mahsusi ambazo sisi Serikalini hatuna, kwa kweli nitakuwa radhi kushirikiana naye ili tuhakikishe kwamba tatizo ambalo amelisema na ninaamini kwamba kwa uzito wake lazima kutakuwa na matatizo ya aina fulani, basi atufahamishe ili sisi tukirishikiana naye na wananchi kwa ujumla, tuweze kuchukua hatua za kufaa. *(Makofi)*

Na. 323

**Maombi ya Simu za *Celtel* - Mahenge**

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alipozindua simu za *Celtel* kwenda Kilombero na Ifakara alipokea ombi la Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kufikisha mawasiliano ya *Celtel* Makao Makuu ya Wilaya Ulanga, Mahenge:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani ombi hilo linatekelezwa?

(b) Je, Serikali inaweza kutamka simu za *Celtel* zitafika Mahenge kabla ya Bunge hili la Bajeti 2003 kumalizika?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wataalamu wa masoko wa Kampuni ya *Celtel* kwa kushirikiana na Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, wamefanya tathmini ya soko yaani *Field Marketing*

*Survey* ya simu za mkononi katika Wilaya ya Ulanga. Hii ni hatua ya mwanzo kabisa katika taratibu za kuepeleka huduma za simu au huduma nyingine popote pale. Hatua nyingine ambazo zinalenga katika kutathmini mambo ya kiufundi, kibiashara, kijamii na kimazingira zimeanza kabla ya kujenga Kituo cha simu yaani *Base Transceiver Station* hapo Mahenge.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inaahidi kumpa Mheshimiwa Mbunge taarifa za kila hatua ambazo kampuni ya *Celtel* na kampuni nyingine za simu zitakuwa zinachukua ili kufikisha mawasiliano ya uhakika ya simu za mkononi Wilaya ya Ulanga. Wilaya ya Ulanga imo katika mpango wa Awamu ya Tatu ya mpango wa *Celtel* wa kupeleka mawasiliano hapo Wilayani.

Mpango huu utaanza kutekelezwa mara tu utakapopitishwa na Bodi itakayokutana hivi karibuni. Matarajio yetu ni kwamba, Mahenge itakuwa imepata huduma za *Celtel* wakati wowote kuanzia mwisho wa mwaka 2003 na katikati ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua mchango na jitihada za Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira katika kuboresha huduma za Sekta ya Mawasiliano. Sio tu Ulanga na Ulanga Mashariki, bali kwa nchi nzima.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ambayo yanatia moyo, lakini kwa sababu ya aina fulani hivi, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ni kwamba *Celtel* ni Kampuni tanzu ya *TTLC,* kwa hiyo, Serikali yetu ina hisa asilimia 67. Je, Waziri anaweza kuwathibitishia wananchi wa Mahenge kwamba atawasiliana na Meneja wa *Celtel* ili kabla ya Bunge lijalo la mwezi Novemba simu ziwe zimefika Mahenge? Hii ni ya kwanza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili, wananchi wa Kilombero na wananchi wa Ulanga ni Wilaya moja na ni ndugu, hivi sasa tunavyozungumza *Celtel* na *Vodacom* wako Ifakara. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii inapunguza maendeleo ya wananchi wa Wilaya ya Ulanga, kwa hiyo, simu ya *Celtel* ingekwenda. Nasema tena, kabla ya Bunge lijalo? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *Celtel* ni Kampuni tanzu ya *TTCL* na si kwa sababu hiyo, lakini ni kwa sababu ni wajibu wangu, nimewasiliana na nitaendelea kuwasiliana na *Celtel* kuhusu simu za mkononi Mahenge kama nitakavyofanya kwa simu za mkononi sehemu nyingine nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezekano wa simu kupatikana Mahenge kabla ya Novemba, mwaka huu, naomba aridhike na jibu langu kwamba nina uhakika simu zitapatikana kati ya Desemba, 2003 na Juni, 2004. Lakini kwa jitihada anazofanya Mheshimiwa Mbunge na msukumo wa Wizara, uwezekano huo upo, lakini sipendi kutoa ahadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili linalohusu wananchi wa Kilombero na Ulanga kuwa ni wamoja, ni kweli Kilombero tayari wameshapata huduma za *Vodacom* pamoja na *Celtel,* lakini kama ninavyofahamu Mheshimiwa Mbunge, kutangulia si kufika. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu *Celtel* Wilaya ya Ulanga. Sasa wengine hamtoki Ulanga. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Beatus Magayane. *(Kicheko/Makofi)*

324

**Mafao ya Wafanyakazi *ZTRS***

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu mwaka 1985 *Zambia and Tanzania Road Services (ZTRS)* iliyovunjwa hadi sasa wanyakazi watanzania wapato 476 waliokuwa wanafanya kazi katika Kampuni hiyo bado hawajalipwa mafao yao na kwa kuwa Mfilisi aliyeteuliwa mwanzo yaani *Coopers and Lybrand* aliamuliwa na

Mahakama kuwalipa wafanyakazi hao mafao yao na kwa kuwa mfilisi huyo hakutekeleza amri hiyo ya Mahakama na kwa kuwa sasa mfilisi huyo hayupo tena:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu ulipwaji wa mafao ya wafanyakazi hao?

(b) Je, *Price Water House* ambayo ilijibadilisha kutoka kwa mfilisi *Coopers and Lybrand* na ambayo kwa kufanya hivyo ni *successor* wa *Coopers and Lybrand* imeshughulikia vipi ulipaji wa mafao hayo?

(c) Je, ni lini wafanyakazi hao watalipwa hususan ikizingatiwa kwamba mali zote za Kampuni hiyo zimekwishauzwa na Mfilisi *Coopers and Lybrand?*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Magayane, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufilisi wa *Zambia, Tanzania Road Services Limited* ulianza tarehe 8 Agosti, 1985 chini ya Mfilisi aliyeteuliwa kisheria yaani *Coopers and Lybrand* wa Zambia na *Coopers and Lybrand Tanzania* ambapo Makao Makuu yake yaani Makao Makuu ya Mfilisi yalikuwa Zambia na Tanzania ikiwa tawi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba jumla ya shilingi milioni 39.9 zililipwa kama mafao yote ya waliokuwa wafanyakazi wa Kampuni hiyo. Kila mmoja alilipwa haki zake zote ambazo aliapa kuwa anadai kwenye fomu maalum yaani *proof of debt form* na kwamba hatadai kitu kingine chochote. Ili kuwapunguzia usumbufu waliokuwa wafanyakazi, Mfilisi alipendekeza utolewe upendeleo maalum kwa wafanyakazi hao ili walipwe mapema kabla ya wadai wengine. Mapendekezo hayo yalikubaliwa na Serikali kama mdai mkubwa wa Kampuni hiyo na kupitishwa kisheria Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupokea fedha hizo, baadaye wafanyakazi waliwasilisha mashtaka yao Mahakama Kuu wakidai kwamba walipwe shilingi milioni 86 kwa sababu ya kucheleweshewa mafao yao na Mfilisi. Hivyo, walitaka walipwe pamoja na mambo mengine, posho ya kujikimu yaani *subsistence allowance* kuanzia muda wa tarehe ya ufilisi hadi walipolipwa mafao yote.

Mheshimiwa Spika, Hukumu ya Kesi ya Madai Na.189 ya mwaka 1989 ilitolewa na Mahakama Kuu tarehe 12 Februari, 1991. Kwa bahati mbaya wafanyakazi hao walishindwa. Wafanyakazi hao hawakuridhika na wakaenda Mahakama ya Rufaa Tanzania, katika Hukumu ya Kesi ya Rufaa ya Madai Na.5 ya mwaka 1995. Mahakama ya Rufaa katika hukumu yake iliyotolewa tarehe 23 Oktoba, 1995 ilitupilia mbali madai hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Beatus Magayane, ni la msingi sana hasa kwa maana ya kusisitiza umuhimu wa kutambua na kutoa haki kwa wafanyakazi wakati Kampuni au Mashirika yanapofilisiwa au kubinafsishwa. Namwomba tuendelee kushirikiana katika maswali kama haya na mengine katika Sekta ya Uchukuzi.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya kina. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Watanzania wanaofanya kazi katika vyombo vya pamoja wamekuwa vinapovunjwa hawalipwi wakati wenzao wa upande mwingine wamelipwa kama ilivyokuwa kwa *East African Community,* waliokuwa wafanyakazi wa Bandari na *Community,* je, hii haionyeshi kwamba Serikali haiko makini katika kutetea wafanyakazi wake ambao wako upande wa pili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kunakuwa na usumbufu mkubwa pale ambapo Kampuni au Shirika linamilikiwa na nchi mbili au tatu na hasa wakati ambapo linafilisiwa au linavunjwa. Haya ndio matatizo ya kuwa na ngazi mbili kufuatana na taratibu

kushughulikia Serikali moja halafu na Serikali nyingine, sheria moja na sheria nyingine. Hili hatuwezi kulizuia, tutakalofanya hapo baadaye ni kujaribu kuwa makini tu kuyazingatia haya mambo kabla ya kuingia katika Mikataba.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Beatus Magayane, kwamba Serikali kwa suala hili la wafanyakazi wa iliyokuwa Kampuni ya *Zambia Tanzania, Road Services,* ilikuwa makini sana, ndio maana Hazina ya Serikali ya Tanzania ilitoa fedha shilingi milioni 30 kati ya zile nilizozitaja katika jibu langu la msingi ili kuwalipa hawa wafanyakazi. Kwa sababu kulikuwa na matatizo ya kwamba mali yote au sehemu kubwa ya mali ilikuwa Zambia, lakini sehemu kubwa ya madeni ilikuwa Tanzania. *(Makofi)*

Na.325

**Bei ya Pamba**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya pamba imekuwa ya wasiwasi kwa wakulima wa zao hilo kwa takriban miaka kumi iliyopita:-

(a) Je, kwa sasa bei ya Soko la Dunia ni shilingi ngapi kwa kilo moja ya pamba *Lint* kwa miezi ya Juni - Julai, 2003?

(b) Je, mkulima wa Tanzania atalipwa kiasi gani kama atalipwa kwa asilimia 65 ya bei ya Soko la Dunia kwa bei ya Juni - Julai, 2003?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kati ya mwezi wa Juni na Julai, 2003 cha msimu uliomalizika, bei ya pamba nyuzi katika Soko la Dunia ilikuwa Dola za Kimarekani 0.88 au Senti 88 za Dola za Kimarekani kwa kilo moja ya pamba nyuzi ambayo ilikuwa sawa na Sh. 880/= kwa kilo moja ya pamba nyuzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uwiano kati ya pamba mbegu na pamba nyuzi wa 3:1 na kama mkulima atalipwa asilimia 65 ya bei ya Soko la Dunia mkulima angestahili kulipwa bei isiyozidi shilingi 190.60 kwa kilo kulingana na bei ya pamba nyuzi katika Soko la Dunia ambayo ni sawa na takriban shilingi 880/= kwa kilo. Kwa msimu mpya, wadau wamekubaliana kwamba bei ya pamba mbegu yaani *Floor Price* isiwe chini ya shilingi 225/= kwa kilo ya pamba daraja la kwanza na shilingi 100/= kwa pamba ya daraja la pili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na takwimu hizi kuonyesha matarajio mema, bado hali halisi inaweza kuwa tofauti kutegemeana na vigezo vingine vinavyoweza kujitokeza na kuathiri mwenendo wa soko na bei.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza, lenye sehemu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa sasa hivi bei ya pamba kwa msimu huu ni kati ya shilingi 260/= na shilingi 300/= kitu ambacho ni *gap* kubwa sana, je, Serikali kwa nini isiwe na tamko la kuonesha kwamba mmoja asipunjwe anayenunuliwa kwa bei ya shilingi 260/=?

(b) Kwa kuwa sasa hivi mazao mengi hapa nchini tuna muda wa miaka kumi bei yake ikiwa ya wasiwasi na Serikali haijaonyesha msimamo wake kwamba kwa nini mazao haya ambayo yanatuletea fedha nyingi za kigeni yasiwekewe msimamo mzuri na hata kutafuta bei ambayo itakuwa ya soko zuri, je,

Serikali ina mpango gani au ina jitihada gani ya kuweza kufanya hata wakulima wawe na moyo wa kulima kwa sababu wanatumia nguvu nyingi lakini wanapata kiasi kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kama anavyosema kwamba bei ya pamba sasa hivi ni kati ya shilingi 260/= na shilingi 300/=. Lakini kusema kweli ndio taarifa rasmi ambayo hata sisi wenyewe tunayo kwamba bei hiyo ndiyo inayoendelea hivi sasa. Kama nilivyokuwa nimesema katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba pamoja na ile bei niliyokuwa nimeitaja, lakini inaweza ikawa inabadilika kwa kadri mambo mengine yatakapokuwa yanajitokeza kutokana na mwenendo wa soko.

Sasa kuhusu kwa nini Serikali isitamke ili watu wengine wasipunjwe, katika utaratibu wa soko huria ambapo tunategemea sana nguvu za soko, Serikali haiwezi ikatamka bei sasa ikasema kwamba bei itakuwa ni kiasi fulani, isipokuwa cha msingi tunachokitegemea ni kuhakikisha tu kwamba wakulima wanaboresha mazao yanayostahili katika soko na hatimaye wale watakaokuwa wanatoa mazao bora zaidi wanaweza wakapata bei nzuri kama ambavyo imejionyesha hapa kati ya shilingi 260/= na shilingi 300/=.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusiana na mazao mengine ambayo hayapati bei nzuri, kama nilivyokuwa nimeshaeleza awali kwamba hivi hivi sasa tunachokifanya ni kuhakikisha tu kuwasimamia wakulima wetu waweze kuongeza ubora wa mazao ili yaweze kuvutia bei zaidi. Lakini isitoshe tunadhani kabisa kwamba ili mazao yetu yaweze kupata bei ya mvuto, tunasisitiza zaidi suala la kubangua mazao yetu ama kuyasindika ili yaweze kuongezea ubora wa thamani na hatimaye kupata bei nzuri zaidi.

**SPIKA:** Wakulima wa pamba nawaona, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara ya Ushirika na Masoko ina majukumu pamoja na kumsaidia mkulima wa pamba, mkulima wa pamba miaka yote amekuwa na matatizo sana ya bei ya pamba na mwaka jana alipata matatizo ya mbegu kutokuota, je, Wizara ya Ushirika na Masoko inamsaidiaje mkulima wa zao la pamba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu bei, sasa nadhani hilo ni jipya. Mheshimiwa Raphael Mlolwa.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika mazingira ya sasa ya uchumi wa soko, baadhi ya wanunuzi wa pamba hujifanya kuongeza bei za pamba za wakulima wakati wamekuwa tayari wamezikorofisha hizo mizani na kuonyesha kwamba hawapati bei halali.

Je, Wizara ya Ushirika na Masoko, itashirikianaje na Taasisi inayohusiana na Vipimo na Uzito kuhakikisha kwamba kunakuwa na mkakati wa kuonyesha kwamba wakulima hawapunjwi zao lao la pamba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba kuna baadhi ya wanunuzi ambao si waaminifu na hatimaye wanafanya vitendo ambavyo vinawahujumu wakulima.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali kama Wizara pamoja na Bodi ya Pamba ni kusimamia taratibu zilizowekwa katika mfumo wa ununuzi wa mazao yote ikiwemo pamba.

Kwa hiyo, kwa upande wangu tu ningeweza nikasema kwamba Serikali inahimiza vyombo vyote vinavyohusika ikiwemo Bodi ya Pamba, Halmashauri za Wilaya na sisi wenyewe viongozi kwa ujumla, kufichua watu ambao sio waaminifu katika kuwahujumu wakulima ili tuweze kusaidiana katika kuwafichua na hatimaye kurekebisha tabia zao ili mkulima aweze kupata bei ambayo ni ya haki. *(Makofi)*

Na.326

**Fedha za *STABEX***

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na maelezo ya kwamba Umoja wa Ulaya ulitoa fedha za *STABEX* kwa ajili ya kusaidia kupunguza matatizo yaliyotokana na kuyumba kwa Soko la Kahawa.

Je, Umoja wa Ulaya umetoa fedha kiasi gani za *STABEX* na fedha hizo zimetumika vipi kusaidia kupunguza matatizo yaliyotokana na kuyumba kwa soko la kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyoeleza katika kuhitimisha hotuba yake ya bajeti ya tarehe 20 Juni, 2003, Umoja wa Ulaya chini ya utaratibu wa *STABEX* ya miaka ya 1994 hadi 1999 pamoja na mabaki ya miaka ya 1990, 1991, 1992 na 1993 umetoa jumla ya *Euro* 38,440,413 sawa na takriban fedha za Kitanzania shilingi bilioni 42 kuendeleza Sekta ya Kilimo cha Zao la Kahawa Nchini. Tofauti na utaratibu wa awali ambapo wakulima walilipwa fedha taslimu, umoja huo sasa umebadili utaratibu wa kufikia makubaliano na Serikali ya Tanzania kwamba fedha hizo za *STABEX* zitatumika katika maeneo yafuatayo:-

(i) Utafiti wa kahawa unaofanywa na Taasisi Utafiti wa Zao la Kahawa *(TACRI)* iliyopo Lyamungo, Moshi. Jumla ya *Euro* milioni 9.0 ambayo ni sawa sawa na shilingi 10,800,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya kazi hii.

(ii) Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Kilimo Nchini *(Agricultural Sector Development Program)* ambapo jumla ya *Euro* milioni 18.0 sawa na shilingi 21,600,000,000/= zimetengwa.

(iii) Kuimarisha barabara za Vijiji katika maeneo yanayozalisha kahawa. Jumla ya *Euro* milioni kumi sawasawa na fedha za Kitanzania Shilingi bilioni 12 zimeidhinishwa kwa shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli hizo, jumla ya *Euro* milioni 1.44 sawa na fedha za Kitanzania shilingi 1,728,000,000/= zimetengwa kugharamia Washauri Waelekezi kwa ajili ya kuratibu, kukagua, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu niliyokwishayaeleza.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu haya ambao utaanza katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 unalenga katika kuendeleza Sekta ya Zao la Kahawa kwa kuboresha uzalishaji pamoja na kukuza Sekta ya Kilimo kwa ujumla kwa kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini yaani *ASDP*. Aidha, uimarishaji wa barabara za Vijijini utapunguza gharama za kusafirishia kahawa na mazao mengine na hivyo kuwaongezea kipato wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina zaidi kuhusu *STABEX* yatatolewa na Serikali kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoahidi hapa Bungeni wakati Hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula ilipohitimishwa.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo yote sikubaliani nayo, nina maswali madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba itatoa maelezo ya kina hapa Bungeni na kwa kuwa unavyozidi kuchelewesha, lolote linaweza likatokea kwa sababu ya muda, je, ni lini sasa Serikali inaweza ikatuhakikishia kwamba itakuwa tayari ili ilete Bungeni hapa maelezo ya kina?

Kwa kuwa kwa hivi sasa tuko katika uchumi wa soko na kwa kuwa katika uchumi wa soko jambo pekee la kumpa motisha mkulima ni mapato anayoyapata na kwa kuwa *STABEX* fedha ilitolewa kwa sababu ya kuporomoka kwa bei ya kahawa; Je, ni kwa nini Serikali ilishindwa kuwashawishi wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya ili waelewe umuhimu huo na kwa hiyo wakubali fedha hizo zipewe wakulima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla hujajibu, nieleze kwamba *Order Paper* ya kesho Jumanne itakuwa na nafasi ya maelezo ya *STABEX* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Atajibu yaliyobaki Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kusema kweli nakushukuru kwa kutoa maelezo hayo hivi sasa kwa sababu swali lilikuwa limehusu kwamba ni lini maelezo yatatolewa. Nakushukuru kwa kunisaidia kusema kwamba maelezo yatatolewa muda wowote. Lakini ningemshauri tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa hayo maelezo yatakayotolewa kesho na Waziri wa Kilimo na Chakula, nadhani tungesubiri basi tuweze tukaona kama yanaweza yakakidhi au la.

Na.327

**Serikali Kuyatoa Magari yaliyoshindikana Kukombolewa Bandarini kwa Jeshi la Polisi Nchini**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la ujambazi nchini na kwa kuwa Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri ya kupambana na uhalifu na mifano mingi ipo dhahiri lakini hawana usafiri wa kutosha katika kupambana na vitendo hivyo viovu na kwa kuwa Serikali huyauza magari ambayo yameshindikana kukombolewa Bandarini:-

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitatu, Serikali imeuza magari mangapi?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ni busara kuwapa Jeshi la Polisi magari hayo ili wakabiliane na wimbi hilo la ujambazi ambalo linawakosesha wananchi amani?

**NAIBU WA WIZARA YA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kipindi cha miaka mitatu (2000 - 2003) Serikali, kupitia Mamlaka ya Mapato imeuza magari 108 kwa minada ya hadhara.

(b) Magari yanayouzwa na Mamlaka ya Mapato kutokana na walioyaingiza nchini kushindwa kuyalipia ushuru yanakuwa bado ni mali ya waagizaji. Kwa hiyo, fedha inayopatikana katika mauzo hayo hulipwa kwa mwagizaji baada ya kutoa ushuru, kodi na gharama nyingine. Iwapo Serikali itataka kuyachukua kwa matumizi yake, inalazimika kushiriki katika mnada wa wazi na kulipa fedha halisi ikiwa itashinda katika mnada. Serikali inaamini kwamba ni bora kutenga bajeti ya kununua magari mapya kwa ajili ya Jeshi letu la Polisi kama inavyofanya kila mwaka kuliko kununua magari machakavu mnadani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ongezeko la matukio ya ujambazi na vitendo vingine vya uhalifu, Bajeti ya mwaka huu 2003/2004 imeongeza fedha kwa ajili ya vyombo vya usalama ili kuvipa uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa aina zote. Idara ya Polisi imetengewa shilingi milioni 70,786 ukilinganisha na shilingi milioni 55,178 mwaka wa fedha uliopita 2002/2003. Hili ni ongezeko la asilimia

28.3. Katika Bajeti hii ya mwaka huu wa fedha Polisi wametengewa shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kununua magari mapya ya kupambana na ujambazi kwa njia mbalimbali.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri hasa kwa kutenga hela za kutosha, lakini nina swali dogo tu.

Kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi ya ujambazi hasa Vijijini na kwa kuwa Vituo vingine vya Vijijini vinafanya kazi nzuri hata bila kuwa na vitendea kazi, je, Waziri katika Bajeti hiyo atakubaliana na mimi kuwa hata Vituo vya Vijijini wangepata angalau pikipiki au baiskeli za kusaidia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika Bajeti yetu ambayo ilipitishwa wiki mbili zilizopita, tulieleza mipango mbalimbali ya kununua vifaa kwa ajili ya Jeshi la Polisi na Vituo vya Vijijini viko vingi sana na vinahitaji pikipiki, baiskeli na vifaa Vinginevyo. Kwa hiyo, kwa kadri hali ya Bajeti inavyoruhusu, tutajitahidi kusambaza vifaa hivyo, lakini hatutaahidi moja kwa moja kwamba na Vituo vyote katika Jimbo la Mheshimiwa Paul Ntwina, lakini jitihada za Serikali zitafanyika kusambaza vifaa hivyo kwa kadri hali ya Bajeti itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Na.328

**Punguzo la Kodi kwa Mazao Yanayoathirika na Kushuka kwa Bei**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na wimbi la kushuka kwa bei ya mazao ya biashara kama vile kahawa, korosho, pamba na kadhalika katika Soko la Dunia na kwa kuwa kodi za Serikali Kuu na zile za Serikali za Mitaa katika mazao hayo zimebaki pale pale:-

(a) Kwa lengo la kuhamasisha kilimo cha mazao, je, ni kwa nini Serikali haiwapi wakulima punguzo kubwa la kodi za Serikali Kuu na zile za Serikali za Mitaa katika mazao yaliyoathiriwa na kushuka kwa bei ya Soko la Dunia?

(b) Je, ni kwa nini Serikali haiwapi wakulima *Tax Holiday* kwa kufuta kodi zote za mazao husika hadi hapo bei katika Soko la Dunia itakapokuwa nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini mchango mkubwa unaotolewa na Sekta ya Kilimo hasa wakulima wanaozalisha mazao ya biashara kwa ajili ya Soko la Nje katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Ni kwa misingi hiyo Serikali imeona umuhimu wa kuondoa kodi za mauzo ya bidhaa za nje *(Export Tax)* tangu mwaka 1997.

Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Serikali imeweka utaratibu wa kufidia kodi ya *VAT* kwa wakulima wakati wa kusafirisha, kusindika na kwenye vifungashio vya mazao yauzwayo nje ya nchi, inapokuwa nafuu hii ya *VAT* inatolewa tu kwa wakulima kupitia vyama vya ushirika au vyama vyao ambavyo vimesajiliwa na *TRA* kwa madhumuni hayo. Serikali inawashauri wakulima wa mazao kujiunga pamoja kwa kufuata taratibu zinazoshauriwa ili wafaidike na nafuu hii ya kodi.

Vile vile kwa upande wa Serikali za Mitaa, Serikali imeweka ukomo wa kodi wa asilimia tano thamani *(fob-free on board)* kwa mazao ya biashara ya kilimo. Marekebisho yote hayo yana lengo la kuhamasisha uzalishaji wa mazao hayo na kuongeza kipato cha mkulima. Aidha, Serikali katika mwaka

ujao wa fedha ina mipango wa kufuta baadhi ya kodi za Serikali za Mitaa ambazo ni kero kwa wakulima na wananchi wa jumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi za Serikali, ni dhahiri kwamba bei za mazao ya wakulima wetu zinategemea zaidi hali ya Soko la Dunia. Serikali, ikishirikiana na nchi na wadau wengine hasa katika nchi zinazoendelea, inaendelea kupinga hali ya unyonyaji katika soko la Dunia la mazao ya kilimo. Vile vile Serikali inapinga hatua za nchi zilizoendelea kutoa ruzuku kwa wakulima wao, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni za biashara za Kimataifa na linaathiri sana uwezo wa wakulima katika nchi changa kuuza katika masoko ya nje.

Mwisho, Serikali inawahamasisha wawekezaji wa hapa nchini kuwekeza katika usindikaji wa mazao yetu hapa hapa nchini ili kuongeza thamani ya mazao yetu na hivyo kuweza kumlipa mkulima bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia bei duni za mazao na unyonge wa mkulima, Serikai imefuta kodi ya maendeleo ya ushuru wa aina toka aina 60 hadi 7, ili kumpa unafuu katika maisha kwa ujumla. Hii ni likizo nzuri zaidi ya kodi kuliko anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge, kwani wananchi, wakulima na wafanyakazi.......

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Naipongeza sana Serikali kwa hatua ambazo imechukua mpaka sasa. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Sekta ya Kilimo ndiyo sekta kiongozi katika kukuza uchumi wetu na mkakati wa kuondokana na umaskini, je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha kilimo na kukuza uchumi wake kwa kutoa ruzuku kwa wakulima wetu?

Je Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo yenye masharti ambayo yanalingana na hali halisi ya wakulima wetu wadogo wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Singo, kuwa katika Bajeti ya Waziri wa Fedha, aliyowasilisha hapa Bungeni, kuna hatua ambazo zinachukuliwa za kutoa ruzuku kwa ajili ya Mikoa ya Kusini inayozalisha mahindi, kwa hiyo, ruzuku ipo lakini pia kuna mipango ambayo inatoka katika kila Halmashauri, Halmashauri zote zichague zao moja la biashara moja la kilimo ambalo litasaidiwa kupatiwa ruzuku. Kwa hiyo, ruzuku katika Bajeti ya mwaka huu ipo na hii ina nia ya kusaidia kuongezeka kwa mazao ya chakula pamoja na biashara.

Mheshimiwa Spika, pia katika Bajeti ya mwaka huu, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kusaidia wale wanaotaka kukopa kwenye kilimo, uvuvi, biashara ndogo ndogo na viwanda vidogo. Kwa hiyo, hili linazingatiwa lakini kadri ambavyo hali yetu ya uchumi itakuwa inaboreka nafuu zaidi ama ruzuku zitaendelea kutolewe katika kuboresha uzalishaji mazao mbalimbali ya biashara na ya chakula katika Mikoa na Wilaya mbalimbali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika. Vikao vya leo ni kama ifuatavyo:-

Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Salome Mbatia, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, wakutane leo Jumatatu tarehe 28 Julai, 2003 saa 5.30 asubuhi chumba namba 58.

Kamati ya pili, ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Kamati ikutane saa 5.00 asubuhi chumba namba 56. Kikao kisichokuwa cha Kamati ni kikao cha Wajumbe wote Wanawake *(TWPG),* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba niwatangazie kwamba kutakuwa na kikao leo kuanzia saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha shughuli za Bunge leo asubuhi chumba namba 56.

Si kikao lakini ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Tume ya Huduma ya Bunge, Makamishna wa Tume, tukutane kwa muda mfupi katika *Lounge* ya Spika baada ya Waziri anayetoa hoja leo kutoa hoja yake. *(Makofi)*

Ufafanuzi katika *Order Paper* ya leo mtaona kuna Miswada sita inayosomwa Mara ya Kwanza. Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amenieleza kwamba Serikali sasa inaanza kutekeleza maombi ya Wabunge ya siku nyingi kwamba wapate Miswada mapema wakaisome kujiandaa kuijadili baadaye. Sasa hii Miswada inasomwa Mara ya Kwanza, lakini itajadiliwa Mkutano ujao. Kwa hiyo, ni nafasi nzuri kwa Wabunge kuipata, waisome ili kujiweka tayari. *(Makofi)*

Maombi ya kutaka wapewe Miswada mapema yamekuwa ya siku nyingi sasa hii ndiyo njia ya kuwapatia Wabunge Miswada mapema. Inasomwa Mara ya Kwanza lakini haijadiliwi.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa Mwaka 2003 *(The Merchant Shipping Bill, 2003).***

**Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2003 *(The Coopoerative Societies Bill, 2003).***

**Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Huduma ya Wanyama wa Mwaka 2003 *(The Veterinary Bill, 2003).***

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Magonjwa ya Wanyama wa Mwaka 2003 *(The Animal Diseases Bill, 2003).***

**Muswada wa Sheria ya Kuunda Chombo cha Majadiliano ya Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi katika Sekta ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2003 *(The Public Service Negotiating Machinery Bill, 2003).***

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Viwango vya Mbegu wa Mwaka 2003 *(The Seeds Bill, 2003).***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004**
**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba nitumie fursa hii kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa jumla kwamba mwezi Oktoba, 2002, Mheshimiwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliridhia ombi la kubadilisha jina la Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu inafahamika kwa jina la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na umuhimu wa watoto ambao ni Taifa la kesho, imekubalika kuundwa kwa Idara ya Maendeleo ya Mtoto.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kilichokuwa Kitengo cha Habari na Mawasiliano, kimebadilishwa jina na sasa kinaitwa Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Jamii *(Community Information, Education and Communication Unit).*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara yangu ni haya yafuatayo:-

Kutayarisha Sera za Wizara na kusimamia utekelezaji wake, kuiendeleza, kuieneza na kuitekeleza dhana ya maendeleo ya jamii kwa kuwashirikisha wananchi wote, kuandaa programu, mikakati na mifumo ya utekelezaji ili kuchochea maendeleo ya wananchi wote, kuona kwamba wanawake na wanaume katika ngazi zote za Serikali, Mashirika ya Umma, Taasisi mbalimbali na jamii kwa ujumla wana uwezo na wanashirikiana katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo na kunufaika sawa na maendeleo yao, kuendeleza jamii ili iweze kuwapatia watoto wote haki ya kuishi, kulindwa, kutobaguliwa, kuendelezwa na kushiriki katika maendeleo ya Taifa na kusimamia utendaji kazi Wizarani kwa misingi ya uadilifu, haki na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, dira ya Wizara yangu ni kuwepo kwa jamii yenye uwezo thabiti wa kutambua matatizo yanayoikabili, kuyachambua na kuyawekea mikakati ya kuyatatua kwa kutumia raslimali zilizopo ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu ulifanyika kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kuondoa Umaskini, Sera ya Maendeleo ya Jamii, Sera ya Maendeleo ya Mtoto, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia na sera nyingine za Serikali kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga Taifa linalojitegemea, Wizara yangu imetafsiri Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii katika lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu utawawezesha wataalam, wananchi na wadau wengine kuandaa programu na miradi ya maendeleo kwa kutumia mbinu shirikishi ambayo itawajengea uwezo na kuwapa nafasi zaidi ya kushiriki katika mchakato mzima wa kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wataalam wa maendeleo ya jamii ni wawakilishi wa watu katika jitihada mbalimbali za maendeleo yao ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na hata kiutamaduni. Wataalam hawa huwasaidia watu kwa kuwapatia elimu, ujuzi na stadi mbali mbali ambazo hatimaye zitawawezesha kubadili fikra, mwelekeo na mitazamo yao ili iwiane na mahitaji ya maendeleo kwa wakati uliopo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika wakati tulionao watu hawana budi kujielekeza zaidi katika kukuza uchumi, kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha upatikanaji wa huduma za jamii na raslimali ambazo ndiyo nyenzo zitakazosaidia kuiwezesha jamii kupambana na umaskini, rushwa, uharibifu wa mazingira na janga la Ukimwi linalotishia uhai wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa wanakuwepo wataalam wa kutosha wa maendeleo ya jamii, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya taaluma hiyo kwa ngazi za cheti na stashahada ya juu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Misungwi, Rungemba na Tengeru. Jumla ya wanachuo 63 walihitimu mafunzo ya stashahada ya juu katika Chuo cha Tengeru, wakiwemo wanawake 43 na wanaume 20.

Aidha, wanachuo 101 walihitimu mafunzo ya cheti katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Misungwi na Rungemba. Hali kadhalika, mwaka 2002/2003, Wizara iliendesha mafunzo ya rejea ya muda mfupi huko Kibaha kwa watumishi wa maendeleo ya jamii 79 kutoka mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Manyara, Mbeya, Pwani, Shinyanga, Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa wananchi juu ya maarifa na stadi mbali mbali kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58. Jumla ya wananchi 3,751 wakiwemo wanawake 1,353 na wanaume 2,398 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na jumla ya wananchi 5,255 wakiwemo wanawake 2,569 na wanaume 2,686 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

Aidha, katika kipindi hicho, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Bariadi, Kiwanda, Mabughai, Malampaka, Mlale, Musoma, Mwanva, Nandembo, Same, Sengerema, Sikonge na Uyole viliendesha mafunzo nje ya chuo *(outreach)* na jumla ya washiriki 4,021 wakiwemo wanawake 2,057 na wanaume 1,964 walipata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wizara yangu ilipeleka fedha za ukarabati mdogo mdogo kwa vyuo 16 kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka 2002/2003. Vyuo hivyo ni Bariadi, Buhangija, Chisalu, Kihinga, Kilosa, Mabughai, Monduli, Msaginya, Msinga, Munguri, Musoma, Nandembo, Ruaha, Sofi, Tango na Ulembwe. Aidha, vyuo vya Kilosa, Kisarawe, Njombe na Tango vilipatiwa fedha za kufanya ukarabati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, mhimili wa maendeleo ya jamii ni ushiriki wa jamii yenyewe. Kwa kutumia mbinu shirikishi, wananchi huwezeshwa kubuni, kupanga, kutekeleza, kuendesha na kuifanyia matengenezo miradi yao ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na miradi ya maji na usafi wa mazingira. Mbinu hii imeleta mafanikio makubwa katika mpango wa *HESAWA.* Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara yangu imetoa uzoefu huo kwa kushiriki katika maandalizi ya Sera ya Taifa ya Maji na kuhakikisha kuwa dhana ya *HESAWA* inazingatiwa katika Sera hiyo.

Aidha, Wizara yangu inashiriki kikamilifu katika maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji. Hali kadhalika, Wizara yangu ni mjumbe wa Kamati ya wataalam inayoelekeza utekelezaji wa mipango ya maji na usafi wa mazingira. Kupitia ushiriki huo, Wizara yangu imehakikisha kuwa dhana ya *HESAWA* imezingatiwa katika mipango ya maji na usafi wa mazingira katika wilaya za Handeni, Igunga, Iramba, Kilosa, Kiteto, Kondoa, Kongwa, Manyoni, Mpwapwa, Morogoro Vijijini, Rufiji na Singida Vijijini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Ukimwi ni la kijamii. Hivyo mapambano dhidi ya Ukimwi hayawezi kufanikiwa bila ya mwananchi mmoja mmoja, familia au jamii kubadili tabia na kuacha mila na desturi zinazochangia kuenea kwa virusi vya Ukimiw.

Kwa kuzingatia yote hayo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetoa Mwongozo wa Uundaji wa Kamati za Kudhibiti Ukimwi katika mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinaratibiwa na wataalam wa maendeleo ya jamii. Ili kuwawezesha wataalamu hao kutekeleza majukumu yao vizuri, mwezi Juni, 2003 Wizara yangu iliendesha mafunzo kuhusu masuala ya Ukimwi mjini Morogoro kwa wataalamu hao.

Vile vile, Wizara yangu iliendelea kusambaza Mkakati wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya Ukimwi kwa wadau mbali mbali wakiwemo wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa, Wilaya na Wakuu wa Vyuo vilivyo chini ya Wizara ili kuwapa ufahamu wa namna ya kujikinga na kuwakinga wanawake na watoto dhidi ya maambukizo ya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, mkakati huo uliwasilishwa na kujadiliwa kwenye warsha ya kuingiza masuala ya jinsia katika mipango ya kudhibiti Ukimwi iliyozijumuisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Warsha hiyo iliandaliwa kwa pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola na *UNIFEM* mwezi Machi, 2003.

Mheshimiwa Spika, ujumbe wa Tanzania kwenye warsha hiyo ulioongozwa na *TACAIDS,* ulikubaliana kuwa mkakati huo wa Kijamii wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya Ukimwi uimarishwe na usambazwe kwa wadau wote wanaojihusisha na vita dhidi ya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliwasilisha maelezo katika Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imeanza kutayarisha Mwongozo wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Wizara imetayarisha rasimu ya mwongozo huo na warsha mbili zilizoshirikisha wadau mbalimbali ziliandaliwa ili kupata maoni na uelewa kuhusu namna ya kuutumia.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia inaelekeza kuundwa kwa chombo cha wanawake, ambacho kitawaunganisha wanawake bila kujali itikadi zozote.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Septemba, 2002, Wizara yangu iliitisha mkutano mjini Morogoro ambao ulishirikisha baadhi ya wadau ambao walijadili jinsi ya kuwezesha uanzishwaji wa chombo cha wanawake.

Mwezi Mei, 2003, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar iliitisha mkutano wa kujadili uundaji wa Chombo cha Wanawake hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huo uliwahusisha wawakilishi wa wanawake kutoka wilaya mbalimbali za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Waheshimiwa Wabunge, vyama vya siasa, asasi zisizo za kiserikali, mashirika ya dini, vyama vya wafanyakazi na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya maendeleo ya wanawake.

Aidha, washiriki wa mkutano huo walitoa pendekezo kuwa chombo hicho kiwe katika mfumo wa Tume itakayoundwa kwa mujibu wa sheria. Kamati ya mpito iliundwa kuratibu na kuendeleza mchakato wa kuundwa kwa Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao walishiriki katika mkutano huo. Wabunge hao ni Mheshimiwa Janet Kahama, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa mkutano huo kwa kushirikiana na Mheshimiwa Martha Wejja. Kupitia Bunge lako Tukufu, namshukuru pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto Zanzibar aliyefunga mkutano huo.

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wengine walioshiriki ambao ni Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah na Mheshimiwa Bakari Mbonde. Ushiriki wao katika mkutano huo ulichangia kwa kiasi kikubwa katika mapendekezo ya aina ya Chombo kitakachoundwa. Aidha, napenda kuyashukuru mashirika yote yaliyowezesha mkutano huo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mwaka jana nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu iliwasilisha Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma mapendekezo kuhusu uundaji wa vitengo vya jinsia kulingana na muundo wa Serikali katika ngazi zote.

Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekubali madawati ya jinsia yaanzishwe katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Madawati haya yatasaidia kujenga misingi mizuri na kuhakikisha uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mipango, programu na miradi ya sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendesha warsha ya Makatibu Wakuu wa Wizara na Makatibu Tawala wa Mikoa ya Tanzania Bara huko Bagamoyo tarehe 20 Machi, 2003 kuhusu masuala ya jinsia. Warsha hiyo ilizungumzia uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango ya Wizara na mikoa ili kutilia mkazo uundaji wa madawati hayo, pamoja na kukubaliana utaratibu wa kuanzishwa kwake.

Aidha, ilikubalika kuwa katika ngazi ya Wizara, madawati hayo yatashughulikiwa na wataalam wa idara za mipango na katika ngazi ya mikoa na halmashauri za wilaya, miji na manispaa, madawati hayo yatashughulikiwa na wataalam wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapendekezo ya warsha hiyo, Wizara yangu iliwasiliana na Makatibu Wakuu wa Wizara na Makatibu Tawala wa mikoa Tanzania Bara kuwaomba wateue watumishi katika Madawati ya Jinsia. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya Wizara, Mikoa na Wilaya zimeanza kuwasilisha majina ya walioteuliwa kushughulikia madawati hayo. Wizara ambazo zimekwisha wasilisha majina ya watumishi hao ni Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Fedha, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Kilimo na Chakula, Elimu na Utamaduni, Mipango na Ubinafsishaji, Nishati na Madini, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mikoa ambayo imewasilisha majina hayo ni Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya na Tabora.

Aidha, Halmashauri za Wilaya zilizowasilisha majina ya watumishi ni Iramba, Kasulu, Kibondo, Manyoni na Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji. Ningependa kuchukua fursa hii kuwaomba Wizara, Mikoa na Halmashauri za Wilaya ambao hawajateua watumishi katika nafasi hiyo kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilihudhuria mikutano ya Kimataifa kuhusu ufuatiliaji na utekelezaji wa ulingo wa Beijing na mkataba wa Kimataifa wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake *(CEDAW)* kwa mwaka 2002/03. Katika mikutano hiyo Tanzania ilipata nafasi ya kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mikataba hiyo.

Vile vile, Wizara iliiwakilisha nchi yetu katika mkutano wa Tume ya Haki ya Wanawake kuanzia tarehe 8 hadi 15 Machi, 2003, huko New York, Marekani. Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa ni "Kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake kwa kutumia vyombo vya habari." Aidha, Wizara ilihudhuria mikutano mbali mbali ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* iliyohusu masuala ya jinsia. Mikutano hii ilitoa mwelekeo wa jinsi ya kuainisha kwa pamoja masuala yanayohusu jinsia na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyomo katika Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Kwa kuzingatia hilo, mwezi Machi, 2003, Wizara yangu iliwasilisha katika Bunge lako Tukufu, Azimio la kuridhia Mikataba ya Kimataifa ya Haki na Ustawi wa Mtoto.

Napenda kulishukuru na kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa kuridhia Mikataba ifuatayo, Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Haki za Mtoto kuhusu Ushirikishwaji wa Watoto katika Migogoro ya Kivita na Itifaki ya Nyongeza kuhusu Biashara ya Watoto, Ukahaba wa Watoto na Upigaji Picha za Udhalilishaji watoto.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuridhia mikataba hiyo kwa Tanzania, kwanza ni kutimiza wajibu wake kama nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Pili ni kuweka mazingira ya ushirikiano kati yetu na mataifa mengine na tatu ni kuweka mazingira mazuri yatakayotuwezesha kutekeleza sera, sheria na mipango inayohusu maendeleo ya watoto katika nchi yetu. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha Azimio hilo kwa kauli moja na kuwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika zilizoridhia mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Viwanda na Biashara, pamoja na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF),* Wizara yangu iliendelea kuratibu ushiriki wa wanawake katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam *(DITF)* yaliyofanyika mwezi Julai, 2002, kwa kutoa mwongozo wa namna ya kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonyesho hayo. Tathmini ya ushiriki wa wanawake katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara inaonyesha kuwa uwezo wa wanawake kibiashara na ubora wa bidhaa zao unaongezeka mwaka hadi mwaka.

Hata hivyo takwimu zinaonyesha kwamba ushiriki huo ulianza kupungua kutoka mwaka 2001 baada ya ongezeko kubwa la mwaka 2000. Napenda nitumie fursa hii kutoa mwito kwa Halmashauri pamoja na wadau wengine kuendelea kuwasaidia akinamama kushiriki maonyesho hayo muhimu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wanawake kiuchumi, mwaka 2002, Wizara yangu iliendelea kuratibu na kuimarisha mfumo wa kutoa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF).* Wizara iliingia mkataba na Halmashauri za Wilaya kuhusu fedha za mikopo za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Mkataba huu unazitaka Halmashauri kusimamia uendeshaji wa mfuko huu. Mfuko huu unatakiwa kuwa wa mzunguko, hivyo kila halmashauri inatakiwa kurejesha fedha ilizopokea katika akaunti ya Wizara kabla ya kupelekewa fedha nyingine.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zilipewa shilingi 4,000,000/= kila moja ikiwa ni mgao wa mwaka wa fedha 2001/2002 ambazo walitakiwa kurejesha ilipofika Juni 30, 2003. Fedha za mwaka 2002/2003 zitagawiwa mara halmashauri zitakaporejesha mgao wa mwaka 2001/2002. Wilaya ambazo zimekiri kupokea fedha hizo ni 74 na mpaka sasa ni Wilaya za Mtwara Mikindani na Bagamoyo zilizorejesha shilingi 2,000,000/= na shilingi 1,000,000/= tu kati ya shilingi 4,000,000/= walizopewa. Aidha, Wizara iliendelea kuhimiza Halmashauri kuchangia asilimia kumi ya mapato yao katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuzihimiza Halmashauri kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kulingana na mikataba iliyofikiwa kati yao na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendeleza mchakato wa kuwezesha uanzishaji wa Benki za Wanawake. Shirika la Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Jamii *(ESRF)* lilifanya utafiti wa jinsi ya kuanzisha benki hizo. Mapendekezo ya utafiti huo yalibainisha umuhimu wa kuanzishwa kwa vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* kama msingi wa kuanzisha Benki za Wanawake. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa wadau mbalimbali ambao wote waliafiki kuanzisha benki hizo kupitia vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa. Hivyo, wanawake wataendelea kuhamasishwa kuunda vyama hivyo na kuvimiliki wenyewe. Waraka wa Baraza la Mawaziri juu ya uanzishwaji wa benki hizo umeandaliwa ili kuweza kumshauri Mheshimiwa Rais akubali mfumo huo utumike.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha jitihada za kupiga vita mila na desturi zinazodhalilisha wanawake na watoto wa kike, Wizara yangu kama Mwenyekiti wa Mtandao wa Kanda ya Afrika Mashariki wa kutokomeza ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike, iliwezesha kufanyika mkutano wa wanachama wa mtandao huo huko Bagamoyo mwezi Aprili, 2003. Nchi za Kenya, Uganda na Tanzania zilishiriki mkutano huo uliotoa maazimio na mapendekezo ambayo yataimarisha utekelezaji wa mpango wa kutokomeza ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike. Kwenye mkutano huo, Bunge la Tanzania liliwakilishwa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi. Wizara inapenda kumshukuru sana kwa mchango wake na hasa kama Mbunge mwanaume. *(Makofi)*

Wizara yangu pia ilishiriki mkutano wa Cairo uliozungumzia mbinu za kutokomeza ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike *(Afro-Arab Expert Consultation)* uliofanyika tarehe 21 hadi 23, Juni, 2003. Mkutano huo ulijadili umuhimu wa kuwepo sheria maalum kama nyenzo ya kuzuia ukeketaji *(Legal Tools for the Prevention of FGM).* Tanzania ilialikwa kwenye mkutano huo ili itoe uzoefu wake kwa vile ni nchi mojawapo yenye sheria ya kuzuia ukeketaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliratibu maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi, 2003, Siku ya Familia tarehe 15 Mei, 2003 na Siku ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni, 2003. Madhumuni ya kufanya maadhimisho haya ni kuelimisha na kuhamasisha wananchi kutafakari masuala yanayohusu wanawake, familia na watoto katika kujiletea maendeleo yao kijamii na ya kiuchumi.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Kitaifa yalifanyika mkoani Singida na mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, kwa kushirikiana nasi katika maadhimisho haya.

Vile vile, napenda niwapongeze na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Mkuu wa Mkoa, viongozi na wananchi wa mkoa wa Singida kwa kushiriki kikamilifu na kufanikisha maadhimisho hayo. Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa: "Heshimu Utu, Acha Ukatili Dhidi ya Wanawake." Wananchi katika Mikoa mingine, Wilaya na Vijiji nchini kote waliendelea kuadhimisha siku hiyo kulingana na mazingira na raslimali walizokuwa nazo. Maadhimisho hayo yalilenga kuhamasisha jamii kuacha tabia ya ukatili kwa wanawake ambayo kwa njia moja au nyingine inachangia kuwadhalilisha na kuwanyima haki zao. Aidha, kwa kupitia maadhimisho haya jamii ilielimishwa juu ya athari za Ukimwi na jinsi ya kujikinga.

Mheshimiwa Spika, maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani yalifanyika Kitaifa na kaulimbiu yake ilikuwa: "Uvivu katika Familia ni Adui wa Maendeleo." Katika kuadhimisha siku hii, jamii ilielimishwa na kuhamasishwa kupitia vyombo vya habari na mabango kuhusu jukumu la kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kuondokana na umaskini. Napenda kupitia Bunge lako Tukufu, kuvishukuru vyombo vya habari vikihusisha Redio, *Television* na Magazeti kwa kutoa matangazo na kuandika makala kuhusu siku hii.

Mheshimiwa Spika, maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalifanyika katika kijiji cha Boko, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dr. Salim Ahmed Salim, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere. Tunapoadhimisha siku hii tunapata nafasi ya kutathmini na kutafakari utekelezaji wa sera na mikakati tuliyojiwekea kuhusu maeneo mbalimbali yaliyo muhimu kwa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto wa Tanzania ikizingatiwa pia mikataba ya Kimataifa ya haki za mtoto.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa: "Malezi Bora Utotoni ni Msingi wa Maisha." Napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Luteni Mstaafu Yusuf Makamba, viongozi wote, wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na wananchi wote nchini kwa kufanikisha maadhimisho haya.

Aidha, napenda nimshukuru Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Omar Mohammed Mwenda na Mheshimiwa Janeth Mashele, kwa kushiriki kikamilifu katika maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilitoa maelezo kuwa Wizara yangu ilikuwa imeandaa hatua ya mwanzo *(design on paper)* ya kuweka katika kompyuta mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaopima matokeo ya matumizi ya raslimali kulingana na mahitaji kijinsia *(computerized gender sensitive monitoring and evaluation system).* Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa zoezi la kutambua vigezo *(indicators)* vya jinsia kutoka sekta mbalimbali limekamilika.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili lilifanywa na kampuni ya utaalam na ushauri ya *Stoas International (T) Ltd,* kwa kushirikiana na Wizara yangu na vigezo vilivyotambuliwa viliwasilishwa kwa wadau mbalimbali ambao ni *UNICEF,* Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *UNDP, TAWLA,* Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Utamaduni, Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kupata maoni yao. Vigezo hivi vitaiwezesha Wizara kufuatilia na kutathmini maeneo ya vipaumbele vilivyotolewa na Serikali kuhusu Utekelezaji wa maazimio ya Beijing *(Beijing Platform for Action).*

Vipaumbele hivyo ni kuwaimarisha wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini, kuwawezesha wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi na za siasa, kuwawezesha wanawake kupata elimu, mafunzo na ajira na Kuwawezesha wanawake kuzielewa na kuzitumia sheria zinazolinda haki zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, ilifanya tathmini ya kuona jinsi gani itaimarisha utendaji kazi na utoaji huduma zake *(Institutional Sector and Organizational Analysis - ISOA).* Utaratibu huu ulilenga kujitazama sisi wenyewe *(internal analysis)* na vile vile kutathmini namna watu wa nje wanavyotuona *(external analysis).* Kulingana na tathmini hiyo upungufu ufuatao uligundulika, kutokuwepo kwa takwimu za kutosha zinazohusu masuala ya Wizara, kutokuwepo miundo mbinu ya kuridhisha na ukosefu wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vyetu, umuhimu unaostahili wa Idara za Maendeleo ya Jamii kutofahamika vema hususan katika ngazi za wilaya na manispaa, mazingira ya kazi yasiyoridhisha na upungufu wa

vitendea kazi, kutokuwepo wataalam wa kutosha katika ngazi muhimu za jamii kama vile vijiji na kata na mawasiliano hafifu kati ya wadau hasa waliopo mikoani, wilayani kwa upande mmoja na Wizara kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini hiyo ya *ISOA,* Wizara yangu inakamilisha maandalizi ya mpango wa miaka mitatu *(Master Plan)* utakaotekelezwa kuanzia mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006. Mpango huu utaiwezesha Wizara kuondoa upungufu uliojitokeza kwenye tathmini na utaiwezesha Wizara kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa jamii. Maeneo ambayo mpango umezingatia ni kuangalia upya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kulingana na mamlaka iliyopewa, uandaaji wa mikakati na miongozo ya sera za Wizara na mikataba ya kimataifa ili watekelezaji waweze kuitekeleza kwa ufanisi, kuandaa utaratibu unaofaa kwa ajili ya mawasiliano na wadau hasa kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya, kuongeza uwezo wa Wizara kitaaluma na vitendea kazi na kuimarisha ufuatiliaji na kufanya tathmini ya mipango na shughuli za Wizara hasa kwenye ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inacho Kituo cha Habari cha Wanawake *(WIC)* kinachofadhiliwa na Serikali ya Italia kupitia Shirika lisilo la Kiserikali la Wanawake la Italia *(AIDOS).* Utekelezaji wa mpango wa awamu ya pili wa uimarishaji wa kituo hicho utakaochukua miaka mitatu, ulianza mwezi Januari, 2003 kwa kuajiri watumishi katika vitengo mbalimbali vya kituo hicho na ununuzi wa vifaa. Pia mtandao wa kompyuta, tovuti na barua pepe umefungwa ili kurahisisha mawasiliano na wadau mbalimbali wa ndani na nje ambao shughuli zao zinafanana na za kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Idadi ya Watu *(UNFPA)* ulitayarisha Kitini cha uhamasishaji kuhusu jinsia, virusi vya Ukimwi na Ukimwi katika Afrika Kusini mwa Sahara, kwa lugha ya Kiingereza. Kitini hiki kilitolewa katika Mkutano wa Mawaziri na Wabunge Wanawake uliofanyika katika visiwa vya Cape Verde mwaka 2002, ambapo Tanzania ilishiriki. Lengo la kutolewa Kitini hiki ni kutoa changamoto kwa uongozi Barani Afrika kuhusu hali halisi ya jamii zetu na mazingira zinamoishi. Katika mkutano huo wajumbe walikubaliana kuwa Kitini hicho kitumike kama nyenzo mojawapo ya kuyashughulikia masuala ya jinsia na Ukimwi.

Aidha, wajumbe waliohudhuria mkutano huo kutoka Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* walikubaliana kukitumia Kitini hicho kama nyenzo muhimu ya kuyashughulikia masuala ya jinsia na Ukimwi kwenye nchi zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia ufadhili wa *UNFPA* imekifanyia tafsiri ya Kiswahili kitini hiki kuhusu Jinsia, Virusi vya Ukimwi *(VVU)* na Ukimwi katika Afrika Kusini mwa Sahara. Madhumuni ya kufanya tafsiri ya kitini hiki ni kukiweka katika lugha inayofahamika na wengi nchini mwetu na hivyo kuongeza wigo wa uelewa miongoni mwa jamii kuhusiana na masuala mbali mbali yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kwamba kuwepo kwa watumishi wenye sifa, ari na uwezo unaotakiwa wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ndio msingi mkubwa wa kuwezesha Wizara kufikia malengo iliyojiwekea. Wizara imeendelea kusimamia ajira za watumishi na maendeleo yao kazini, kuweka mazingira mazuri ya kazi na kuona kwamba sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa zinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/03, Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi Serikalini (TUMEAJIRI) iliwapandisha vyeo Maafisa Maendeleo ya Jamii 18, Wahasibu 2 na Wasaidizi wa Hesabu 6 na Afisa Mipango mmoja. Aidha, Tume ya Utumishi ya Walimu iliwapandisha vyeo walimu 51 ambao waliajiriwa na Wizara kwa ajili ya kufundisha katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii na vya Maendeleo ya Wananchi. Chini ya Mamlaka ya Kamati Maalum ya Utumishi Serikalini *(KAMUS),* watumishi 37 wa kada mbalimbali walipandishwa vyeo. Watumishi wengine 22 ambao walimaliza vipindi vyao vya majaribio kwa mafanikio walithibitishwa kazini.

Vile vile watumishi watatu walibadilishwa na kupandishwa vyeo katika kada za ufundi sanifu msaidizi na udreva baada ya kujiendeleza na kujipatia sifa zinazowawezesha kubadilishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na zoezi hilo la kuwapandisha vyeo watumishi, Wizara yangu imeendelea kuwapatia mafunzo ili kuongeza ari na ufanisi wa kazi. Katika mwaka wa fedha 2002/03, watumishi walipewa mafunzo katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo, Watumishi 9 wanaendelea na mafunzo ya stashahada ya Uzamili, watumishi 15 walipata mafunzo ya kompyuta, watumishi watatu mafunzo ya muda mfupi ya uhasibu *(CPA Review),* watumishi saba mafunzo ya utunzaji nyaraka, watumishi watatu kozi za kiingereza kigumu, mtumishi mmoja mafunzo ya juu ya udreva *(Advanced Drivers' Course)* na watumishi watano mafunzo ya kupiga chapa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/03, Wizara yangu ilipata kibali cha kuajiri watumishi 65 wa kada mbalimbali kama hatua ya kukabili tatizo la upungufu wa watumishi hivyo kuongeza ufanisi na kasi ya kutoa huduma kwa jamii. Watumishi wapya walioajiriwa ni Maafisa Maendeleo ya Jamii Daraja la III – wawili, Dreva - mmoja, Maafisa Elimu Wasaidizi Daraja la IV - 20, Mafundi Sanifu Daraja la IV - 10, Wapiga Chapa - 4, Walinzi - 19, Wahandisi - 2, Maafisa Elimu Daraja la III - 2, Wasaidizi wa Hesabu Daraja la II - mmoja, Afisa Ugavi mmoja, Mkutubi Daraja III – mmoja, Mtaalamu wa Mfumo wa Kompyuta - mmoja na Mkutubi Daraja la I - mmoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza mikakati ya Kitaifa ya kutoa mafunzo ya kupambana na maambukizo ya Ukimwi katika sehemu za kazi. Watumishi waliopatiwa mafunzo hayo ni wa makao makuu ya Wizara, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Rungemba na Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Arnautoglou, Ilula, Kisangwa, Kisarawe, Monduli, Musoma, Njombe, Ruaha, Tarime na Ulembwe. Elimu hiyo itaendelea kutolewa kwa watumishi wengine waliobaki.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Sera ya Chama cha Mapinduzi unazungumzia pamoja na masuala mengine, umuhimu wa kuwepo Utawala Bora na kupiga vita rushwa. Mwezi Juni, 2003, Wizara yangu iliendesha mafunzo kwa Wakuu na Wasaidizi wa Hesabu 124 wa Vyuo vilivyoko chini ya Wizara. Mafunzo hayo yalifanyika Morogoro na yalilenga kuimarisha utawala bora na kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakabiliwa na matatizo kadhaa ambayo yanaathiri utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na upungufu wa watumishi na wataalam, kuwepo kwa Bajeti ambayo haikidhi mahitaji ya Wizara, uhaba wa vitendea kazi kama vile nyenzo, vifaa na vyombo vya usafiri, ukosefu wa takwimu zinazohusu masuala ya Wizara, uchakavu wa vifaa, majengo na miundombinu, mfumo hafifu wa mawasiliano kati ya Wizara na wadau wengine wa maendeleo na upungufu wa wataalam wa maendeleo ya jamii katika wilaya, manispaa na miji pamoja na uhaba wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii sasa kutoa matarajio ya mipango na utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu inatarajia kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii kwa wadau mbali mbali.

Aidha, itaendelea na jitihada za kutafuta rasilimali za kutekeleza Programu ya Kuimarisha Shughuli za Maendeleo ya Jamii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuhimiza wananchi kutumia sayansi na teknolojia katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku za kiuchumi na kijamii. Aidha, Kitita cha Teknolojia Sahihi kilichochapishwa mwaka 2002/2003, kitasambazwa kwa wadau mbali mbali katika mwaka 2003/2004. Inatarajiwa kuwa wadau hao watakitumia Kitita hicho na hivyo kuongeza kasi ya usambazaji na utumiaji wa sayansi na teknolojia sahihi katika mchakato mzima wa kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaanzisha mafunzo ya Stashahada za Juu katika michepuo mipya miwili, mmoja wa Jinsia na Maendeleo na wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Miradi kuanzia mwaka wa masomo utakaoanza mwezi Septemba, 2003. Kutokana na kuongezeka kwa michepuo hiyo miwili, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kinatarajiwa kuongeza idadi ya wanachuo kutoka 70 hadi kufikia 210. Aidha, mafunzo ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya cheti yataendelea

kutolewa katika vyuo vya Buhare, Missungwi na Rungemba. Inatarajiwa wanafunzi 120 watajiunga na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kupitia vyuo vya maendeleo ya wananchi, inatarajia kutoa mafunzo kwa wananchi 13,640 ambapo kati yao wananchi 4,640 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na 6,000 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na 3,000 watapatiwa mafunzo nje ya Chuo *(outreach).* Aidha, mafunzo hayo yatatolewa kwa kufuata mtaala mpya uliochapishwa na kusambazwa vyuoni mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya cheti cha taaluma ya ujenzi na ufundi kwa wataalam wa ujenzi na mafunzo ya ufundi vijijini. Mafunzo haya hutolewa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii na Mafunzo ya Ufundi Misungwi. Wataalam kutoka chuo hiki huajiriwa na Halmashauri za Wilaya zenye Vikosi vya Ujenzi ambavyo vina jukumu la kuwapatia wananchi ujuzi na stadi za kiufundi ili waweze kutekeleza shughuli za ujenzi vijijini kwa njia ya kujitegemea.

Vile vile, Wizara itaendelea kukiimarisha Chuo hiki kwa kubadilisha programu ya mafunzo kutoka cheti cha kawaida *(BCC)* kwenda ngazi ya cheti cha ufundi *(FTC),* kuwaendeleza walimu kitaaluma, kuimarisha majengo na miundo mbinu pamoja na kununua nyenzo na vifaa vya kiufundi ili kiweze kutoa mafundi wenye ujuzi na mbinu za kisasa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/04, Wizara yangu inatarajia kuvifanyia ukarabati mdogo mdogo vyuo 24 vifuatavyo, Handeni (Handeni), Ifakara (Kilombero), Ikwiriri (Rufiji), Kilwa Masoko (Kilwa), Kisarawe (Kisarawe), Mamtukuna (Rombo), Masasi (Masasi), Mbinga (Mbinga), Msinga (Moshi Vijijini), Munguri (Kondoa), Mwanhala (Nzega), Mwanva (Kahama), Newala (Newala), Ngara (Ngara), Nzega (Nzega), Nzovwe (Mbeya Mjini), Same (Same), Sengerema (Sengerema), Singida (Singida), Tango (Mbulu), Tarime (Tarime), Ulembwe (Njombe), Urambo (Urambo) na Uyole (Mbeya Mjini).

Aidha, vyuo 12 ambavyo viko katika hali mbaya, vitafanyiwa ukarabati mkubwa wa majengo na miundo mbinu. Vyuo hivyo ni Chisalu (Dodoma), Gera (Kagera), Karumo (Mwanza), Kihinga (Kigoma), Kilosa (Morogoro), Kisangwa (Mara), Mabughai (Tanga), Mlale (Ruvuma), Monduli (Arusha), Mtawanya (Mtwara), Ruaha (Iringa) na Sofi (Morogoro).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu vile vile inatarajia kufanya ukarabati mkubwa wa vyuo vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Missungwi, Rungemba na Tengeru ili kuweza kuongeza idadi ya wanachuo na kutoa huduma bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Wizara uliofanyika Tanga mwezi Oktoba, 2002, zinaonyesha kuwa vipo vikosi 51 vya Ujenzi na Mafunzo ya Ufundi ambavyo viko hai. Vikosi hivi vimeendelea kushirikiana na wananchi katika utekelezaji wa miradi yao ya kujitegemea kama ile inayofadhiliwa na *TASAF.* Hata hivyo, tunazo taarifa kuwa katika baadhi ya halmashauri, vikosi hivyo vimehamishiwa katika Idara za Ujenzi na hivyo kutoshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa moja kwa moja wa miradi ya kujitegemea ya wananchi.

Kwa ujumla hali ya vikosi hivyo kuhusiana na mafundi na vifaa haiwezi kukidhi mahitaji ya wananchi katika utekelezaji wa miradi yao. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itatoa mafunzo ya rejea ya muda mfupi kwa baadhi ya mafundi wa vikosi hivyo. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Vikosi vilivyohamishiwa kwenye Idara ya Ujenzi vinarejeshwa kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii ili viendelee kutekeleza majukumu yake yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kuanzia mwezi Februari hadi Juni, 2003 ilishirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuchambua miradi ya utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy).*

Mheshimiwa Spika, nia ilikuwa ni kubaini miradi iliyoandaliwa kutekelezwa kwa utaratibu wa mbinu shirikishi jamii ambayo watu wenyewe wameshiriki kuibuni na inayolenga kuwaondolea vikwazo vya uzalishaji na uuzaji wa mazao yao na hivyo kuongeza tija na ufanisi. Kwa mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula pamoja na Wizara nyingine katika utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya Serikali ya kuondoa umaskini ni utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Elimu nchini *(Education Sector Development Programme – ESDP).* Programu hii ilianza na mkakati wa kuboresha elimu ya msingi (MMEM) mwaka 2002 ambao utekelezaji wake unaendelea kote nchini.

Hivi sasa Serikali inaelekeza jitihada na rasilimali zake katika Mpango wa Elimu na Mafunzo baada ya Elimu ya Msingi *(Post Primary Education and Training).* Mpango huu unazihusisha Wizara zinazosimamia Shule za Sekondari, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni pamoja na Wizara nyingine zinazosimamia elimu nchini katika kufanya utafiti utakaoiwezesha Serikali kuandaa Mpango wa Kuimarisha Elimu na Mafunzo baada ya Elimu ya Msingi. Kwa upande wa Wizara yangu, jumla ya vyuo 30 vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo 3 vya Maendeleo ya Jamii vilishirikishwa katika utafiti huo. Utafiti huo unatarajiwa kubaini mafanikio, matatizo na masuala muhimu ya kushughulikiwa katika kuviimarisha vyuo hivyo. Matokeo ya utafiti huo yatawasilishwa Serikalini kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Mkakati wa Kijamii wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya Ukimwi unatakiwa kuwekewa mipango thabiti ya kuutekeleza. Kwa kuzingatia hilo, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendesha vikao kwa kuhusisha wadau mbalimbali yaani Wizara zinazotoa huduma za jamii, asasi zisizo za kiserikali, watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi, wataalam wa matunzo ya nyumbani, wataalam wa afya na viongozi wa dini ili kuimarisha mkakati huo na kuweka mpango wa kuutekeleza. Hii ni pamoja na kuhakikisha unazingatia masuala ya kudhibiti unyanyapaa, kuzuia maambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto *(mother to child transmission)* na kuongeza muda wa kuishi. Vile vile, Wizara yangu itaendesha mafunzo ya uraghbishi kwa wadau hao kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs).*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuendesha mafunzo ya rejea ya muda mfupi kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii. Mafunzo haya yatalenga masuala ya Ukimwi, biashara, utunzaji wa mazingira, jinsia na kuondoa umaskini kwa ujumla. Mafunzo hayo yatawawezesha kuihudumia jamii kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, masuala ya jinsia na maendeleo yanavuta jitihada za wadau wengi ambao wangependa kushiriki nasi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itachapisha Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia katika lugha ya Kiingereza na kuisambaza kwa wadau mbalimbali ambao hawafahamu lugha ya Kiswahili ili nao waweze kuchangia zaidi katika utekelezaji wake. Wizara pia itakamilisha mwongozo wa utekelezaji wa sera hiyo na kuusambaza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako tukufu katika kipindi kilichopita familia ndiyo chimbuko la maisha na maendeleo ya binadamu. Kuwepo kwa Sera imara itakayoongoza masuala ya familia ni jambo muhimu katika nchi yetu. Kwa msingi huu, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa sasa rasimu ya Sera ya Familia imekamilika. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara yangu itawasilisha Sera hii katika ngazi mbalimbali za maamuzi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Taifa letu yanaletwa kwa ushirikiano kati ya wanawake na wanaume katika jamii yetu. Ili mwanamke aweze kushiriki kikamilifu katika mchakato wa maendeleo, anahitaji elimu, stadi na taaluma katika nyanja mbalimbali. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali, itatekeleza programu inayoshughulikia masuala ya maendeleo ya

wanawake na jinsia *(Gender and Women's Advancement Programme Support).* Programu hii inalenga maeneo matatu, ambayo ni kujenga uwezo wa Wizara kwa kuendesha mafunzo ya jinsia kwa wataalamu wa Wizara ili waweze kuratibu masuala ya jinsia nchini, kuwapa uwezo wanawake ili waweze kufikia angalau asilimia 30 au zaidi kwenye uwakilishi Bungeni na katika nafasi nyingine za uongozi na uboresha nafasi za wanawake wafanyabiashara ndogo ndogo kwa kuwawezesha kushiriki katika maonyesho ya biashara ya kimataifa ikiwa ni njia mojawapo ya kuongeza uelewa wao kibiashara, ubunifu wa biashara, utafutaji wa masoko na upangaji wa bei.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuhakikisha kunakuwepo usawa wa kijinsia katika sekta mbalimbali. Kwa msingi huo, Serikali inaendelea kuteua watumishi katika ngazi mbalimbali watakao ratibu uingizaji wa masuala ya jinsia katika nyanja zote za maendeleo. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, watumishi walioteuliwa watapatiwa mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kuhakikisha kuwa usawa wa kijinsia ambao ni muhimu sana katika maendeleo unazingatiwa vema katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kuwawezesha wataalamu wa maendeleo ya jamii na ushirika wa mikoa na wilaya kuwahamasisha wanawake kuanzisha vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* kama njia ya uanzishaji wa Benki za Wanawake. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF).* Vile vile, Wizara yangu itapeleka fedha kwenye wilaya zitakazorejesha mikopo waliyopewa mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kuwezesha mchakato wa uundaji wa chombo cha wanawake kwa kufuata mfumo wa Tume.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kuratibu shughuli zote za maadhimisho ya kitaifa na kimataifa zinazohusu wanawake, watoto na familia. Umoja wa Mataifa kama chombo kilichoanzisha na kupendekeza maadhimisho ya siku hizi, umezitaka nchi zote wanachama kusherehekea maadhimisho hayo kwa kuandaa programu ambazo zitalenga masuala ya maendeleo kulingana na mazingira ya nchi zao. Mwaka 2004 utakuwa ni mwaka wa kumi tangu Siku ya Familia Duniani ianze kuadhimishwa kimataifa. Kipindi hiki kilionekana kuwa muafaka kupima juhudi zilizofanyika katika kuimarisha familia tangu Umoja wa Mataifa ulipoanza maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Familia mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tutaendelea kuitumia siku hiyo kuelimisha jamii kuhusu maendeleo, wajibu na majukumu ya wanafamilia katika kupiga vita umaskini. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu itafanya maandalizi ya maadhimisho ya miaka 10 ya Siku ya Familia na baadaye kuendelea kuadhimisha siku hiyo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara yangu itakamilisha Sera ya Maendeleo ya Mtoto iliyodurusiwa kwa kuipitisha katika ngazi mbalimbali za maamuzi Serikalini. Haja ya kudurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996, ilitokana na upungufu uliojitokeza katika Sera hiyo. Upungufu huo ni kutoingizwa kwa dhana ya ushiriki wa watoto katika masuala mbalimbali ya maendeleo, kutobainishwa kwa makundi mahsusi ya watoto wenye mahitaji maalum na wanaoishi katika mazingira magumu kama vile watoto wenye ulemavu, yatima, wasio na makazi maalum na wale wanaoishi na virusi vya Ukimwi na Ukimwi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo tunaona muhimu yawe sehemu ya Sera hii ni kama vile ajira ya watoto, ukatili, kubakwa, biashara ya ukahaba na ushiriki wao katika vita. Pamoja na kuainisha maeneo haya, Sera iliyodurusiwa inalenga kubainisha nafasi na majukumu ya kila mwanafamilia, wanajamii, Serikali na taasisi nyingine. Vile vile, mwongozo wa utekelezaji wa Sera hiyo utafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia Sera iliyodurusiwa, utasambazwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni yao na hatimaye kupitishwa katika ngazi nyingine husika za kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wenye dhamana ya ustawi na maendeleo ya mtoto, itaandaa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Waraka uitwao Dunia Iwafaayo Watoto

na Afrika Iwafaayo Watoto. Waraka huu ni matokeo ya maazimio ya Mkutano Maalum wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu watoto uliofanyika tarehe 8 hadi 10 Mei, 2002 huko New York, Marekani na mkutano wa Afrika kuhusu watoto uliofanyika Cairo, Misri tarehe 28 hadi 31 Mei, 2001 ambapo nchi yetu ilishiriki kikamilifu. Mikutano yote hii inasisitiza umuhimu wa kuendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata malezi mazuri katika maisha. Ni muhimu kwa mtoto kukua, kulelewa na kuendelezwa katika mazingira mazuri yenye upendo, amani, usalama na heshima ambamo haki zake za msingi zitaendelezwa na kulindwa.

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la Wizara yangu ni kuwahamasisha wananchi waondokane na mila zinazoleta madhara kwa wanawake na watoto. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendeleza juhudi za kutokomeza ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike. Aidha, Wizara yangu inatarajia kutekeleza programu ya kutoa elimu ya idadi ya watu na maisha ya familia. Programu hii itasaidia kuwatanabahisha wananchi kuhusu mila zinazoleta madhara hususan kwa wanawake na watoto. Vile vile, programu hii itasaidia kujenga maadili mema hasa kwenye ngazi ya familia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuratibu kwa kufuatilia na kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa inayohusu haki za watoto. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto *(CRC)* na ule wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Afrika *(ACRWC).* Wizara itaratibu pia utekelezaji wa Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Haki za Mtoto kuhusu Ushirikishwaji wa Watoto katika Migogoro ya Kivita na Itifaki ya Nyongeza kuhusu Biashara ya Watoto, Ukahaba wa Watoto na Upigaji Picha za Udhalilishaji Watoto.

Katika kutekeleza azma hii, Wizara yangu itaendesha mafunzo kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii wa Mikoa na Wilaya juu ya mikakati ya utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu haki za mtoto. Vile vile, Wizara itaendelea kuhudhuria mikutano mbalimbali ya Kimataifa na kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa nchi yetu kuhusiana na mikataba niliyoitaja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa sera za Wizara pamoja na kufuatilia uingizaji wa masuala ya jinsia katika bajeti na sera za sekta mbalimbali. Aidha, Wizara itaendelea kuwasiliana na asasi zisizo za kiserikali kwa ajili ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano katika utekelezaji wa dira na sera za Wizara.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Wizara yangu kuhusu mpango wa kutambua vigezo vitakavyotumika kufuatilia na kutathmini masuala ya jinsia kwenye sekta mbalimbali, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004, itatekeleza hatua ya kuingiza vigezo hivyo pamoja na takwimu nyingine zinazohitajika Wizarani kwenye kompyuta. Kazi hii itafanywa na wataalam wa Wizara yangu wakishirikiana na Kitengo cha Kompyuta cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mfumo huu wa kompyuta utakusanya takwimu zitakazotuwezesha kutathmini utendaji kazi, utekelezaji wa programu na miradi kama inazingatia masuala ya jinsia, vipaumbele vya Serikali vya ulingo wa utekelezaji wa maazimio ya Beijing na utekelezaji wa Mkakati wa Kuondoa Umaskini. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2004 na mfumo huu kuanza kutumika mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, licha ya Mpango wa miaka mitatu *(Master Plan)* kuandaliwa kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma wa Wizara yangu, pia mpango huu utasaidia Wizara kuondokana na utaratibu wa sasa wa utekelezaji wa mradi mmoja mmoja na badala yake kutumia mfumo wa kisekta *(Sector-wide Approach).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kujiimarisha kwa kuajiri wataalamu mbalimbali na kuwa na vifaa na nyenzo zinazohitajika, Kituo cha Habari cha Wanawake kitajenga tovuti *(Website)* kwa ajili ya kusambaza taarifa zinazohusu wanawake, watoto, maendeleo ya jamii na jinsia.

Aidha, kituo kitaanzisha jarida litakalotoa habari zinazohusu maendeleo ya wanawake ambalo litakuwa likichapishwa kila mwezi. Vile vile, Wizara yangu itaendelea kukusanya taarifa zinazohusiana na fursa mbalimbali zinazotolewa kwa wanawake kuhusu ajira, mafunzo, ujuzi na elimu. Hali kadhalika, Wizara itaanzisha sehemu maalum ya wanawake katika kituo hicho *(Women's Information Window)* itakayotoa taarifa na ushauri kwa wanawake wanaotafuta kazi, nafasi za masomo na uhisani pamoja na

kuwapa mbinu za kushiriki katika uombaji na usaili wa kazi. Pia, Wizara itafanya utafiti wa kuanzisha uwekaji wa kumbukumbu zinazohusu wanawake katika Kompyuta *(Women's Data Base).* Hii itasadia kufahamu wasifu wa wanawake walioko katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/04, Wizara yangu kwa kushirikiana na wataalam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itafanya utafiti wa kuainisha uwezekano wa kuwa na utaratibu utakaowezesha uanzishaji na uendeshaji bora wa biashara zinazofanywa na wanawake *(Feasibility study for the establishment of a business incubator for women in Tanzania).* Utaratibu huu utawasaidia wanawake wa Tanzania kufahamu mbinu za kuanzisha, kuendeleza, kukuza na kupanua biashara.

Aidha, utasaidia kuwapatia elimu na ujuzi wa kuendesha biashara, kupata mitaji na huduma ya kiufundi pamoja na kuwaunganisha na masoko ya biashara ya kitaifa na kimataifa kama vile *EAC, SADC, AGOA, EBA* na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako tukufu hapo awali, Kitini cha uhamasishaji kuhusu masuala ya jinsia na Ukimwi kinatoa ufafanuzi kuhusu masuala mbali mbali ya kijamii na kiuchumi. Baadhi ya masuala hayo ni usawa wa kijinsia, maambukizo ya virusi vya Ukimwi, maisha ya vijana walio katika umri wa balehe na huduma kwa waathirika wa Ukimwi. Mengineyo ni vitendo vyenye madhara kwa jamii, unyanyasaji wa wanawake na mikakati ya kuwalinda, uhamasishaji na utetezi wa mabadiliko, mikakati ya kupunguza umaskini, ukusanyaji wa rasilimali na mgawanyo wake katika jamii na Malengo ya Milenia. Katika kuhakikisha kuwa ujumbe huu unawafikia walengwa wengi, mwaka 2003/2004, Wizara yangu inatarajia kuchapisha nakala 5,000 za Kitini hiki na kuzisambaza kwa walengwa mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu, Wizara inashiriki katika kuandaa mpango maalum wa Serikali wa kuimarisha huduma zake *(Perfomance Management System)* ambao utaweka mikakati ya kuhakikisha kwamba huduma zitolewazo na Wizara zinafikia matarajio ya wadau na walengwa wengine. Mpango huu utakapokamilika utasaidia Wizara kuweka malengo yanayopimika na kutekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wa kada mbalimbali kwa wakati unaostahili kwa kuzingatia Sera mpya ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma. Aidha, watumishi wataendelea kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kama hatua ya utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kuondokana na rushwa kwa kufanya kazi kwa kuzingatia misingi inayosisitiza uwazi na ukweli, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na rushwa ili kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili mema katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kufanya mkutano mkuu wa mwaka wa Wizara ambao hujumuisha viongozi wa Wizara, Maafisa Waandamizi kutoka Makao Makuu ya Wizara, Washauri wa sekta ya maendeleo ya jamii katika sekretarieti za Mikoa, wataalam wa maendeleo ya jamii wa Wilaya, wakuu wa vyuo vya maendeleo ya jamii na wakuu wa vyuo vya maendeleo ya wananchi. Aidha, utaratibu wetu unatoa fursa ya kuwakaribisha wawakilishi kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali na Wizara nyingine, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Vijana, Ajira na Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar.

Madhumuni ya mkutano huo unaofanyika kila mwaka ni kubadilishana uzoefu, kutathmini kazi za Wizara ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake na ya kisekta, kubaini matatizo katika utekelezaji wa majukumu na kupanga namna ya kuyatatua hasa kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejiwekea utaratibu wa kufanya mikutano miwili kila mwaka ya ushirikiano na Wizara ya Vijana, Ajira na Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar. Mikutano tunayofanya ni muhimu kwa Wizara zetu mbili kwani inatupa nafasi ya kujadili masuala yanayohusiana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa manufaa ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi kila mwaka kwa mujibu wa Agizo la Rais Na. 1, mwaka 1970. Vikao hivyo vinasaidia kuimarisha uhusiano kati ya viongozi wa Wizara na chombo cha wafanyakazi *(TUGHE)* kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi ndani ya Wizara na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, Ukimwi ni janga la Taifa ambalo linaathiri maendeleo ya nchi kwa kuwa linagusa nguvu kazi muhimu ya Taifa letu. Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kutoa mafunzo ya kupambana na maambukizo ya Ukimwi katika sehemu za kazi. Mafunzo hayo kwa mwaka 2003/2004, yatatolewa kwa watumishi waliopo kwenye vyuo 15 vilivyopo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai, 2003 Wizara yangu itatekeleza mpango wa Serikali wa kuboresha huduma kwa umma kwa kushirikisha sekta binafsi. Ushirikishaji huo utafanywa kwa kubinafsisha baadhi ya shughuli za utoaji wa huduma ambao utaanzia makao makuu ya Wizara katika maeneo ya usafi wa mazingira na ulinzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, tutaimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Jamii kwa kukipatia vifaa na kutoa mafunzo kwa wataalamu wanaofanya kazi katika Kitengo hicho katika kuandaa majarida na vipindi vya redio. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaelimisha jamii kuhusu majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Wizara yangu ni mtambuka, na mapitio ya utekelezaji wa mpango na malengo ya Wizara yanaonyesha kwamba tutaendelea kuhitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kuimarisha utendaji wa sekta hii. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa tutaendeleza juhudi zetu katika kuiwezesha jamii kuchangia katika maendeleo yao na ya taifa letu kwa ujumla. Lengo la Wizara yangu ni kushirikiana na wadau waliopo katika sekta mbalimbali ili kuleta maendeleo stahimilivu nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang na Waziri Mkuu, kwa hotuba yake iliyoeleza kwa kina hali ya maendeleo ya Watanzania kiuchumi na kijamii. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imetupa upeo mpana wa kuelewa wapi tuelekeze nguvu zetu ili Mtanzania azidi kupiga hatua katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuwapongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, na Waziri wa Nchi, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda , kwa hotuba zao ambazo zilieleza vizuri hali ya uchumi wetu na nini mategemeo yetu ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Mawaziri wenzangu waliotangulia kuwapongeza wabunge wote waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo uliofanyika mwezi Mei, 2003. Wabunge hao ni Mheshimiwa Abu Kiwanga, CCM, Jimbo la Kilombero, Mheshimiwa Nazir Karamagi, CCM, Jimbo la Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Edward Ndeka, CCM, Jimbo la Kigoma Kusini, Mheshimiwa Sumri Mohamed, CCM, Jimbo la Mpanda Magharibi, Mheshimiwa Karim Said Othman, *CUF,* Jimbo la Chambani, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, *CUF,* Jimbo la Mtambile, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, *CUF,* Jimbo la Chonga, Mheshimiwa Ali Said Salim, *CUF,* Jimbo la Ziwani, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, *CUF,* Jimbo la Micheweni, Mheshimiwa Salim Omar Ali, *CUF,* Jimbo la Tumbe, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, *CUF,* Jimbo la Konde, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, *CUF,* Jimbo la Mgogoni, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, *CUF,* Jimbo la Wingwi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, *CUF,* Jimbo la Gando, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, *CUF,* Jimbo la Mtambwe, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, *CUF,* Jimbo la Ole, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, *CUF,* Jimbo la Utaani, Mheshimiwa Ali Said Juma, *CUF,* Jimbo la Kojani na Mheshimiwa Omar Juma Omar, *CUF,* Jimbo la Pandani.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kutoa shukrani zangu kwa iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, kwa ushauri na mchango wa busara tulioupata katika kipindi kilichopita. Aidha, naomba kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba,

Mbunge wa Viti Maalum, kwa ushauri na hekima za Kamati yake ambazo zimesaidia sana uchambuzi wa kazi za Wizara yangu.

Aidha, mwezi Mei, 2003, Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati hii walipata nafasi ya kutembelea baadhi ya vyuo vyetu vya Arnautoglou, Kibaha na Kisarawe pamoja na kujionea wenyewe baadhi ya shughuli za Maendeleo ya Jamii zilizoko mkoa wa Dar es Salaam. Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Kamati hii kwa ushauri na maelekezo waliyotupa ambayo tuna hakika yataimarisha utekelezaji wa majukumu yetu. Ni kwa msingi huo, Wizara yangu itaandaa ziara za namna hiyo siku zijazo ili kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kupata uelewa wa hali halisi ya vyuo vyetu pamoja na kujionea shughuli zetu nyingine ili waendelee kutushauri na kutuelekeza ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, utulivu na hekima kubwa.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, kwa ushirikiano, ushauri pamoja na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vile vile, napenda kutoa shukrani kwa Bibi Mary Mushi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu katika ngazi zote na katika taasisi zetu zote kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Bila ya mchango wao muhimu ingekuwa vigumu kupiga hatua katika majukumu tuliyonayo ya kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wale wote tunaofanya nao kazi na wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana. Peke yetu kama Wizara tusingeweza kufikia mafanikio niliyoyataja. Napenda kutumia nafasi hii kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wafuatao, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF),* Shirika la Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP),* Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania *(TAWLA),* Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania *(TAMWA),* Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania *(FAWETA), Plan International* na Mashirika mbali mbali pamoja na wale ambao wanafanya kazi kwa maslahi yetu kwa namna moja au nyingine.

Napenda kuzishukuru Serikali za nchi rafiki ambazo kwa kupitia Mashirika yake ziliendelea kutusaidia. Nchi hizo ni Canada, Finland, Holland, Ireland, Italia, Japan, Netherlands, Sweden na Uingereza. Mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Dunia, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto *(UNICEF),* Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu *(UNFPA),* Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake *(UNIFEM)* pamoja na mashirika mengine ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya mwaka 2003/2004, ili Wizara yangu iweze kufikia malengo yake kwa mwaka 2003/2004, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Matumizi ya shilingi 5,266,365,600/=. Kati ya hizo shilingi 3,893,286,200/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 1,392,975,400/= ni kwa ajili ya kulipia mishahara na shilingi 2,500,310,800/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges).* Aidha, shilingi 1,373,079,400/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo shilingi 600,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 773,079,400/= ni fedha za nje.

Mwisho kabisa, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja Waheshimiwa Wabunge kwa kunikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Kabla hatujamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua makadirio ya Wizara hii, katika utaratibu wangu wa kuwapangia zamu wasaidizi wangu wa kuongoza Bunge, ili wajenge uzoefu, sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti Anne Makinda, aendelee kuongoza Bunge. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA – MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2003, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati kwa kunichagua niwe Mwenyekiti wao kwa kipindi cha miaka mitatu ya uhai wa Bunge (2003-2005).

Pia napenda kuwapongeza kwa ushirikiano wao katika kuchangia mawazo, maoni na mapendekezo katika kukamilisha taarifa hii na kuiwezesha kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwapongeze Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mama Mary Mushi, Katibu Mkuu, pamoja na Maofisa wa Wizara hiyo kwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2002/2003 na makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioshinda katika chaguzi ndogo zilizofanyika tarehe 18 Mei, 2003, Vile vile Kamati inampongeza Bibi Betty Mkwasa, kwa kujinyakulia tuzo ya *CNN* kutokana na ushindi alioupata kwa kuwa Mtangazaji wa kwanza katika Afrika kuwa mbunifu mzuri katika kuandaa vipindi vyake vya kuelimisha umma kupitia *ITV* kuhusu masuala ya Ukimwi. Mtangazaji huyu ameiletea Tanzania heshima kubwa. Aidha, Kamati yetu inampongeza Bibi Rosebud Kurwijila, kwa kuteuliwa kuwa Kamishna katika *AU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii ya Kamati kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuteuliwa kama *Good Will Ambassador* wa *WHO* Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, ameteuliwa kuhamasisha jitihada za kupunguza vifo vya Wanawake vinavyotokana na uzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2003 Kamati ina wajumbe wafuatao:-

Mimi Sophia Simba, ndiyo Mwenyekiti wa Kamati hii na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe wafuatao ndiyo wanaunda Kamati hii ambao ni Mheshimiwa Janeth Mashelle, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa na Katibu wetu Ndugu Angelina Sanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 pamoja na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iliwasilisha taarifa yake mbele ya Kamati tarehe 4 Juni, 2003 Jijini Dar es Salaam na kufafanua masuala muhimu kama ifuatavyo, mwelekeo wa Wizara *(vision),* majukumu ya Wizara, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha 2002/2003, Mapato na Matumizi ya mwaka 2002/2003, mafanikio na matatizo

yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji kwa mwaka uliopita, kazi zilizopangwa kufanywa katika mwaka wa fedha 2003/2004 na maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2002/2003. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilifanikiwa kutekeleza maagizo ya Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii yaliyotolewa mwaka wa fedha 2002/2003. Wajumbe waliridhika na utekelezaji uliofanyika kama ifuatavyo, mabadiliko ya jina la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Wizara imeweza kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Cheti na Stashahada ya Juu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka 2002/2003 Wanachuo 63 walihitimu katika Stashahada ya Juu ya Maendeleo ya Jamii na 101 walihitimu katika ngazi ya Cheti. Waliotarajiwa kuhitimu walikuwa 103, wawili waliahirisha masomo yao kwa sababu ya afya zao.

Aidha, Wizara inaendesha mafunzo ya muda mfupi,ambapo hadi sasa wataalam 110 wa maendeleo ya jamii katika ngazi ya Mkoa na Wilaya wamepatiwa mafunzo haya. Kuanzia mwaka 2002 Wizara imetenga 60% ya nafasi za kujiunga na masomo ya stashahada ya juu ya Maendeleo ya Jamii katika Chuo cha Tengeru kwa watumishi walioko kazini.

Kuhusu ushirikiano na Wizara zingine Wizara inashirikiana vizuri na Wizara ya Elimu katika kudurusu Mtaala wa vyuo ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Aidha inashirikiana na Wizara ya Kazi, TAMISEMI na Wizara ya Vijana, Ajira na Maendeleo ya Wanawake na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kutoa mafunzo ya Stadi mbalimbali kwa wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kuangalia uwezekano wa vyuo vyote vya maendeleo ya wananchi kuandikishwa na *VETA* ili vyeti vyake viweze kutambulika, Wizara iendelee na utaratibu wa kuyafanyia ukarabati majengo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kote nchini kutokana na mengi ya majengo hayo kuwa machakavu sana .*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wabunge Wanawake wote wawe Wajumbe wa Bodi ya Vyuo hivi vilivyomo katika Mikoa yao, Wizara izihimize Halmashauri kuwapatia kazi wanafunzi au wahitimu wa Vyuo hivi kulingana na ujuzi waliosomea ili kuwasaidia katika kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zihamasishwe katika kuchangia Vyuo hivyo, Wizara iwasaidie Wakuu wa Vyuo kupata mafunzo zaidi ya namna ya kuendesha Chuo na kuwa wabunifu ili kuziba pengo la ufinyu wa Bajeti na Wizara iwahimize wenyeviti wa Bodi kuitisha vikao vya Bodi kwa wakati muafaka hasa Wabunge wanapokuwa Majimboni. *(Makofi)*

Mhehssmiwa Spika, pia Serikali iongeze fungu kwa ajili ya kununulia vifaa na zana mbalimbali (vitendea kazi). Kwa upande wa mikopo kwa Wanawake, Kamati inapendekeza Wizara iendeleze zaidi utaratibu wa kuhakikisha kwamba Halmashauri za Wilaya zinatoa mafunzo/Semina kwa walengwa kabla ya kuwakopesha ili mikopo hiyo iwe ya manufaa kwao. *(Makofi)*

Pia Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ihakikishe kuwa asilimia za Halmashauri kwa Wanawake na Vijana zinatolewa na Wizara iandae orodha ya vikundi vilivyokopeshwa na kutoa taarifa kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ukeketaji, Wizara ilishauriwa kuwa uhamasishaji ulenge katika kutoa elimu zaidi kwa wazazi wote wawili (Baba na Mama) ili kukomesha vitendo hivi. Wanaume wakihamasika tatizo hili litakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chombo cha wanawake, Kamati imeshauri Wizara kuendeleza juhudi katika uundaji wa chombo cha wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake, Wizara iendelee kutekeleza agizo la mwaka jana la kuharakisha utaratibu wa kuanzisha Benki hii ya Wanawake kwa kuwa hatua zote za awali zipo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduhuli, Vyuo viruhusiwe kutumia fedha zinazokusanywa katika kuboresha Vyuo na hali ya maisha ya wanafunzi Chuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Wizara, Kamati ilishauri kuwa Wizara Kamati ilishauri kuwa Wizara iongezewe fungu la fedha ili ijenge Ofisi Dodoma badala ya ukarabati wa kila siku Dar es Salaam. Katika ujenzi huo pia Kamati ilishauri ujenzi uzingatie watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Kuhusu Wizara hii ina majukumu mengi sana ukilinganisha na Bajeti inayopata, tunapendekeza Wizara iongezewe Bajeti ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombiya fedha kwa mwaka 2003/2004. Baada ya majadiliano Kamati yangu iliombwa kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kiasi cha shilingi 5,266,365,600/=. Kati ya hizo, shilingi 1,373,079.400 zikiwa ni za Mpango wa Maendeleo na shilingi 3,893,286,200/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kusimamia ipasavyo utekelezaji wa shughuli zote zitakazoidhinishwa kwa kuzingatia maoni, ushauri na mapendekezo tuliyotoa, ikiwa ni pamoja na yale yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu na pongezi kwa wote walioshiriki katika kupitia, kujadili na hatimaye kukamilisha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wakiwemo Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Shamim Khan, Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Bibi Mary Mushi, Wakurugenzi na Wataalam wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, afisa mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, afisa Mwakilishi kutoka Hazina na Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa, bila kumsahau Katibu wetu wa Kamati Bibi Angelina Sanga, kwa kazi yake nzuri katika kuihudumia Kamati na hatimaye kuandaa maoni haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu wake naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43 (5) (b) (c) toleo la 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa idhini yako naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwashukuru sana kwa namna ya pekee wewe mwenyewe na Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa vyama vyote vyenye uwakilishi katika Bunge letu, bila kusahau Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, jinsi walivyonifariji baada ya kufiwa na Baba yangu Mzee Joseph Kasella-Bantu *(M.A),* hapo tarehe 29 Aprili, 2003 Dar es Salaam na kuzikwa Usongo, Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora. Ninawashukuru kila mmoja kwa aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapa pole Wabunge wenzangu waliofiwa na wazazi na watoto mfano Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Dada Janet Kahama na mumewe, Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa *Sir* George Kahama na wengine waliofiwa, wote nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awafariji na Roho za Marehemu wote hao wapate rehema kwa Mungu, wapumzike kwa amani. *Amin*. *(Makofi)*

Pia nawapongeza Wabunge wote waliofunga pingu za maisha na kupata wenzi wao, hongera sana na nawatakia maisha mema mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wabunge wote walioingia hivi karibuni Bungeni kutokana na chaguzi ndogo zilizofanyika na kwa aina ya pekee ninawapongeza Wabunge walioingia kupitia Chama cha *CUF.* Hongera sana kwa kuwa ngangari na kuhakikisha sera ya vipande mnakaa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kwa kuwa Kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani. Naamini kwa uongozi wake tutafanya kazi ipasavyo, tuliyokabidhiwa na wananchi wa Tanzania. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kuniacha niendelee kuwa Waziri ninayesubiri yaani *Shadow Minister* wa Wizara hii kwa mfululizo wa miaka nane sasa. Kwani kila anayesubiri yuko pamoja na Mwenyezi Mungu ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina Idara Kuu tatu yaani Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kambi ya Upinzani inatoa maoni yake kwa kila idara kama ifuatavyo:-

Maendeleo yaJamii, kwa kiasi kikubwa yanategemea utekelezaji wa sera ya Maendeleo ya Jamii kwa vitendo. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imejiwekea malengo mengi mazuri sana ya kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Mojawapo ya malengo hayo ni kuwa na Watalaamu wa maendeleo ya jamii wenye mbinu na stadi za uhamasishaji katika masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo mwanzo, hili ni lengo zuri kama litatekelezwa kwa vitendo. Tunachojiuliza ni kwamba watalaam hawa watapatikana wapi? Je, Wizara itaandaa wataalam hawa wenyewe? Je Wizara itaajiri wataalam walioandaliwa kwenye vyuo au nchi nyingine? Ni mitaala ya aina gani itakayotumika kutoa mbinu na stadi kuhamasisha maendeleo katika nchi kama Tanzania*?* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika dunia nzima, nchi yetu ni mojawapo ya nchi maskini sana duniani. Nchi yetu iko nyuma sana kiuchumi, kijamii, na kadhalika. Kuna viashirio *(indicators)* vingi vinavyoonyesha ukweli wa umaskini uliokithiri. Kwa mfano, ujinga, upungufu au ukosefu wa maji safi na salama, huduma duni za afya, lishe duni, uharibifu wa mazingira, ukosefu wa ajira, kipato kidogo cha Watanzania, ukosefu wa makazi na nyumba bora za kuishi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuna upungufu mkubwa au ukosefu wa huduma za jamii. Viashirio hivi vimefafanuliwa au vitafafanuliwa vizuri kwa undani na Wizara husika kama Wizara ya Afya, ELimu na Utamaduni; Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni zama za uwazi na ukweli. Hawa wataalam waliotajwa na Wizara watakuwa na mbinu na stadi zipi au kutoka wapi za uhamasishaji katika hali kama hiyo? Je, watahamasishaje masuala ya maendeleo katika umaskini uliokithiri kiasi hicho? Suluhisho la umaskini katika nchi yetu sio la miaka saba ua ishirini na miliwi ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu maskini hawezi kutambua matatizo aliyo nayo ili apange, atekeleze na kujiletea maendeleo. Kwa hali hiyo, masuala ya kijamii kama uzazi wa mpango, kujikinga na ugonjwa wa Ukimwi katika hali ya umaskini ni nadharia tu. Haki, uadilifu, utawala bora na uwazi ni mahubiri tu lakini utendaji ni kinyume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imetangaza sera, mipango na malengo ambayo yatatimizwa mwaka huu wa fedha. Kambi ya Upinzani inaipongeza Wizara hii pamoja na Wizara nyingine ambazo zimekuwa zikiahidi au zitaahidi mipango mbali mbali ya kuboresha huduma za jamii na maisha ya Watanzania kwa ujumla. Serikali na Wizara zake zikumbuke kuwa ahadi ni deni; lazima ilipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali ieleze wazi ni hatua gani zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayeshindwa kutimiza ahadi zake. Kama Serikali haitafanya hivyo, basi sisi Waheshimiwa Wabunge tuamue hatua za kuchukua pindi ahadi zisipotimizwa. Bila kufanya hivyo, wimbo utaendelea kuwa ule ule yaani kutokana na Bajeti finyu au hali ngumu ya uchumi, ahadi fulani haijatekelezwa. Uzoefu katika nchi yetu unaonyesha kuwa hakuna matatizo katika kupanga na kuahidi, tatizo ni utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Jamii yana uhusiano wa karibu na taaluma katika nyanja hiyo ambayo kwa nchi yetu, hutolewa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs),* Vyuo hivi vina matatizo mengi makubwa. Majengo na miundombinu ya Vyuo vyote 58 vya Maendeleo ya Wananchi kote nchini yamechakaa sana. Majengo na Ofisi za vyuo zina hali mbaya. Pia kuna upungufu mkubwa wa vifaa. Ukarabati wa hali ya juu unatakiwa. Bila kufanya hivyo, afya za wanavyuo wanaosoma katika vyuo hivyo, wakufunzi wao na wafanyakazi wote kwa ujumla zipo hatarini. Licha ya Wizara kutenga fungu la kukarabati vyuo hivyo, pia Wizara iviruhusu vyuo kutumia fedha zinazokusanywa ili kuboresha vyuo na hali ya wanafunzi vyuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahitimu wa vyuo hivi wana tatizo la ajira kama ilivyo kwa vijana wengi wa Tanzania. Wizara hii ifanye kila linalowezekana ili vijana hawa wasiachwe pembeni *(Marginalization).* Ujuzi wao utumiwe na Halmashauri baada ya kuhimizwa na Wizara. Halmashauri ziwapatie kazi wahitimu wa vyuo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara nyingine kubwa ya Wizara ni Maendeleo ya Jinsia. Kumekuwepo na tafsiri tofauti ya neno Jinsia. Kuna watu wanaodhani jinsia ni wanawake. Jinsia, ni mahusiano yaliyopo kati ya wanaume na wanawake. Jinsia ni tabia na majukumu yanayotimizwa na wanaume au wanawake kutegemeana na matarajio, mila, desturi na utamaduni wa jamii fulani. Kwa hiyo, jinsia haimaanishi wanawake kama baadhi ya watu wanavyodhani au kufikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi katika Tanzania ni maskini kuliko wanaume pamoja na ukweli kuwa wanawake ndio wazalishaji wakuu. Siyo hivyo tu bali, wanawake ni wengi kuliko wanaume. Mwaka 1995, ilikadiriwa kuwa asilimia 51.6 ya Watanzania wote ni wanawake. Pia asilimia 54 ya Watanzania wanaojihusisha na uzalishaji vijijini ni wanawake. Takwimu zilionyesha kuwa asilimia 98 ya Watanzania wanaojihusisha na uzalishaji vijijini wanafanya kazi za kilimo. Asilimia 60 hadi asilimia 80 ya mazao ya chakula na biashara huzalishwa na wanawake ikiwa ni pamoja na kufanya kazi nyingine nyingi za nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wao mkubwa kwa jamii, hawapati mapato au malipo yanayolingana na kazi zao au wanavyostahili. Mila, desturi na utamaduni bado ni vikwazo kwa maendeleo ya wanawake hasa katika kumiliki ardhi na mali nyinginezo. wanawake hawana uamuzi/usemi juu ya mapato yanayopatikana. Bado wanaume wanaendelea kuwa na sauti kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi za ajira kwa wanawake ni chache sana. Matokeo yake, wanawake wanajihusisha na kazi ndogo ndogo zisizokidhi mahitaji. Pia wanawake wachache sana, wanaweza kupata mikopo ili kupanua au kuanzisha biashara ndogo ndogo au kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu, msichana ana nafasi finyu ya kuanza na kuendelea na masomo. Pamoja na msisitizo wa elimu kwa watoto wote, uandikishaji wa wasichana katika shule za msingi ni mdogo kuliko wa wanafunzi wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wa kwenye majimbo yetu unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya wanaume ndiyo wenye mamlaka na uamuzi mkubwa katika uchumi, siasa, elimu na utamaduni. Hali hii imekuwepo kwa muda mrefu, kabla ya wakati na baada ya ukoloni. Unyanyasaji unakuwepo kuanzia utotoni katika familia zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna mgawanyo wa kazi za wasichana na wavulana, kuna michezo ya wasichana na michezo ya wavulana. Angalau sasa wazazi na watu wazima wanajaribu kuleta mabadiliko katika jamii. Tunaomba basi watoto wapewe malezi sawa bila kujali jinsia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasi na ubaguzi huu umekuwa ukisababisha matokeo mabaya ya masomo shuleni na vyuoni kwa msichana. Mitizamo hasi juu ya mwanamke katika jamii pia ni matokeo ya unyanyasaji kijinsia, kwa mfano, mjadala juu ya nafasi za upendeleo. Hata vyombo vya habari hutilia maanani habari zihusuzo wanaume kuliko wanawake.

Pia masuala ya Sheria ya Ndoa, Matunzo ya watoto wanaozaliwa nje ya Ndoa, Mirathi, Wosia na kadhalika, kadri zinavyochelewa sheria hizi kupitishwa kufuatana na wakati, zinaongeza watoto wa mitaani, yatima wasio na msaada wowote na zaidi gonjwa la Ukimwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mgawanyo wa kazi usio sawa katika familia zetu, wasichana wengi huchelewa shule au kukosa masomo. Mwanafunzi wa kike akipata mimba, adhabu ya kufukuzwa shule humwangukia peke yake. Hakuna juhudi zozote zinazochukuliwa kutafuta na kumwadhibu mvulana aliyempa mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu wakati wa Uhuru mwaka 1961, Serikali ilitangaza vita dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini. Lakini mpaka sasa baada ya miaka 40 kupita, nusu ya Watanzania wote ni maskini na wengi wao wanaishi katika ufukara mkubwa. Hivyo basi katika kipindi cha miaka 40 umaskini uliokithiri bado uko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa mkakati wa kupunguza umaskini Tanzania *(PRSP)* unalenga kutokomeza umaskini Tanzania mpaka mwaka 2025. Swali sasa, Serikali hii imeshindwa kumaliza tatizo la umaskini uliokithiri katika kipindi cha miaka 40 iliyopita, je, itaweza kutokomeza umaskini kwa kipindi cha miaka 22 ijayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *New Partnership African's Development (NEPAD).* Makusudio ya Afrika nzima ni kutokomeza umaskini ifikapo mwaka 2015. Sisi Tanzania mpaka 2025, hii ina maana sisi tutabaki nyuma miaka 10 ya nchi nyingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninaendelea kuzungumzia maendeleo ya mwanamke. Sera ya Maji tuliambiwa ifikapo mwaka 2002 maji yatakuwa yameenea Tanzania nzima. Lakini mpaka leo mwaka 2003 tatizo la maji liko pale pale, je, tutafika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma za afya mpaka leo kuna baadhi ya Wilaya kama Ngorongoro ambazo hazina hata Hospitali ya Wilaya ya Serikali. Hii haionyeshi kuwa Serikali inalipa vituo vya afya uzito unaostahili na hata huko ambako kuna hospitali au vituo vya afya vya Serikali, huduma zake siyo za kuridhisha. Wananchi hasa akinamama wanalazimika kujinunulia wenyewe dawa na vifaa vya kujifungulia watoto licha ya kuchangia gharama za huduma ya afya pamoja na kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi chote hiki toka Uhuru, Serikali haijaweza kutoa huduma muhimu na za msingi kama vile elimu, afya na maji safi na salama kwa wananchi wake Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa hali hii ya uonevu, unyanyasaji na ubaguzi wa kijinsia na jamii yetu iendelee ipasavyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kupitia Wizara hii ifanye yafuatayo:-

Kwa kuwa Wizara hii ndiyo inafikisha (tendaji) sera zote kwa jamii *(to the grass root)* na jamii ni wanawake, wanaume, watoto, walemavu, vijana na wazee, basi kwa misingi hiyo Wizara iongezwe fedha za kutosha haswa ili iwe na nyenzo za kutosha yaani baiskeli, pikipiki na kadhalika. Mishahara ya kutosha

kwa wafanyakazi wake (ajira na ujira) na motisha ili Wizara ifanye kazi ipasavyo kufuatana na sera zilizopitishwa na kwa wakati muafaka. Vinginevyo tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu pamoja na uzuri wa sera bila utekelezaji. *(Makofi)*

Serikali ihakikishe huduma za jamii zinapatikana na zinatolewa sawa kwa jinsia zote. Kwa mfano, huduma za maji zipatikane karibu na wananchi ili wanawake ambao kwa kiasi kikubwa huchota maji wasipoteze muda mwingi kufuata maji kwa umbali mrefu. Serikali ihakikishe maji ya mabomba, visima, na kadhalika yanapatikana karibu au kwenye makazi ya wananchi wote ili wanawake waweze kushiriki katika shughuli nyingine za maendeleo na kujikwamua kijamii, kisiasa na kiuchumi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izidishe utoaji wa elimu kwa wanawake ili watambue haki zao na kuzidai. Elimu pia itasaidia kuondoa imani zisizo sahihi juu ya mahusiano ya mwanaume na mwanamke. Kwa mfano, lisiwepo kabila ambalo linaamini kuwa bila kupigwa na mume wako haupendwi, mila hizi zinahalalisha wanaume kuendelea kuwanyanyasa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi za uzalishaji mali hasa kwenye kilimo, Serikali iagize mashine kama trekta na mashine za kusaga ili kupunguza kazi nyingi za akina mama Vijijini, kama kilimo na kutembea umbali mrefu kwenda kusaga nafaka ili kupata unga wa chakula. Pia, ili kuhakikisha afya za wanawake zinakuwa nzuri, Serikali ihakikishe elimu ya uzazi wa mpango inaendelezwa kwa wananchi wote ili wajue njia za kupanga idadi ya watoto kwa kushirikiana kati ya wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine ya kuwakomboa wanawake wa nchi hii ni kuwaelimisha wasikimbilie mikopo kwa sababu mikopo ni deni bali wabadili tabia na kujifunza kuweka angalau kidogo kila siku kwani ndondondo si chururu yaani akiba na kukopa na kukopa kwa mipango thabiti kwa biashara itakayolipa deni na kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mikopo inayotolewa kwa wanawake na Halmashauri za Wilaya, Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa jambo hilo, lakini mikopo hii imekuwa ikitolewa bila kutoa mafunzo au semina kwa walengwa. Matokeo yake ni kwamba mikopo hiyo imekuwa na manufaa kidogo kwa wanawake. Tatizo lingine ni kwamba mikopo hiyo huwa inatolewa kwa vikundi vichache vya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri mikopo hii itolewe kwa wanawake wote bila kujali itikadi zao au ubaguzi wa aina yoyote na kwa wale tu walio tayari kukopa na wanaojua deni lazima walipe na deni si msaada ndio wapewe mkopo. Sio kupelekewa fomu nyumbani na wengine wanasota mpaka soli za viatu zinakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iongeze Bajeti ili vikundi vingi zaidi vya wanawake vipewe mikopo licha ya kuisaidia Wizara kutekeleza majukumu yake vizuri. Pia semina au mafunzo yatolewe kwa vikundi vya akina mama ili mikopo iwe na faida kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la ajira, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na fursa sawa za ajira kwa wanawake na wanaume. Kama kuna Mashirika, Makampuni na Taasisi ambazo zinakataa kuajiri wanawake kwa kuhofia likizo za uzazi, basi zichukuliwe hatua za Kisheria pindi ikibainika hivyo na ushahidi kupatikana. Tunaishauri Serikali na hasa kwenye ajira ya nafasi za kuteuliwa, iwape wanawake kipaumbele bila kujali itikadi zao. Tukitegemea wanawake wakapambane na wanaume kwenye upigaji kura, hatutafanikiwa kutokana na mtazamo hasi *(Negative Attitude)* kwa jamii yetu juu ya jinsia ya kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2002/2003, Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii iliagiza kuainishwa kwa Benki ya Wanawake pamoja na uundaji wa Chombo cha Wanawake. Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na kasi ya utekelezaji wa agizo hilo la msingi kwa maendeleo ya nchi yetu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri afafanue kasi ya utekelezaji wa agizo hilo la Kamati kwa niaba ya Bunge. Vile vile, Kambi ya Upinzani inakubaliana na kuanzisha chombo kwa ajili ya wanawake, lakini wasibaguliwe wanawake wanasiasa iwapo chombo hicho kinawatayarisha wanawake waende katika Mabaraza ya

maamuzi, sasa ukiishaingia kwenye Mabaraza ya uamuzi unabaguliwa. Sasa ubaguzi wa wanawake kwa wanawake haufai, chombo lazima kiwachukue wanawake wote na wa aina zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanaopata mimba wakati wa masomo, waruhusiwe kujifungua na kulea watoto wao, kisha waendelee na kumalizia masomo yao. Si hivyo tu, bali wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shuleni hasa wa kike waandikishwe wote. Shule zaidi za wasichana zijengwe na Serikali ibuni mbinu mpya za kuwahamasisha wanafunzi wa kike wasome masomo ya sayansi kama fizikia, kemia na uhandisi, badala ya kuyakimbia na kudai ni masomo ya wanaume au ni masomo magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliagizwa na Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii ijenge Ofisi Dodoma badala ya kuendelea kutumia pesa nyingi kukarabati Ofisi ya Wizara Dar es Salaam. Lakini Wizara imesema imejiwekea lengo la ujenzi wa jengo jipya la Ofisi, Wizara haijaeleza jengo hilo litajengwa wapi, Dodoma au Dar es Salaam, je, Wizara ikisema ujenzi wa jengo jipya inamaanisha ukarabati au ikisema ukarabati inamaanisha ujenzi wa jengo jipya? Tunaishauri Wizara itekeleze agizo la Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya watoto pia yanashughulikiwa na Wizara hii, kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Afya, Elimu na Utamaduni. Idara ya watu katika jamii yoyote huongozwa na idadi ya watoto wanaozaliwa, wanaokufa na idadi ya watu wanaohama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kutokana na sababu mbali mbali. Ukilinganisha na nchi nyingine, idadi ya watoto wanaozaliwa ni kubwa na pia idadi ya watoto wanaokufa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanyika mwaka 1997 unaonyesha kuwa kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa Tanzania, 96 wanakufa, ukilinganisha na watoto saba tu katika nchi zilizoendelea. Vifo vya akina mama wanaojifungua ni kati ya 200 na au 400 katika wanawake 100,000 wanaojifungua. Kwenye nchi zilizoendelea vifo kama hivyo ni 95 tu kati ya 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni kiashirio cha umaskini tulionao hasa kwa upande wa huduma za jamii. Huduma za afya ni duni sana. Watoto ni viumbe visivyo na hatia yoyote, hata Misaafu ya dini inasema hivyo. Wafuasi wa Manabii waliambiwa wawaache watoto waende kwa Mungu. Maandiko Matakatifu yanatuasa tuishi kama watoto na tukiwakosea watoto tumemkosea Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kuwa inatenda dhambi kwa Mungu kama inahusika moja kwa moja na idadi ya vifo vya watoto vilivyotajwa hapo juu. Hii ni pamoja na vifo vya akinamama wajawazito. Hali hii pia inawahusu Madaktari ambao husaidia kuwatoa mimba wanawake kwa kificho. Serikali iboreshe huduma za afya ili kupunguza vifo vya watoto na wajawazito. Hii itatusaidia kupata nafasi mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wimbi la kujifungua na kutupa watoto vyooni au sehemu yoyote linazidi kuwa kubwa katika nchi yetu. Pamoja na ukweli ulio wazi kuwa chanzo chake kikubwa ni umaskini. Tunahisi kuwa kuna sababu nyingine zaidi. Kwa mfano, wanafunzi wanaopata mimba hujifungua kwa siri na kutupa watoto wakihofia kufukuzwa masomo. Wanafunzi wengine hutoa mimba kwa kificho kwa hofu hiyo hiyo.

Kwa maana hiyo, Serikali ifute sheria au utaratibu wa kumfukuza mwanafunzi masomo baada ya kupata mimba. Mwanafunzi akishapata mimba atoe taarifa kwenye uongozi wa shule mapema ili aruhusiwe kwenda kutunza mimba na kujifungua. Baada ya kujifungua apewe likizo ya miaka mwili au mitatu ya kumnyonyesha mtoto wake na kisha arudi kuendelea na masomo yake katika shule ile ya awali au ahamishiwe shule nyingine. Kwa kufanya hivyo, wimbi la kujifungua na kutupa watoto litapungua na pia wanafunzi wetu au wasichana wetu wafundishwe kwamba kutenda tendo la ngono siyo kuzaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezuka wimbi la watoto omba omba, watoto hawa hukaa kando kando ya barabara na wengine huzunguka na wazazi au jamaa zao, hii ni pamoja na watoto wa mitaani. Tuna watoto wa mitaani lakini hatuna wazazi wa mitaani. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iwakamate watoto hawa na kuwahoji kwa kina. Kama itaonekana wazazi wao hawajulikani, basi wafunguliwe Makambi na kutunzwa pamoja badala ya kuzurura ovyo mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na taarifa za kusafirishwa watoto wa Tanzania kwenda kufanya kazi za nyumbani nchi za nje hasa Uarabuni. Taarifa hizi zimekuwa zikitolewa na vyombo vya habari kadri ya habari hizo, watoto hawa wakifika huko hufanyishwa vitendo vya kinyama ikiwa ni pamoja na kufanyishwa mapenzi na wanyama kama mbwa. Tunaitaka Serikali ifanye utafiti juu ya suala hili ili ukweli ubainike na hatua kali za Kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika ili kuondoa hali hii ya udhalilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tunasisitiza kuwa maendeleo ya jamii yanategemea sana usawa wa kijinsia na utekelezaji wa haki za wanawake na watoto. Kukiwa na ubaguzi, unyanyasaji, unyonyaji wa jinsia fulani pamoja na watoto, hatutakuwa na maendeleo. Pamoja na kuishauri Serikali isimamie uboreshaji wa hali hii, pia sisi Wabunge tuwaelimishe watu katika Majimbo na sehemu zetu tunazopita zote ili matatizo yaliyoelezwa kwenye hotuba hii yapungue kama siyo kuisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji walioomba kuchangia mpaka sasa katika Wizara hii ni watu 15. Kwa uzoefu wetu ni kwamba siku nzima hawawezi kuzidi watu 12. Sasa kuna ambaye hakuchangia kabisa yuko mtu mmoja, waliochangia mara moja wako wawili, waliochangia mara mbili wako saba, waliochangia mara tatu wako wanne na waliochangia mara nne yuko mtu mmoja. Sasa aliyechangia mara nne naomba asifikirie kama ataitwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukushukuru kwa kuweza kupata nafasi ya kwanza ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema kitu chochote ningependa kutoa shukrani zangu za dhati na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na uongozi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ningependa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wote wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wa CCM. Tunawakaribisha katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu mikopo ya wanawake. Ningependa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kutoa mikopo hii ili iwafikie wanawake na waweze kupunguza ukali wa maisha. Lakini ningependa kulizungumzia jambo moja ambalo nafikiri lingekuwa ni vema likaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa mikopo Wizara ilikuwa imemega kiwango fulani cha kuwapa wanawake. Lakini nahisi kiwango hiki tukifikirie upya ili kiweze kuongezwa kwa mfano shilingi 50,000/= labda kwa mtu mmoja inakuwa ni vigumu kwa maisha ya leo. shilingi 50,000/= ni pesa lakini si pesa za kuweza kukidhi haja ya mtu ambaye anaweza akazalisha na kuongeza kipato chake cha kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vema tuongeze kipato hiki ikiwa kwa mtu mmoja mmoja au ikiwa ni kwa Vyama vya Ushirika kwa sababu pengine tunaweza tukachukulia Vyama vya Ushirika vina watu kama 10, inawezekana pengine watu wakigawana haifiki hata hiyo shilingi 50,000/=, inaweza ikawa chini ya hapo. Kwa hiyo, mtu inakuwa bado hatujamsaidia ili aweze kujiongezea kipato chake cha kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri nia yake ilikuwa ni nzuri lakini kila mwaka ikiongezeka na maisha yanazidi kuwa magumu zaidi na ukali wa maisha unaongezeka. Kwa hiyo, nafikiri ingekuwa ni vema Mheshimiwa Waziri akalifikiria upya suala hili, akaongeza zaidi ya mikopo hii ili iweze kuwafikia wanawake na waweze kujisaidia katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba katika mikopo hii wanawake wengi hawana taaluma ya kuitumia mikopo hii. Utaona kwamba wengine wana nia nzuri ya kuweza kuirudisha mikopo hii lakini wanashindwa kutokana na elimu kuwa ndogo. Elimu ya matumizi ya mikopo na urudishaji wa mikopo itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alizungumza hapa kwamba kuna baadhi ya Mikoa hawajarudisha mikopo hii mpaka leo lakini kuna baadhi ya Mikoa wamerudisha, umetajwa Mkoa wa Mtwara hapa, Mikindani. Tunapenda kuwapongeza watu wa Mkoa huo na wanawake wa Mkoa huo walioweza kurudisha mikopo hii kwa sababu hii mikopo imekuwa kama *Involving Fund*, watu wanaweza wakachukua, wakarudisha, wakakopa na wengine wakarudisha. Sasa ikiwa kama wanawake wengine hawawezi kuirudisha hii mikopo wanawake wengine watashindwa kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili suala la elimu tulitilie maanani zaidi ili kuweza kuwafundisha wanawake kwa kupitia vikundi maalum vya kutoa elimu ili waweze kupata elimu zuri zaidi na waweze kuilipa mikopo hii ambayo inatakiwa ilipwe kwa mwanamke ambaye anaweza kujihusisha na kupata faida katika mambo yake ambayo amejipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la maonyesho ya biashara. Katika suala hili napenda kumpongeza vile vile Mheshimiwa Waziri. Maonyesho haya chanzo chake ni mashirikiano, si kwa Wizara hii tu peke yake ila ikiwa ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara katika kuweza kuwaunganisha wanawake wawepo katika mabanda ya maonyesho ya biashara ili wapate kuonyesha biashara zao na vile vile kuuza biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulikuwa na mpango mzuri zaidi katika kipindi cha nyuma, japokuwa wanaendelea lakini hauendelei vizuri kutokana na Wizara hizi mbili, Wizara yetu hii ya huku Bara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Wanawake, Ajira na Maendeleo ya Watoto kwa upande wa Zanzibar, walikuwa wanashirikiana vizuri ili kuwahusisha wanawake wa upande wa Zanzibar na wao waje Dar es Salaam ili waweze kuona jinsi gani ya kuweza kushirikiana na wanawake wenzao.

Haya yanaendelea kutokea lakini naona kidogo hatukuwapata wanawake wengi ili kuweza kuja kushiriki katika maonyesho haya kwa sababu pengine kuna sababu kadhaa ambazo zimeweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiria hili suala tulitilie maanani zaidi ili wanawake wa kule nao, licha ya kwamba wanakuja kuuza biashara zao lakini watapata mashirikiano na wanawake wenzao kibiashara kwa sababu tumezoea zaidi kisiasa na Kimuungano lakini kibiashara kwa wanawake wa Zanzibar na wa huku Bara bado haujawekwa mkakati mzuri zaidi ili waweze kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mama Anna Mkapa. Kwanza, napenda kumpongeza kutokana na mwaliko ambao umetupa sisi Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kushiriki katika maonyesho haya na kuona jinsi gani wanawake wanavyojishughulisha na mambo ya biashara na vile vile jinsi gani walivyokuwa na harakati ya kujitazama na kujishughulisha zaidi na mambo yao ya biashara. Kwa hiyo, hili ni jambo nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumepata mwaliko huu lakini Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, ana desturi ya kutuunganisha sisi wanawake kutokana na *NGO* yake ya Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF)*. Inawakusanya wanawake hawa wa Mikoa mbalimbali wakishirikiana na Wizara hii ili nao wawe karibu na wanawake wenzao na kuona jinsi gani ya kubadilishana mawazo na wanawake pengine wa Kenya, Uganda na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kumpa pongezi nyingi zaidi ili aendelee na ushirikiano huu wa kutuunganisha sisi wanawake Watanzania na wa nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kulizungumzia suala moja la kuhusu kuwaleta wanawake Dar es Salaam katika maonyesho. Wanawake hawa wanauza kwa kipindi kile cha maonyesho tu, lakini maonyesho yale ya Saba Saba yakimalizika, wanawake hawa bado wanakuwa wanahangaika na

kupata soko la kuuza bidhaa zao. Bado Wizara haijashughulika na kutafuta soko la nje la bidhaa za wanawake hawa Watanzania ili wapate kuuza bidhaa zao nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba bidhaa za wanawake hawa ni nzuri tu, kuna bidhaa nyingi ambazo wanaweza wakatengeneza ni nzuri na pengine kwa kile kiwango cha Kimataifa lakini wanashindwa wapate wapi soko na wanatuuliza wanawake wenzao kwamba, jamani kweli sisi mnatuambia tuje katika maonyesho ya Saba Saba lakini tukirudi bidhaa zetu zinalala, hatuna masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Wizara hii ya Ushirika na Masoko, itakuwa ni jambo la busara mkashughulika ninyi na haya mambo ili hawa wanawake wenzetu waweze kupata soko katika bidhaa zao. Mpaka sasa hivi huwa wanalalamika sana, bidhaa zinawalalia tu na hawajui wafanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni kwamba ningependa kuzungumzia kuhusu janga letu hili la Ukimwi. Kwa kweli Ukimwi ni janga la Taifa, jamii yetu inaathirika na hususan wanawake na vijana vile vile wanaathirika. Sisi wanawake tunaathirika kutokana na wimbi kubwa ambalo linatugusa na malengo mbalimbali au mambo mbalimbali ambayo yanatufanya tuathirike kwa wingi zaidi.

Kwa mfano, wanawake ndio tunaobakwa, wanawake ndio tunaolaghaiwa, wanawake ndio tunaoathiriwa, wanawake ndio tunaorithiwa na wanaume ambao wake zao wamekufa pengine yule mwanaume anakuwa amekwishaathirika na Ukimwi halafu unaambiwa uolewe naye na wewe huwezi kujua na huwezi kupinga mila hizi potofu, kwa hiyo inabidi uathirike na Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanawake tunaathirika kutokana na ukeketwaji. Kwa hiyo, nafikiri hili suala la Ukimwi linatuathiri sana sisi wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba kuna baadhi ya mila hizi potofu inabidi ziangaliwe na zitolewe taaluma kwa wale watu ambao wanapenda kuzipepelea hizi mila ambapo moja nimeisema hapa ya kurithiwa na ya pili niliyoisema ni ya ukeketaji. Mambo haya yanatufanya sisi tupate Ukimwi kwa haraka.

Kwa hiyo, nafikiri Wizara ibebe jukumu la kutoa elimu. Elimu ya semina tu au semina hizi zikafanyika Dar es Salaam katika Vijiji na kwingineko semina hizi hazifiki, bado wanakuwa hawajapata taaluma na hususan wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Wizara hii ichukue jukumu zaidi la kuwaelimisha wanawake na hata wanaume vile vile kwa sababu kama suala hili la kurithiana mtu anaona kaka yake amekufa na halafu na yeye anajipeleka hapo hapo, ni kwamba haya mambo yamekwishapitwa na wakati. Kwa hiyo, nafikiri ni jambo jema taaluma ikatolewa kwa wanawake na kwa wanaume vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kusema kuhusu haya mambo ya Ukimwi kwamba bado athari tunayo na hususan wanawake tunaathirika lakini dawa ya Ukimwi tunayo sisi wenyewe Watanzania. Kwa nini nimesema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu dawa hii ambayo ninaweza nikaiita *K5,* ni maneno ambayo sisi wenyewe tunayo na elimu yetu sisi wenyewe tunayo. Kuna mambo matano ambayo ninaweza nikayasema, kwanza, ni kujilinda, pili, kujielimisha, tatu, kuacha kuzini, nne, kuishi na mtu mmoja na ya mwisho ni kubadilisha tabia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri niichukulie hii ya mwisho ya kubadilisha tabia. Kubadilisha tabia ni dawa kubwa ya Ukimwi kwa sababu wewe mwenyewe utakuwa unajisema kwamba mimi sasa hivi ninaacha, kama nilikuwa ninayafanya haya mambo sasa hivi ninaacha, nimeamua kuishi na mtu mmoja, basi hiyo itakuwa ni dawa ya Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliko huku unakwenda kuchukua kondomu, huku unapata semina na bado unakwenda vichochoroni tu, sasa tutauondoa vipi Ukimwi? Hautakwisha na tutaendelea kuwa na

Ukimwi kwa sababu bado tabia inakuwa iko pale pale, ukiona mwanamke anapita, msichana wa umri wa mwanao unamwandama, unasema nitakula muhogo tu kila siku sionji na wali eeh!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya maneno ni maneno potofu, haya ni lazima tuyabadilishe, huo wali si umeuweka kwako na ndio maana ukauona mzuri ukauweka ndani, leo kinacho kuhangaisha ni kitu gani kwenda kupapatika na vichangudoa vya nje? Mimi nasema ni kubadilisha tabia, ubadilishe tabia wewe mwenyewe, hapo ndio Ukimwi utakapopungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano wa Uganda. Uganda walikuwa na wao wana matatizo haya ya Ukimwi na walitupita kwa sababu *percent* kubwa ya watu wao walikuwa wameathirika na Ukimwi. Kutokana na tabia yao inasemekana ilikuwa siku ya Jumamosi anakuja shoga yako ambaye ni shoga yako unayempenda, unampisha nyumba, unatoka wewe unakwenda kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi tabia za mila potofu zikawa zimewafanya watu wa Uganda waathirike sana kutokana na tabia hizi na mila hizi. Lakini nafikiri kwa sisi wenyewe hapa Tanzania mila hizo hatuna isipokuwa yale niliyoyasema kwamba kuna baadhi tunaathirika kwa yale ambayo niliyokuwa nimekwishayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nafikiri tubadilishe tabia, hilo ndiyo jambo kubwa haswa, isiwe mimi kila siku nakula muhogo basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa nia moja ya utendaji wao ulio mahiri katika Wizara hii kwa sababu nina imani kuwa wako bega kwa bega Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wake ndio maana mambo yanakuwa mazuri, yanafanikiwa na yanakwenda kama yanavyopangwa, tuseme yanakwenda kwa mambo ya kisasa kutokana na wao wenyewe jinsi walivyo, ukimwona Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na hata Katibu Mkuu unaweza ukasema wote ni mapacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchangia katika sehemu kuu zilizo tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, naomba kuchangia sehemu inayowahusu vijana, wanawake ambao wanasoma shule za msingi na pia shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niliweza kuliongelea katika Wizara ya Elimu na Utamaduni lakini pia nimeona itakuwa vizuri zaidi kuongea katika Wizara Mama ambayo ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako vijana ambao wanasoma katika shule hizo na bahati mbaya huweza kupata mimba, kama alivyoongelea Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu.

Vijana hawa wanapata mimba lakini wanaowapa mimba zile wapo na wanajulikana kama ni Walimu au wafanyakazi wengine ambao wako nje sio Walimu, lakini wapo Walimu ambao wanashirikiana na vijana hao kimapenzi mpaka kuwapa mimba. Matokeo yake mwanafunzi yule atatolewa katika masomo, Mwalimu atabadilishwa kituo cha kazi. Mfano hata kwenye *ITV* kuna mchezo mmoja unaitwa Jahazi wanaonyesha jinsi Mwalimu anavyomfuatilia msichana yule na wako katika mikakati ya kumkamata, mambo yale ni kweli yanatokea.

Je, Wizara ina utaratibu gani wa kuwasaidia vijana wetu kwa kuleta sheria itakayowasaidia waweze kuendelea na masomo yao na italetwa lini? Kwa sababu wale wanawake wana haki ya kuendelea na elimu lakini wanaikosa na ni kinyume cha haki za binadamu kwa sababu yule mwanamke kila siku atabaki nyuma na sisi wanawake tunahitaji kuzidi kushirikiana ili vijana hawa waje kuwa viongozi wa baadaye. Kama sasa hivi tukiwaacha wakikosa elimu ile kwa asilimia kubwa watakuwa nyuma kabisa na hata huu umoja tunaolilia wa mwanamke kuwa kiongozi kama tutaliachia sasa hivi itakuwa ni vigumu sana mwanamke huyu kuongoza. *(Makofi)*

Vile vile napenda kuzungumzia Sheria ya Mirathi. Zipo Sheria za Mirathi za Kimila, Kiserikali na za Kidini na zote kwa kweli ni nzuri. Tukiangalia Sheria za Mirathi za Kimila ni nzuri lakini zina kasoro zake, za Kidini ni nzuri sana lakini sisi wenyewe ndio tunazipotosha kwa sababu ile ni sheria tunatakiwa kuifuata jinsi ilivyo lakini tunafanya kinyume. Bunge lililopita nilizungumzia kuhusu mtoto wa nje ya ndoa kwamba, naye anatakiwa apate urithi wake, lakini bahati mbaya au nzuri kuna gazeti ambalo liliandika kwamba, mimi namtetea mtoto ambaye yuko nje ya ndoa. Ni kweli mtoto wa nje ya ndoa Kidini mtoto yule hatambuliki, lakini kama mtoto hatambuliki baba yake aliwezaje kwenda kumtafuta nje ya ndoa? Kwa sababu hiyo hiyo dini yetu inatuambia usifanye zinaa lakini unaifanya na matokeo yake unaenda kumtafuta mtoto yule. Je, kwenye sheria kama kweli tunafuata dini yule mtoto ana makosa au baba ndio mwenye makosa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani asilimia kubwa baba au mama yule ndiye mwenye makosa kwa sababu wao ndiyo wamekiuka sheria ile ya dini ambayo inawakataza kufanya vile. Kama mtoto amezaliwa na ametambulika na baba amekubali kuwa ni mtoto wake wakati wa mirathi ndio unamtoa, je, kama sheria ina haki zake na kuna sheria ya dini inayosema mtu anayefanya zinaa apigwe mawe mpaka afe ...

**MBUNGE FULANI:** Mbona hamuwapigi?

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Kutimiza sheria ya dini? Kwa nini tusingeanza kumpiga yule baba mawe mpaka afe kusudi tumwache yule mtoto? Zote hizi hatufuati tunamwangalia tu yule mtoto anayezaliwa nje ya ndoa. Mimi naona mtoto yule hana makosa na lazima haki yake apewe na atunzwe kutokana na sheria hiyo hiyo ya dini tukiingalia kwa upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mirathi upande wa mwanamke, kutokana na maumbile aliyoumba Mwenyezi Mungu, yuko mwanamke ambaye atazaa watoto mpaka 24, 12, 2, 1 na mwingine hazai kabisa. Lakini yuko huyu mwanamke ambaye ameolewa wanaishi na mumewe kwa mapenzi hakubahatika kuzaa. Yeye anajua mume wangu naishi naye kwa mapenzi anatoka nje kama alivyosema anazaa au mwingine anaruhusiwa kuoa mke mwingine kwa sheria za dini hata wanne lakini sasa huyu mmoja mume wake atakapofariki hapati chochote, anapata thumni na inaweza kuwa shilingi laki mbili au shilingi 50,000/=. Je, hapo haki iko wapi kwa huyu mwanamke ambaye hakuzaa lakini amechangia nguvu zake pale. Sasa jamani lazima tuangalie hizi sheria nyingine, muda unakwenda, wakati unakwisha na wako wanaoathirika mama zetu wanateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mifano mingi ambayo tunaweza kuelezea, wako akina mama ambao hawakuzaa na yule bwana amezaa nje ya ndoa anapokufa yule mwanamke anatolewa kwenye nyumba anaambiwa wewe hukuzaa kwa hiyo haki yako hapa haipo, chukua hizi shilingi laki mbili ukaaenze maisha, umri wake ni miaka 50 hivi atakwenda kuanza maisha gani kwa shilingi laki mbili? Kwa hiyo, anapata taabu, muda wake mwingi ameupoteza akiwa na yule mume wake mpaka kufikia kumuuguza pengine au anaweza kuwa yule mwanaume amekufa kwa maradhi haya ya sasa hivi kila mmoja anaelewa sasa yule mwanamke ataenda wapi na dunia ya sasa hivi kila mmoja anajua yeye na familia yake yaani mume, watoto amehaingaika sana anaweza akamchukua mtoto wa dada yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo sisi tunahitajika sana kuangalia ni watoto yatima. Namshauri Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake, utaratibu wake na mipango yake aliyoipanga kuelimisha jamii nzima kuhusu kuwalea watoto yatima kwa ndugu zao na wasio ndugu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikwenda kutembelea Kituo kimoja cha Watoto Yatima, nikamkuta msichana mmoja amembeba mtoto wa miezi mitatu anampeleka kwenye Kituo cha Watoto

Yatima. Nilimwuliza hivi huyu mtoto ni wa nani au umempata wapi? Akaniambia huyu mtoto ni wa mdogo wangu ambaye amefariki. Nikamwambia kama ni mtoto wa mdogo wako inakuwaje umlete huku kwenye Kituo cha Watoto Yatima? Akaniambia mimi mwenyewe nina mtoto wa miezi sita kwa hiyo siwezi kumlea. Pale pale nilimwambia wewe huna imani au mapenzi na yule ndugu yako aliyefariki. Kama amefariki yeye ina maana hakuwa na kitu chochote kwa ajili ya mtoto huyo mfano kitanda na godoro? Akaniambia alikuwa navyo viko nyumbani akikua atavikuta. Kitu ambacho sio kweli godoro na kitanda atalalalia yeye na familia mpaka vitakwisha yule mtoto ndio atakua. Kwa hiyo, yule mtoto atakulia kwenye mazingira ya watoto yatima hata kile kidogo alichokiacha mama yake hataweza kukipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa jamii ielimishwe namna ya kurudisha imani na mapenzi kwanza kwa watoto yatima na pili kwa watoto wao wenyewe. Maana mtoto yatima anaweza akawa amefiwa baba na mama lakini yule mtoto bado anakuwa wa kwako kwa sababu damu ya ndugu yako lazima uilee. Hata hili tatizo watoto yatima wangepungua kama sisi wenyewe tungekuwa na imani ya kulea watoto wetu au watoto wa ndugu zetu, kaka zetu na dada zetu. Hilo lingetusaidia zaidi kuboresha jamii yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo napenda kuizungumzia ni mikopo ya akina mama. Wakati Mheshimiwa Waziri anatoa hotuba yake amenifurahisha sana, amesema katika mikakati yake iko mikakati ya kuelimisha wanawake jinsi ya kuendeleza biashara na mikopo yao mara wanapoipata. Namsifu Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa sababu wako akina mama wanaofanya biashara walipata matatizo nikampelekea Mheshimiwa Waziri na alipoona yamekuwa mazito sana alikaa na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuyazungumzia na akina mama wale wananishukuru na wamenituma nipitie Bunge hili, kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ushirikiano wao mzuri sana. Kilikuwa ni kikundi kimoja na walipata matatizo ya kudhulumiwa katika biashara zao, nawapongeza sana Mheshimiwa Dr. Rose Migoro na Mheshimiwa Khan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna matatizo ya kina mama wanaofanya biashara. Tatizo kubwa ni kutoelewa utaratibu wa kufanya biashara. Wanawake wengi ni watu wenye huruma, watu wenye kuamini haraka sana kwa hiyo hata tunapopeleka biashara zetu tunamwamini yule ambaye tunampelekea biashara lakini wale tunaowapelekea biashara zetu awe ni mwanamke au mwanaume hawana imani. Kuna mfano mmoja nitawatolea umetokea katika Wilaya ya Kiluvya. Akina mama wale wanapeleka biashara hawaweki mkataba na yule wanayempelekea biashara wanaambiwa njooni baada ya mwezi mmoja. Kila siku wanapeleka biashara, mwezi mmoja ukifika wanaambiwa ninyi hamkuleta biashara hapa, mna ushahidi gani? Kwa hiyo, akina mama wengi hawaelewi utaratibu huo, laiti kama wangeelimishwa jinsi ya kuweka mikataba wao na wale wanaowapelekea biashara ili ule mwezi ukifika wakifuata pesa zaoe akikataa mkataba ule unaweza kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo limetokea Kiluvya na bahati nzuri kuna Askari mmoja jina lake ni Lwambo, yuko kwa Tibaigana pale, niliwapeleka akina mama wale kwake na akamwita tajiri yule ambaye ni maarufu sana Dar es Salaam, ana hoteli zake na akina mama wale walikuwa wanapeleka kuku na mayai, lakini ilipofikia wakati wa malipo tajiri aliwakataa, akaenda kwa Mwanasheria na akaandika kabisa ili kupoteza ushahidi na akina mama wale wakawa wamezidiwa nguvu. Bahati nzuri kwa kutumia chombo cha dola, waliweza kuwasaidia akina mama wale ili kupata haki yao na kujiendeleza. Namshukuru sana Ndugu Lwambo, kwa kuwasaidia akina mama wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuongelea kuhusu michezo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika masuala ya michezo inachangia kwa asilimia kubwa na napenda kuwapongeza vijana wengi wanawake wanaojishughulisha na michezo ya *football.* Wako wanawake wengi wanaocheza michezo hiyo mfano Twiga, naamini hii Twiga hata siku moja ikicheza na Yanga tunaweza kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache kuhusu hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kuzungumza, napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, kijana wetu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migoro, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu wa Wizara, pamoja na watendaji wao wote kwa ujumla, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa hotuba hii. Kwa kweli hotuba hii iko wazi na imejieleza yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kuzipongeza kwa ujumla juhudi zinazofanywa na Wizara hii. Toka mwaka 2001, Wizara hii kwa kweli imejitahidi sana kusimamia masuala mbalimbali yanayohusu Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa inajulikana zamani, Wizara imebadilishwa jina na hivyo ule utaratibu wa kushughulika na maendeleo ya wanawake na watoto peke yake haupo tena, sasa hivi inajulikana kwa jina la Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kweli kishughuli zake imepanuka sana. Kwa maana hiyo basi, Wizara hii inatakiwa ijizatiti kwa ajili ya kusukuma maendeleo ya jinsia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kweli jina hili la jinsia linafanya kazi vizuri au hapana? Kama walivyosema wenzangu, inaelekea neno jinsia bado watu hawajaelewa maana yake, wanaelewa jinsia ni wanawake watupu lakini ni kweli kabisa kama tunavyofahamishwa na kama tulivyoelezwa kwamba, jinsia ni wanawake na wanaume. Wizara hii sasa inapaswa kushirikiana kwa karibu zaidi na Wizara nyingine kwa sababu hakuna Wizara inayoshughulikia eneo moja wanaume watupu au wanawake watupu zote kwa ujumla zinashughulikia jinsia kwa ujumla, ukienda Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Chakula, Maliasili na Utalii, zinashughulika na suala zima la jinsia. Kilichobaki sasa ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kushirikiana kwa karibu sana na Wizara nyingine ili kila Wizara ione kwamba, inawajibika kufanya kazi ya jinsia karibu na Wizara hii. Naomba suala hilo lieleweke na kufanyiwa kazi kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza zaidi katika suala zima la Vyuo ambavyo vinasimamiwa na Wizara hii. Kama ilivyoonekana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jitihada wanazofanya katika kuvikarabati, kuvisimamia na kwa kweli Vyuo hivi vimeanza kufanya kazi nzuri. Kazi nzuri inayofanywa na Vyuo hivi ni ile ya kutoa elimu ya stadi mbalimbali kwa vijana wetu wa kike na wa kiume na stadi wanazojifunza kule ni pamoja na useremala, ushonaji, uashi na nyingine nyingi. Vijana hawa wanapojifunza kule kwa kweli wanakuwa tayari wameshapata elimu ambayo inaweza kuwasaidia katika maisha yao. Waswahili wanasema: “Utaalam hauozi”. Kama mtu ameshajifunza useremala ni kweli kabisa atatumia ufundi ule kwa ajili ya kujitafutia mahitaji yake, hatakosa nyumba ya kujenga, hatakosa kiti cha kutengeneza, hatakosa kazi atakuwa na kazi za kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, tukiwaelimisha vijana wengi, wake kwa waume vile vile itatusaidia kupunguza suala zima la umaskini. Ninaomba Serikali ijitahidi kuviangalia Vyuo hivi na hata kuviongezea fedha kwa ajili ya kununua vifaa na zana mbalimbali ambazo zinaweza kutumika katika Vyuo hivyo kwa sababu wanaofaidika ni vijana wetu na hasa wale wanaotoka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko Dodoma na bahati nzuri sisi wa Dodoma tuna Vyuo viwili na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, Chuo kimoja cha Chisalu ambacho kiko Mpwapwa, wamekiingiza katika utaratibu wa kukikarabati. Kwa kweli naipongeza sana Wizara kwa kazi hiyo waliyoifanya. Naamini Chuo kile kikikarabatiwa kinaweza kufanya kazi nzuri ya kuelimisha vijana wetu wanaotoka katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Chuo kile yapo mapungufu mojawapo ni tatizo la watumishi ambao ni wachache sana hawatoshelezi na vile vile hata idadi ya vijana wanaokwenda katika Chuo kile ni ndogo sana. Naiomba Wizara isaidie kuweka utaratibu ambao utawezesha kuongeza idadi ya Walimu na vijana wanaokwenda kuchukua mafunzo katika Chuo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunacho Chuo cha Munguri ambacho kiko Kondoa. Kwa kupitia Halmashauri tunashukuru Chuo kile kilipata msaada wa kuchimbiwa kisima cha maji na wafadhili wa *DSF* lakini kiko pale pale na kimefungiwa bomba pale pale. Kwa hiyo, wanakijiji wanaozunguka Chuo kile, watumishi wa Chuo na wanafunzi wanaokwenda kuchukua mafunzo pale wanachota maji katika maeneo yale. Sasa hizo ni jitihada za Halmashauri ya Kondoa pamoja na wafadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ichukue jukumu la kusambaza maji yale katika kijiji kile na vile vile yaingizwe Chuoni ili kuwarahisishia Wanachuo hawa kazi ya kuchota maji ili waweze kufanya kazi nyingine zaidi za mafunzo kuliko kuyaacha maji pale yalipo. Kwa hiyo, tunaomba Chuo kisambaziwe maji. Vile vile Chuo hiki kilishafanyiwa ukarabati na bahati nzuri kuna chumba kimoja tu ambacho kimebaki, basi tunaomba Wizara isaidie kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa chumba kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumzie suala la Walimu wa Vyuo hivi. Kwa ujumla ni kwamba, inaonekana hawajapatiwa mafunzo muda mrefu. Naiomba Serikali iwawezeshe Walimu hawa kupata taaluma mpya na kwa kweli wakielimika ni rahisi kuwaelimisha vijana wanaoenda katika Chuo kile. Pia Chuo kile kina upungufu wa watumishi na chenyewe kinahitaji kuongezewa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa utaratibu na maandalizi mapya wanayofanya kwa kuandaa sera hii ya watoto. Kwa hiyo, naiomba Serikali iharakishe sera hii ili iweze kuwasaidia watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Mama Anna Mkapa, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia shughuli za Maonyesho ya Saba Saba kwa upande wa akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao wanatoka katika Mikoa na Wilaya kupeleka vifaa vya Maonyesho mara nyingi husimamiwa na Halmashauri. Unakuta baadhi ya Wilaya na Mikoa mingine akina mama hawa wanashindwa kwenda kwa sababu uwezo wa kujisafirisha na kupeleka vifaa vile katika Maonyesho ya Saba Saba unakosekana kwa hiyo wakati mwingine wanashindwa kushirikiana. Naomba Wizara iwahimize na iwaelimishe viongozi wa Halmashauri zote walione na walijue tatizo hilo ili kuwezesha Mikoa yote na Wilaya zote kushiriki katika Maonyesho ya Saba Saba hasa kwa akina mama wanaopeleka vifaa na ni vizuri vifaa hivi vikaonekana kwa sababu hakuna Mkoa ambao akina mama hawajishughulishi kutengeneza vifaa mbalimbali. Ni kazi za mikono ambazo wanazifanya kila siku na kwa kweli kazi hizo ndizo zinazowafanya akina mama angalau wapate chochote kwa ajili ya kujikimu katika maisha yao. Wanapopeleka kule kwa kweli bei wanayoipata ni nzuri zaidi kuliko wakiviuza katika maeneo yetu ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuiomba Wizara baada ya jitihada nzuri waliyoifanya ya kukarabati Vyuo, maeneo haya yote itueleze je, baada ya kazi hii ina mpango gani kwa ajili ya kuendeleza taaluma ya wale ambao wanaenda kujifunza pale ili tujue malengo ya Wizara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iiongezee fedha Wizara hii kwa sababu fedha inazopata ni kidogo sana kwa sababu kazi inayofanya ya kuelimisha wananchi vijijini ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nikupongeze sana sana kwa namna ulivyofanikisha shughuli ya Wabunge Wanawake siku ya Jumamosi. Kweli kitendo kile kimeonyesha umahiri wako na Wabunge wote Wanawake namna mlivyofanikisha shughuli ile. Ni mategemeo yetu kwamba, mtaendelea kufanya tena na tena na tena, ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Shamim P. Khan, Katibu Mkuu wa Wizara, pamoja na wataalam wote, kwa hotuba nzuri na sio hotuba tu pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimpongeze sana sana Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii, ukweli Mheshimiwa Simba, ana kila sababu ya kupongezwa kwa sababu anailea Kamati yake vema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii, kwanza nataka kuzungumzia suala la biashara ndogo ndogo za akina mama. Nia ya Serikali ni kuondoa umaskini na umaskini hauwezi kuondoka kwa wale ambao wanatarajiwa kuondoa umaskini kila siku wanakuwa ndani ya mateso, kuadhibiwa na kunyang'anywa bidhaa zao. Kina mama pamoja na vijana wanateseka sana hasa katika miji yetu mikubwa wanapoendelea kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitatoa mfano, tarehe 22 Julai, 2003 saa moja za usiku, katika eneo la Ubungo Dar es Salaam, Mheshimiwa mimi mwenyewe binafsi, nimeshuhudia, nimesikitika na machozi yamenitoka, namna askari wa Jiji walivyokuwa wakiwaadhibu akina mama na vijana ambao walikuwa wamejipanga pembeni mwa barabara wakiuza biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshuhudia si mwanamke mmoja wala wawili, inafika wanne, wanakimbia marungu wameanguka chali barabarani, wanakoswa koswa kupondwa na magari. Sasa hivi ni kweli wakati hapa tunanadi sera zetu kila siku tuondoe umaskini. Kama wamekaa mahali ambapo labda Halmashauri ya Jiji haipendi, kuna tatizo gani maeneo yale mkayatenga, mkawajengea, mkawakodisha ili akina mama na vijana walipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakemea sana na ukweli ni udhalilishaji mkubwa sana unaofanywa na askari wa Jiji kama vile wanaifunga Serikali kamba mbili, moja nyuma na moja mbele, mmoja anavuta nyuma na mmoja anavuta mbele. Ukweli hatuendi namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sitaki kuchangia, nimechangia kwa suala hilo nililoliona kwa macho yangu basi naomba sana Mheshimiwa wa Tawala za Mikoa, ajaribu kuzungumza nao hawa askari wa Halmashauri kama kweli utaratibu wa kazi ndiyo ule. Mama ameshapika vitumbua vyake au ubwabwa wake anakimbia na sufuria lake anaanguka, je, kama ubwabwa ule ni wa moto ukimwunguza makosa ni ya nani? Ni ya Serikali kwa sababu askari wa Jiji ni Serikali na kama wale wanafanya, wanafanya kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo, ni lazima tuwakemee kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali ambapo nimeona mfano mzuri kabisa ni Manispaa ya Ilala. Kamati yetu ilikwenda kutembelea baadhi ya mama lishe wa maeneo mengi. Katika eneo ambalo tumependezewa sana sisi kama Kamati na ni lazima niseme kwamba, Halmashauri nyingine ukitoa Halmashauri ya Ilala, tujaribu na sisi kuiga. Wamewajengea vibanda sehemu ya mnazi mmoja, pale akina mama wakawawekea, viti, meza nzuri, safi kabisa, wanawatoza pesa ingawa pesa wanazotozwa, ukweli ni nyingi sana lakini angalau wamefanya chanzo kizuri. Sasa kwa nini Serikali kwa ujumla au Halmashauri zetu zote haziigi mfano huu zikawatengea kuliko kuwachukua watu kwenda kuwa-*dump* mahali ambapo ukodi teksi kwenda kununua fulana ya mtumba ya shilingi mia tano. Haivumiliki hii. Sasa mimi nasema hivyo, waige Halmashauri ya Ilala na kama wanataka kwenda kusoma waende pale wakasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ningeomba kwa kupitia kwako, nimwambie Mheshimiwa Waziri, azungumze na Halmashauri ya Ilala wawapunguzie kodi. Akina mama pale wanauza ubwabwa na maharage, wanatozwa shilingi 15,000/= kwa mwezi. Fedha hizi ni nyingi, angalau ingekuwa shilingi 5,000/= au ikizidi ingekuwa shilingi 7,000/=. Shilingi 15,000/=, unakodi mlango wa duka zima sio mahali *open* kama pale. Kwa hilo nadhani taarifa imefika na *Inshallah,* Mheshimiwa Waziri, atatimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba nizungumzie kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ambayo yametajwa na Mheshimiwa Sophia Simba na mimi napongeza vile vile jina la Wizara

limeshatekelezwa. Lakini moja ambalo nilikuwa nisilizungumze, nitalizungumza kwa sababu nilisikia limetajwa hapa asubuhi kama vile Wizara haijafanya chochote kuhusu maandalizi ya Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi na wengine ni mashahidi zaidi kwa sababu tunaona juhudi za Wizara namna ilivyokuwa imeajiri wataalam kushughulikia maandalizi ya hii Benki ya Wanawake. Ushahidi ni kwamba, wiki iliyopita tarehe 21 na 22 wataalam hao walikuwepo Kibaha katika kupitia tena rasimu zao za awali za uanzishaji wa Benki ya Wanawake na walishirikisha Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa yote ya Tanzania hii. Sasa tukisema kwamba, Wizara au Serikali haiko *serious* mimi nasema si kweli wanafanya kazi zao na huwezi ukaibuka. Nadhani hata ndege inapotaka kuruka haikai pale pale ikaruka kama inavyoruka helikopta moja kwa moja inakwenda juu, ndege kwanza inakwenda taratibu, inakwenda kwenye *run way*, inapinda, inakwenda tena *speed* kuchochea moto, mpaka pale inapofikia *stage* ya kuruka, ndiyo inaruka angani. Sasa na benki hii kwa hatua iliyofikia, itakuwa tayari katika kipindi cha miaka miwili au mitatu ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kuzungumzia suala la ukeketaji. Suala la ukeketaji mimi nalisema kwa uchache sana. Ni suala ambalo bado ingawa wananchi wetu au baadhi ya mikoa wanajaribu kuliacha taratibu lakini naomba nitoe rai kwa kupitia kwako, mimi nadhani sisi wanaume tukitaka ukeketaji ukomeshwe basi utakoma bila hata kumtia hatiani mtu yeyote. Tuweke kuanzia leo hapa wanaume wote wasimkubali msichana yeyote ama kumuoa au kuwa naye kwa njia yeyote ile, msichana yeyote aliyekuwa amekeketwa. Wakigundua haya basi nakuhakikishia hakuna msichana yeyote atakayekeketwa katika nchi hii kwa sababu watakuwa hawatakiwi. Lakini sasa sisi wenyewe tunayapenda yale sasa itakuwaje, watafanya zaidi kuliko vile. Mimi naomba akina baba tuwasaidie akina mama kuhusu kusimamia suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaeleza lile nililolikusudia, nasema tusigeuke Ngariba wa Bopwe. Kule Pemba Wete, kuna Mtaa mmoja unaitwa Bopwe. Kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar, alikuwepo Ngariba mmoja jina lake Bahamad, Muislam huyo, yeye alikuwa kazi yake kutahiri wanaume, hodari sana, watu wote wanasafiri kwenda kwake, kila mtoto wa kiume akizaliwa anapelekewa yeye anamtahiri. Sasa alipofariki, desturi zetu lazima akaoshwe, kwenda kuoshwa wakamkuta ana govi yule yaani hakutahiriwa. Yule Bahamadi hajatahiriwa. Watu wakasema huyu ameshatahiri watu lukuki, lukuki maana yake laki moja na yeye mwenyewe hajatahiriwa. Sasa na mimi nasema hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, asiwe na yeye Ngariba wa Bopwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, tutapiga kelele sisi na yeye kwamba mambo ya jinsia haya tumwendeleze mwanamke, tumpe elimu mwanamke na mimi napiga kelele hizo hizo na mwaka 2002 nilisema, basi hata Mawaziri wanashindwa kuajiri madreva wanawake. Hata yeye Mheshimiwa Waziri, mimi nilidhani atatuonyesha mfano. Mimi mwaka 2002 nilipotoa hotuba ile, sasa hivi nina madreva wawili Zanzibar wote wanawake. Sasa kwa kuanzia ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri, mwakani atakapokuja hapa kutueleza angalau awe na dreva mwanamke, madreva wazuri sana bwana na aende Shabiby akamuone Ndugu Jane, Ndugu Jane akikamata ungo, utaona labda kama upo ndani ya ndege unaruka kwa raha. Mwanamke lakini mwanamke jasiri, anajua namna ya kazi yake. Sasa Mheshimiwa Waziri, hamwamini mwanamke mwenzake kumwendesha, haoni tabu kuendeshwa na mwanaume! Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na jirani yake Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba hapo anapokaa amshawishi, kwa sababu nilizungumza naye akasema yeye yuko tayari lakini anasubiri Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aanze. Hilo nadhani limefika na litatekelezwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Tunaomba sana Serikali iongeze fungu katika Vyuo hivi, tulitembelea hivi karibuni tulipofika Chuo cha Kisarawe, tulisikitishwa sana kuona hali mbaya ya mabweni, sakafu zimepasuka zote, maji hawana, matatizo matupu na *fund* hawana. Basi ningeshauri tu mimi kama alivyozungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wangu kwamba, yale maduhuli wanayoyapata waachiwe angalau asilimia ndogo ili waweze kutumia. Lakini vile vile na wao wenyewe Wakuu wa Vyuo wawe wabunifu. Naomba Mheshimiwa Waziri, akaonane na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ili wawasiliane na Wakuu wa *VETA* kwa sababu Vyuo vya *VETA* vimeendelea sana.

Hakuna tofauti baina ya *TCC* na Vyuo vya *VETA*. Lakini tofauti iko kati ya mbingu na ardhi, kama kutoa maksi Vyuo vya *VETA* naweza kutoa 99.9% na kule nikatoa 20% *only*. Sasa bora Mawaziri wawili, wakae na Wakuu wao wa Vyuo, wawaelimishe wale Wakuu wa Vyuo namna ya ubunifu walioufanya wenzao. Natarajia hilo litaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu gonjwa la UKIMWI. Gonjwa la UKIMWI litazidi kuenea kutokana na tamaa zetu sisi wanaume. Mtu hatosheki maisha, maisha huthamini chako, tutakwenda wapi? Dini zetu zinatukataza zote, hakuna dini hata moja hata ile ya Makadiani wanakataza kuzini. Lakini sisi tunaingia katika zinaa tu moja kwa moja. Ukitosheka na chako mimi sidhani kama utataka kingine zaidi wala sifikirii kama kuna mtu amefariki kwa kutosheka na kile ambacho amekimiliki nyumbani kwake. Hakuna kaburi ambalo umeambiwa huyu amefariki kwa sababu ya kukaa na mkewe tu. Kwa nini? Unataka wali utimie ongeza ongeza zana zake, nyama nyingi, mbatata, hiliki, kidogo hiki na kidogo hiki, unukie nukie ule wali na mchele wa Kyela ule wa tule na bwana uwepo pale. Ukitimiza yale hutaki tena kwenda kula kwa mama lishe, utatosheka na ule ubwabwa anaopika mkeo. Lakini kwa sababu nyumba ya pili au kule ambako unakoiba ndiyo unatimiza zana zote, lazima utasifu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda wapi sisi? Tunazungumzia suala la UKIMWI, pesa zinatengwa kila siku, tunapiga kelele, semina haziishi lakini kwa sababu ni kwamba hatujawa *serious.* Hatuna kinaa ya moyo. Lazima binadamu uwe na kinaa ya moyo wako na utosheke na kile kidogo ulichokipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la UKIMWI, Kamati yetu tulipokwenda, inasikitisha kukuta walioathirika, walioachwa bila mama na baba, waliokimbiwa na wazee wao baada ya kupata UKIMWI, waliokimbiwa na baadhi ya ndugu wa karibu baada ya kupata UKIMWI. Ni jambo ambalo lazima tukae pamoja tuelimishane na tuambizane kwamba, suala la UKIMWI litaondoka pindi pale ambapo sote tutaamini kwamba, kila mmoja awe na mkewe na wala sisemi awe na mwanamke, awe na mkewe, aliyekuwa hana aoe. Hii ndiyo *solution* zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, lakini nasema Mheshimiwa Waziri agizo langu nililotoa alitekeleze. Ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu juu ya hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambayo ndiyo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niungane na Mheshimiwa Haroub, kukupongeza wewe kipekee kwa jinsi ulivyofanikisha harambee iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge Wanawake siku ya Jumamosi. Kweli inaonyesha ni jinsi gani ulivyo mbunifu na ambavyo unaweza kuwafanya akina mama wawe na mshikamano na kuwa na mfuko wao kwa ajili ya maendeleo ya wanawake na watoto huko Vijijini tutokako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, dada yangu Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro na Naibu wake, Mheshimiwa Shamim Khan. Kwa kweli siku ya Jumamosi wametuonyesha mfano wa kuigwa. Wamekuwa na mshikamano wa hali ya juu. Imeonyesha hata katika utendaji wao wa kazi ndivyo walivyo. Wameingia kwa pamoja na sare zao naamini kabisa hata Wizara zingine, Mawaziri watakuwa wamejifunza lolote pale. Hata mimi mwenyewe nimejifunza na kwa kweli nimefarijika sana. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu, watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii. Kwa kweli Bajeti hii ni nzuri sana hata tungeweza kusema ipite bila kujadili. Ninaamini Bajeti hii itapita kama ilivyopita Bajeti ya Mheshimiwa Cheyo, kwa sababu ipo wazi, imejieleza lakini tunasimama tu kwa ajili ya kutoa changamoto katika maeneo kadhaa ili kuhamasisha yaboreshwe zaidi kuliko hapo yalipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nichukue nafasi hii sasa kuchangia hoja iliyo mbele yetu, nikianza na Maafisa Maendeleo ya Jamii. Ni kweli Wizara hii ndiyo Wizara ambayo inawasimamia Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kwa bahati mbaya sana Wizara hii ina Maafisa Maendeleo ya Jamii mwisho ngazi ya Mkoa, kitu ambacho hakiunganishi watendaji hawa na walengwa. Halmashauri zetu za Wilaya zina Maafisa wa Maendeleo wa Jamii, lakini Maafisa hao wapo chini ya TAMISEMI. Hivi kama nyumba mwenye nyumba ni Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, huyu mwingine anaingiaje kulea watoto wa mtu mwingine wakati mzazi wao yupo! Mimi naamini kabisa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wangekuwa na mlezi mmoja, wangekuwa ndani ya Wizara moja, Waziri akatoa maelekezo yake kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri na tukawaongezea na watendaji wengine ngazi ya Kata, naamini ufanisi wa kazi kwenye Wizara hii katika kuwawezesha akina mama kuondokana na umaskini ungekuwa wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi sera ya wanawake inaongozwa na Wizara hii lakini wanaosimamia ni watendaji ambao wapo chini ya TAMISEMI. Sasa hata tukisema kwamba, hawa wanahitaji elimu, taaluma, wapate semina na kadhalika, atakayewajibika ni nani? Mimi naamini kabisa kuna haja na kila sababu kwa Serikali kuona umuhimu wa kuunganisha watendaji hawa kuwe na mtiririko mzuri kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri na vile vile wawepo Watendaji ngazi ya Kata. Wanawake wapo huko Vijijini, huyu Afisa Maendeleo wa Wilaya atazunguka kwa muda gani mpaka amalize Vijiji vyote hata kuona vikundi vyote. Ndiyo maana akina mama wetu wanakuwa hawana taaluma kwa sababu hawana mtu wa kuwaelimisha ama kuwahamasisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali itakuwa imesikia na itaona umuhimu wa kuongeza Watendaji, yaani Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa ngazi ya Kata. Ni muhimu sana katika kuwasaidia akina mama hasa hawa wanaojitahidi kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo sasa naomba niongelee suala la mafunzo kwa hawa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Ni kweli Maafisa hawa elimu wanapata lakini bado haitoshi na siyo kutotosha tu, hawajapata wote. Hii inatokana na Bajeti anayopewa Mheshimiwa Waziri huyu ni ndogo. Naiomba Serikali ione umuhimu wa Wizara hii, Wizara hii ndiyo Wizara Mama. Mama ndiye mwenye majukumu makubwa ndani ya familia kuhakikisha familia imekula, imeshiba, imevaa na pia ukimkomboa mwanamke umekomboa familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafisa wetu hawana taaluma, hawana hata mbinu za kisasa za kumsaidia mwanamke ama vikundi ili viweze kuwa na ubunifu wa kwenda na mambo ya kisasa katika uendeshaji wa miradi yao ama biashara zao. Nina hakika kabisa elimu hii ikitolewa kwa Maafisa Maendeleo wa Jamii, watakuwa na changamoto kubwa katika kusimamia vikundi vya akina mama na kuendesha mambo yote kwa ajili ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea hilo, sasa labda niongelee kuhusu huu Mfuko wa kuwasaidia akina mama. Naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kutoa kwa kila Halmashauri kusaidia Mifuko ya akina mama kwa ajili ya kuwakopesha ili kuendesha miradi yao. Naipongeza sana Wizara hii kwa sababu kila mara inajitahidi kutoa fedha, mwaka 2002 kama sikosei kila Halmashauri ilipata shilingi milioni nne, hata mwaka huu ninaamini imeshatoa shilingi milioni nne kwa kila Halmashauri na kama zipo ambazo hazijapata basi ni wao tu kwenda kuchukua. Waziri atakuwa amefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa sana. Sasa hivi pamoja na kwamba, Wizara hii inajitahidi kutoa lakini ni ndogo, shilingi milioni nne katika Halmashauri zetu ni ndogo mno kwa sababu hata Halmashauri ile asilimia kumi waliyopangiwa kutoa hawatoi. Sasa ni afadhali jahazi hili likabebwa moja kwa moja na Wizara hii, wakaongeza fungu, likawa kubwa ili akina mama waweze kunufaika na mikopo hii. Inawezekana pia hata hizi ambazo zinatolewa kuna tabu ya urejeshaji wa mikopo. Akina mama wanaokopeshwa hawarudishi mikopo. Hivi mnadhani kwa nini hawarudishi? Akina mama hawarudishi kwa sababu hawana taaluma za uendeshaji miradi yao. Wanaendesha miradi yao kwa tabia ya kubahatisha. Hawaelewi wafanye nini, wajizatiti vipi katika kuboresha miradi yao na hawaelewi wazalishe vipi.

Ndugu zangu kuna haja kubwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii sasa kuona umuhimu wa kutoa elimu hii kwa akina mama ili waweze kurejesha mikopo. Mikopo hii isiporejeshwa haitawezekana tena Waziri wetu kuweza kuendelea kutoa mikopo katika Halmashauri zetu kwa sababu hela zitakuwa zinakwenda zinazama moja kwa moja. Lakini kama zitarejeshwa zitamsaidia sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Wizara yake kwa ujumla, kuweza kuuendeleza huu Mfuko na kuweza kuboresha mikopo hii kwa akina mama kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa hivi niongelee kuhusu soko la bidhaa za akina mama. Ni kweli akina mama wanajitahidi sana katika kuondokana na umaskini. Wanajitahidi kabisa kabisa kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa mfano, Mkoa wa Singida wanatengeneza Visonzo yaani mapambo, wanasuka vitu vingi tu kama mikeka, vikapu, siyo hayo tu vile vile akina mama wa Mkoa wa Singida, hata kwenye uchimbaji wa madini wamo, vikundi vya akina mama vina migodi hata ya madini na wanachimba. Hata kupika chumvi, akina mama wa Mkoa wa Singida wanapika chumvi, lakini akina mama hawa soko la kupeleka bidhaa zao hawana. Hivi ninavyoongea Singida wametengeneza Visonzo vingi na vizuri ajabu lakini hawana pa kupeleka. Wana vikapu pale Kikuyu kwa Mheshimiwa Chiligati vingi na mikeka lakini pa kupeleka hawana. Hivi kama akina mama hatutawasaidia wapeleke wapi biashara zao tutakuwa tumewakomboa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kuna haja ya Wizara mbalimbali kushirikiana na Wizara hii katika kuwasaidia akina mama. Kuna Wizara ya Viwanda na Biashara, wanatakiwa wawajibike, kuna Wizara ya Ushirika na Masoko nao wawajibike. Vile vile kuna Wizara na Madini na Nishati na wenyewe vile vile wawasaidie hawa wachimba madini hawana hata vifaa. Kama Wizara hizi mbalimbali zitashirikiana kwa pamoja katika kumkwamua mwanamke na atakuwa amewezeshwa kuondokana na umaskini kuliko ilivyo sasa hivi wanatengeneza bidhaa mbalimbali lakini hawana pa kupeleka. Mimi sasa hivi nikiwa kama Mbunge wao hata kufanya ziara sasa ninaanza kupata wasiwasi, kila ninapopita nakuta bidhaa mbalimbali, hivi mimi kama Mbunge wao nitanunua nitazimaliza? Naulizwa sasa Mheshimiwa tuzipeleke wapi? Jibu sina, kwa hiyo, naiomba Serikali inisaidie, Wanawake wa Mkoa wa Singida, kwa kweli wapo mstari wa mbele katika kuondokana na umaskini na wana bidhaa mbalimbali ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi wa soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi labda nipongeze *NGOs* za Mkoa wa Singida ambazo zinajitahidi kuwakopesha akina mama. Kuna *PRIDE, WEGCC, SEMA* na *NGOs* zingine mbalimbali ambazo zinasaidia kukopesha akina mama na siyo *NGOs* tu hata mabenki. Yapo mabenki ambayo sasa hivi yanasaidia kama vile Benki ya Posta na *NMB.* Kwa kweli zinawasaidia sana kuwakopesha akina mama na ndiyo maana wamefikia hatua hata ya kuwa na bidhaa nyingi ambazo zinakosa soko kwa sababu ya mikopo wanayoipata. Sasa kwa nini *NGOs* hizi zinafaulu kurudishiwa mikopo? Zinafaulu kurudishiwa mikopo kwa sababu zenyewe zinatoa elimu, lakini sisi tunakopesha kiholela holela. Tuige mifano ya *NGOs* jinsi zinavyotoa elimu na jinsi zinavyofaulu kwa akina mama kurudisha mikopo. Tukiiga hawa wenzetu wanavyofanya, nina hakika hata mikopo ya Serikali itarudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie suala zima la uzalishaji mali kwa akina mama. Akina mama wanajitahidi mno kuzalisha mali. Wanafanya kila aina ya juhudi lakini kama ninavyosema, hawana mtu wa kuwasukuma. Ninafanya ziara Mbunge, natembea na Afisa Maendeleo wa Jamii hata ukimpa uwanja huu hapa hebu ndugu yangu toa angalau mwanga kidogo kwa akina mama namna ya kujizatiti, kuunda miradi yao na nini, lakini unakuta mtu hata kulitawala jukwaa tu anashindwa, hata namna ya kujieleza anashindwa kwa sababu hizo taaluma zao ni ndogo. Siyo hivyo tu inawezekana hata vitendea kazi hawana, hawana hata usafiri, kwa hiyo, anasubiri mpaka Mbunge aanze ziara ndiyo aongozane naye lakini kumbe angewezeshwa akapewa hata usafiri, taaluma hii ingeweza kutolewa wakati wowote hata bila kusubiri ziara ya Mbunge. Naomba Wizara itilie maanani sana kuwaweka katika mazingira mazuri hawa Maafisa Maendeleo wa Jamii, ili waweze kutoa elimu kwa hawa akina mama wanaojitahidi kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara kwa kuwa ina mpango mzuri wa kuunda Bodi. Bodi zote za Vyuo vya Maendeleo zina Wajumbe kutoka maeneo Vyuo vilipo, siyo sawa na Wizara zingine zinachukua watu wa Bodi kutoka katika maeneo yasiyojulikana. Lakini hawa wenzetu wana mpango mzuri sana. Siyo hivyo tu, nawapongeza kwa sababu tayari walishaanza ukarabati wa Vyuo hivi

toka mwaka 2002. Singida tuna Vyuo viwili, Chuo cha Maendeleo ya Msingi na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida, ambapo Chuo cha Maendeleo ya Msingi kimeshafanyiwa ukarabati mwaka 2002, kimemalizika na cha Singida Mjini pale tayari kipo kwenye ukarabati na ninaamini mpaka Desemba ukarabati huu utakuwa umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kukarabati Vyuo siyo mwisho, Vyuo hivi pia havina vitendea kazi. Vyuo vya Singida vina masomo ya useremala, masomo ya ufundi uashi, ufundi chuma, ufundi umeme, lakini vifaa hakuna. Hivi Serikali hii ina matabaka? Mbona Vyuo vya *VETA* vina vifaa? Au ndiyo huu unyanyasaji wa kijinsia hata kwenye Wizara upo? Kwa kuwa Wizara inaongozwa na wanawake, basi inakuwa ndiyo hivyo tena. Ukienda Chuo cha *VETA* hapa vifaa vingi, nenda Morogoro hapo *VETA* vifaa kemkem, nenda Dar es Salaam na Mwanza huko hivyo hivyo. Lakini ndani ya Vyuo vya Maendeleo vifaa havitoshi au hakuna. Sasa hivi tayari wakufunzi wetu wameshachukua kozi ya kompyuta, ninaomba Serikali itoe msaada wa kompyuta ili walimu waendane na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu juu ya hoja iliyoko mbele yetu. Mimi nitachangia maeneo mawili, suala la UKIMWI, madhali Mheshimiwa Waziri amelitamka na Idara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la UKIMWI, katika ziara zangu siku moja niliielimisha jamii kwenye mkutano wa hadhara juu ya hili. Nikafika kwenye suala la kondomu. Kijana mmoja akasimama akasema Mheshimiwa Mbunge, ukitaka tukueleze ilivyo kwa nini hatutaki kutumia kondomu, fanya mkutano wa vijana peke yake, tukupe maneno. Mimi nikasema nalala hapa hapa leo katika hili.

Nikakutana nao vijana usiku, nikasema nipeni maneno, wakaniambia nenda ukamwambie Waziri wa Maendeleo ya Jamii, mbinu yake tumeijua. Nikasema hebu niambieni mbinu ipi? Akasema anapendelea sana akina mama katika kondomu, lakini ni wao wanaosema siyo mimi, mtaniwia radhi.

Mwanamume akivaa kondomu kuna sehemu inayobakia kwenye ncha ya kumwagikia maji ya mwanamume, asilimia 100 hayamgusi mwanamke, wao ndiyo wanavyosema hivyo. Lakini wanaume kwa asilimia kubwa tu hupata maji ya mwanamke kwenye kitovu na kwenye mapanja, sasa akiwa na vipelepele basi kwa vyovyote hawezi kukwepa. Sasa wameshaona upumbavu kwamba, wanakingwa wachache, sasa wameamua kutotumia kondomu kama ni kwenda waende wote tu. *(Kicheko)*

Sasa nikamwuliza wewe unasemaje katika hili, wafanyeje? Akasema kamwambie Mheshimiwa Waziri, atengeneze kitu kama chupi hivi, yaani ile kondomu ukiivaa ianzie kwenye kitovu mpaka kwenye mapaja hata yale maji yakimwagikaje hayatamgusa mume popote, hapo tutaelewa. Lakini katika hili wala hatutaki kuwakinga wanawake peke yao, sisi hatuwezi kuendelea na upambavu huo tumeamua kutoa kondomu na kutupa huko twende tu wote. Kamwambie sisi hatutaki. Nikamwuliza kumwambia tu, kama ni kusema tu madhari sichinjwi mle na nina haki ya kusema nitalisema hili. Mheshimiwa Waziri, umesikia kondomu inawa-*favor* wanawake kwa asilimia kubwa sana kuliko wanaume, ndiyo maana vijana siku hizi hawataki kuzitumia kondomu wanazitoa waende wote tu. Ujumbe huo umefika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mimi ninadhani wakubwa hawaelewi barabara hii Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa mawazo yangu mimi. Sina hakika kama Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Katibu Mkuu wake, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa, wanaelewa barabara *Court Community Development* na ndiyo maana kwenye Halmashauri zingine zimeunganishwa kuwa Maendeleo ya Jamii, Ushirika sijui na Masoko, sehemu zingine Maendeleo ya Jamii, Kilimo sijui na nini, yaani hawazielewi kazi zake, umuhimu wake hasa kwa nchi maskini kama Tanzania. Idara ya Maendeleo ya Jamii, ilitakiwa iwe pekee yake na ukikosea sana basi ishirikishwe na Mipango iwe Idara ya Mipango na Maendeleo ya Jamii hapo ndipo umekosea sana. Kwa sababu Idara ya Mipango huhusika na Idara zote, Mipango hupangwa katika Idara zote, Mipango ya Kilimo, Mipango ya Mifugo, hivyo vyote ni Idara ya Mipango.

Lakini inavyotakiwa badala ya Mipango kupangwa na Idara inayohusika, wapelekewe watu wa Maendeleo ya Jamii kabla hawajapeleka kwa wananchi. Watu wa Maendeleo ya Jamii ndiyo watakaosema Mpango huu katika jamii fulani hupelekwa kwa mtindo fulani ndipo utakapofanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana si lazima *approach* itakayopeleka mradi wako wa kilimo au mifugo katika jamii "A" si lazima iwe sawasawa na *approach* itakayopeleka mpango huo kwenye jamii "B". Kwa utofauti wa mila na desturi na mambo mengine. Watu wa Maendeleo ya Jamii ndiyo wanaotoa jibu kwamba, muda wa kupeleka jambo hili katika jamii fulani ni muda fulani. Ama tukitaka tufanikiwe ni lazima vijana wakubali kwanza kwa sababu jamii hiyo ndivyo ilivyo au tukitaka tufanikiwe wakubali wazee kwanza na ndivyo ilivyo pale au tukitaka tufanikiwe asiende mtoto wa kike kutoa elimu pale, kwa sababu walivyo wale lolote akisema mwanamke hawalijali. Nyie mnapeleka shambani mwanamke, wakati jamii ile mwanamke akisema chochote hawaelewi hata likiwa la maana ndivyo walivyo wale. Au katika jamii ile mtoto mdogo kuliko wale pale akisema chochote hata kama ni cha maana hawaelewi. Nyie mnampeleka bwana shamba kijana, katika jamii ile mila na desturi yao hawaelewi akisema kijana. Au mnafanya Mkutano shuleni, kumbe mila ya jamii ile mkiwapeleka tena shuleni alikofeli wakati anasoma pale haelewi.

Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, ndiyo watatoa majibu hayo. Ila mimi naona ajabu Idara ya Maendeleo ya Jamii haipo katika Idara nyeti, mimi sielewi, nawaombeni Wizara iimarisheni Idara ya Maendeleo ya Jamii. Kuna kijiji kimoja bwana maji aende kuhamasisha wananchi kuchimba bwawa pale, alipokwenda bwana afya akatoa amri lifukiwe lile bwawa kwa sababu litaleta mbu. Lakini wote ni watu wa Wilayani huko huko, walikosa *coordination.* Idara ya Maendeleo ya Jamii *as a coordinator* wangeweza ku-*coordinate* mipango hii miwili yote ikafanikiwa. Mtu wa Maendeleo ya Jamii yeye ni mtafiti anakwenda kufanya utafiti wa mpango ule jinsi gani unaweza uka-*fit* pale. Kuna Mheshimiwa Waziri Mkuu mmoja, alituletea ng'ombe Mtwara, alitaka tuwe na maendeleo katika mifugo, unaona matatizo hayo. Sisi tukamwuliza Wasukuma wa kuchunga ng'ombe wako wapi, kwa vile hatukumuelewa tukawachinja ng'ombe wote. Hakutakiwa kutuletea ng'ombe, ilitakiwa mtu wa Maendeleo ya Jamii kumweleza mpango huu, akafanya *research* kulingana na mila na desturi zetu.

Halafu watu wakaja kutu-*inject idea,* sisi wenyewe baada ya kuelewa na kuhamasika tukaenda kununua ng'ombe siyo kutuletea ng'ombe. Wewe tu-*approach* kiasi ambacho tukuelewe, sisi wenyewe tukiuza korosho tukanune ndama. Sasa jinsi ya kubadilisha watu mawazo kuna *approach* zake. Ukizikosea unaweza ukafanikiwa kijiji fulani na kijiji kingine usifanikiwe. Sasa watu wa Maendeleo ya Jamii wana maabara ya ku-*test high process* ya jambo fulani, sehemu gani limeingia, muda gani na lina-*fit* vipi, haiwezekani au linawezekana tunafanyaje watu wa Maendeleo ya Jamii. Ndipo jamii itaisaidia Serikali hii maskini kuchangia kwa kiwango kikubwa sana katika shughuli za maendeleo ya jamii. Vinginevyo Serikali itatumia fedha nyingi sana wakati hatuwezi kupata maendeleo ya jamii kwa sababu *participation* ya watu ni ndogo sana. Kama kunatakiwa raslimali ya asilimia 100, basi ukitumia *approach* nzuri, *participation* ya watu inaweza ikawa asilimia 75 na asilimia 25 ikawa fedha kutoka Serikalini, madhali tuna fedha kidogo ikatosha. Ukienda kichwa kichwa basi itatakiwa raslimali ya Serikali kiasi cha asilimia 90, kwa sababu *participation* ya watu itakuwa asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Jamii iimarisheni na wapeni vitendea kazi. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wawe katika kila Kata na wapatiwe usafiri kwa sababu inabidi wazoeleke wataalam wa Maendeleo ya Jamii kwa kila kijiji, yaani waonekane mara kwa mara kwenye pombe, kwenye migahawa, kwenye harusi ili jamii iwaone kwamba hawa ni miongoni mwetu wawe katika kila kijiji. Hawa Wakurugenzi wako katika suala hili sisi hatuelewi kabisa kwa sababu sisi tunataka iwe hivi wakati wakiwa kwenye pombe huko, mtaalam wa Maendeleo ya Jamii amelidaka, anakwenda kutoa taarifa Wilayani katika hili pale haliingii hivi, liingie hivi. Sasa kama mtaalam wa Maendeleo ya jamii haonekani kwenye kijiji kile mara kwa mara, siku anakuja kwa sababu mna mipango yenu ya kilimo wakishashtuka watu wanakaa kimya. Lakini wakiwa wanawaona mara zote watakuwa miongoni mwao. Sasa ili aweze kutembelea kila kijiji karibu mara moja kwa siku au mara mbili, lazima awe na usafiri. Mbona Wizara ya Kilimo na Chakula pale Wizarani pikipiki ni za kumwaga na Wilayani pikipiki za kumwaga, inashindikana nini kwenye Maendeleo ya Jamii? Kama mnataka tuendelee muimarishe Idara ya Maendeleo ya Jamii ili tuweze kuitumia vizuri.

Mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, awape semina Wakurugenzi wa Halmashauri, juu ya kazi na umuhimu na mipaka na faida ya Idara ya Maendeleo ya Jamii na watumishi wake, pamoja na kuongeza wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie mchana huu. Nianze na kuunga mkono hoja hii. Naomba nianze na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Nchini ni muhimu mno, lakini inaonekana jamii yetu ya Watanzania na hata baadhi ya wasomi walio wengi bado hawajavipokea kikamilifu. Hii inanielekeza kusema hivyo, kwa sababu hata Serikali yenyewe kwanza inatoa Bajeti ndogo sana kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama vile hawaijali na hawaijui, haina msaada wowote, wanakaa wanahangaika hangaika wakati Wizara nyingine mnazipatia fedha nyingi, huu ni uonevu kwa wanawake, ukitilia maanani kwamba, ni Wizara ya Jinsia ya Wanawake na Wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukitazama Vyuo vyake ni vichakavu mno, walimu hawatoshi, vitendea kazi hakuna, lakini pia Vyuo vingi hivyo bado hamjavisaidia kujiandikisha au kujisajili na *VETA* ili vijana wetu wanapomaliza pale waweze kutambulika mahali pengi wanapokwenda kufanya shughuli zao. Hata Halmashauri zetu hazioni umuhimu wake licha ya kusema *DEDs* ndiyo Wenyeviti wa Bodi na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo, mahali Vyuo vilipo nao ni Wajumbe katika Bodi hiyo. Lakini hawajali kuvisaidia kupata fedha na vilevile hata Bodi hazikutani, hili ni tatizo kubwa na hapo ndipo mnapoonyesha ni jinsi gani Serikali inapendelea baadhi ya Wizara na baadhi ya Wizara zingine hazipendelewi. Unyanyasaji huu naomba Serikali iuache kuanzia leo. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshanisikiliza hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo kwa wanawake ni kidogo mno na kama kweli tumedhamiria kuwakomboa akinamama katika kuondoa kwenye umaskini, ni lazima tuweke mkakati wa kuhakikisha kwamba, wanawake hawa tunawapatia mikopo na kuwapa mafunzo juu ya mikopo hiyo na ikiwezekana tuelekeze mikopo yao kutazama vijiji pale mahali walipo. Ikiwezekana kila kijiji wanawake waliopo pale wakopeshwe. Lakini mbaya zaidi ni wanawake ambao ni walemavu, mimi sijawahi kuona wanawake walemavu wanapewa mikopo, hawapewi kabisa, kwa nini tusiwasaidie kuwakopesha mikopo. Hata Serikali kuwasaidia pengine vifaa vya ulemavu kwa kuvipunguza bei au hata kuwapa bure Serikali badala yake inavifanya kuwa vya gharama na vya hali ya juu kwa walemavu. Je, huo nao siyo unyanyasaji? Naomba Serikali izingatie kuhusu hilo na ijaribu kuona umuhimu wa kuongeza mikopo kwa wanawake na hata pia kuwajali wanawake walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala litakalonipotezea muda wangu wote ni suala la ukeketaji. Mimi binafsi nilikuwa sijui mambo ya ukeketaji yanafanana vipi na pengine ninavyoongea hivi watu wa Jimbo langu na Mkoa wangu, wanaweza wakashindwa kuelewa kwani unaposema ukeketaji haelewi una maana gani, nimeshaanza kuwaelimisha ni nini? Nilipata bahati Wizara ilinialika kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, mwezi Aprili, 2003 kwa siku tatu kule Bagamoyo kuhudhuria ule Mkutano wa Kimataifa uliokuwa unahusiana na masuala haya ya ukeketaji, nilishangaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika Afrika tunaambiwa kwamba kati ya nchi 57, nchi 28 zinashiriki katika ukeketaji wa wanawake. Kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki, Kenya wana makabila 42, lakini ni makabila manne tu ndiyo yanayofanya shughuli hizo za ukeketaji na wanaofanyiwa ukeketaji huo ni kuanzia umri wa kati ya miaka 15 hadi miaka 45 na hao takriban asilimia 38 hufanyiwa ukeketaji huo. Kwa upande wa Uganda makabila hayatofautiani sana na hayo, yapo takriban 37, lakini wao wana kabila moja tu ambalo linafanya ukeketaji nalo ni kabila la Kapcholwa na wengi wanaokeketwa katika eneo hilo wanatokea eneo la Kenya kwa mujibu kwa taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna Mikoa 26 kwa wakati huu, Mikoa 10 katika Mikoa hiyo 26 inafanya shughuli za ukeketaji. Mimi namshukuru Mwenyezi Mungu, Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa

Mbeya haipo katika mambo ya ukeketaji. Wanawake wanakeketwa, wanakataa neno kukatwa, lilionekana kama kuchukiza vile tulipokuwa kwenye Mkutano wetu. Lakini baadhi ya Wajumbe walisisitiza kwamba, hapana ni lazima hilo lisemwe ili ionekane kwamba, kile kitendo ni cha ukatili mkubwa. Kwa sababu wanapofanya tendo la namna hiyo kwanza, wanalifanya bila ganzi na wanalifanya kwa ukatili mkubwa na walituonyesha mkanda mmoja kutoka kule Eritrea nadhani na Ghana, ambapo tulimwona binti anashikwa kwa nguvu, kwanza anapakwa masizi kutishwatishwa namna hiyo, anaogopeshwa ananyweshwa vitu vya ajabu ajabu licha ya kusema wanapiga kelele kubwa, lakini wanaume wamekaa pale wanamkeketa kwa nguvu na damu nyingi zinatoka. Kule shughuli ya kukeketa wanafanya wanaume, lakini kwetu huwa wanafanya wanawake. Wanawakeketa kwa nguvu na kwa kweli wanapata maumivu makali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya juhudi za Tanzania kwa mfano kuanza kukataza ukeketaji, sasa tatizo limegeuka badala ya kukeketa watoto wa kike wenye umri wa miaka 14 hivi na kuendelea, wameanza kukeketa hata watoto wachanga wanaozaliwa, ambao wana siku mbili, tatu, wanawakeketa na watoto wengi wanakufa. Lakini mbaya zaidi ni kwamba, imefikia mahali fulani kwa baadhi ya wale waliokwepa kukeketwa wanapofariki, jamii inakataa kuwazika hapa Tanzania, kwamba hawawezi kwa kwa sababu wana mikosi, hawawezi wakazikwa kwa sababu wana dhambi hawataenda mbinguni na hawawezi wakazikwa kwa sababu balaa kwa jamii inayohusika itawaandama eti kwa sababu hawakukeketwa. Sasa hili linatisha na nitashangaa wanadini wa Kiislam, wa Kikristo na wa madhehebu mengine, kama watakaa kimya bila kukemea na kuweka mbinu na mikakati ya kuzuia jambo hili la ukeketaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia mahali fulani katika vijiji hata katika baadhi ya Mikoa ambapo tupo hapa, Polisi, Watendaji wa Vijiji na Viongozi wa Serikali za Vijiji, wanapewa hongo ili kusudi wahalalishe ukeketaji kwa sababu wale mangariba wanaokeketa huwa wanalipwa chochote kile. Wanapewa hongo halafu wanawaruhusu ili waende kufanya shughuli ya kukeketa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda wameanza kulitatua tatizo hili kwa wale mangariba ambao walikuwa wanafanya shughuli hiyo kwa kuanza kuwaelimisha. Lakini wanapoachana na shughuli hiyo ya ukeketaji, wanawapatia mikopo au wanawawezesha ili waweze kujiingiza katika shughuli nyingine za kujipatia kipato na kuachana na kipato haramu ambacho si halali kinachotokana na ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni, wapo sina haja ya kuwataja, lakini nitawafuata na mmoja nilikwishakumfuata. Wanaume wanaogopa kwenda kwenye Majimbo yao, mahali ukeketaji unapofanyika, kukemea kitendo cha ukeketaji kwa sababu wanasema wakikemea katika jamii zao watakosa kura na Madiwani pia nao wanaogopa. Wale wanaoshughulika na shughuli za ukeketaji watu wa *AFNET*, walipomwendea Mheshimiwa Mbunge mmoja na baadaye kumwendea Mheshimiwa Mbunge mwingine. Mheshimiwa Mbunge huyo aliwafukuza hataki kabisa kuwaona kwamba, nyie mnataka kuniletea balaa. Hivi ninyi mnatetea vyeo vyenu katika udhalimu wa namna hiyo, hivi vyeo vyenu vina raha gani katika kutenda udhalimu. Kama mtu umeamua kuchukua fomu na umeamua kuwaongoza wananchi kwa nini ufunike mabaya kwa sababu ya kutetea wewe uendelee kuwepo. Kuwepo kwako ni laana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusiwe wanafiki. Mimi nadhani kama utakuta kiongozi mzuri nenda kawaambie kuwa ni mila yetu, lakini matatizo yake ni moja, mbili, tatu. Lakini kuwaambia kwamba aah naogopa na mimi nisije nikakosa kuchaguliwa, wakati unajua kitendo hicho ni athari kubwa kwa wapiga kura wako, wewe siyo mnafiki! Unataka kumwongoza nani wewe usiyekuwa na huruma! Nawaomba wale wote mnaohusika katika Majimbo yenu, nendeni mkawaelimishe wananchi na msipowaelimisha katika hili, wananchi watanisikia katika hili, watawakatalieni katika uchaguzi unaokuja kwamba, kumbe mlikuwa mnatupumbaza mnataka tufe, kwa sababu ya kutetea vyeo vyenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwaelimishe wananchi kuhusu suala la ukeketaji waachane nalo lina athari kubwa. Ninaomba nitoe wito kwa vijana wadogo na familia zote, vijana wakatae kukeketwa, katаeni kukeketwa, kwa sababu kama mnakeketwa wazazi wenu hawawapendi wanataka mfe. Baadhi ya wasichana nilipotembelea kama vikundi vitatu hapa katika kufanya utafiti, wakaniambia sasa hivi baadhi ya vijana huko vijijini wameanza kuwakataa wale waliokeketwa kwamba, aah hatutaki kuwaoa kwa sababu mmekeketwa. Aaah si nzuri sana hili kwa sababu wale kwa bahati mbaya walikwishakeketwa

muda mrefu uliopita, mimi naomba hao waolewe. Labda wale ambao wataanza kukeketwa sasa hivi na kuendelea hao wakataeni. Mnaposema katika kuwakeketa eti mnawapunguzia ile hamu ya mapenzi wao wamekataa kwamba, siyo kweli, hata wale ambao tayari wamekwishakeketwa wengine wana hamu zaidi kuliko kawaida! Kwa hiyo, kama mnadhani mnafanya hivyo kuwazuia tamaa, siyo kweli wanatoka kama kawaida. Acheni tendo ovu na baya la kishetani la kuwakeketa wanawake bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishia hapo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kujaribu kutawala wakati, imeonekana kwamba, wale wote waliochangia mara tatu hawatapata nafasi ya kuchangia katika hoja hii, tutamaliza tu orodha ya wale waliochangia mara mbili. Kwa hiyo, tukirudia jioni wa kwanza kabisa atachangia Mheshimiwa Lydia Boma, kwa sababu hajachangia hata moja, atafuatia Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, atafuatia Mheshimiwa Maria Watondoha na atamalizia Mheshimiwa Esha Stima.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia taarifa ya Waziri ambaye yuko mbele yetu. Kabla ya yote, naomba nimpongeze sana Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kazi zake nzuri na kwa jinsi anavyojitahidi, ukiangalia hii Wizara bado ni mpya, lakini yuko makini katika kujibu maswali katika kujitahidi mambo mbali mbali kuleta ufanisi katika shughuli za wanawake. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi na wataalam wote walioshirikiana katika kuandaa hii taarifa. Kabla sijasahau niunge mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeunga mkono nikiwa na maana ya matumaini ya utekelezaji. Kwa hiyo, kitu ambacho kabla sijaendelea kuwaasa wataalamu kuwa mipango mizuri lakini ikikaa kwenye makaratasi itakuwa haina maana kama hatutakuwa na ufuatiliaji wa karibu sana na utekelezaji. Kwa hiyo, ninawaasa nikianza kuweka hilo wazi la ufuatiliaji kila jambo. Wenyewe ndio wawajibike, kuwa makini katika ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais Mkapa, kwa upendo wake kwa wanawake, kwa jinsi anavyojitahidi na bila kutubagua humu ndani katika maelekezo yote anayoyaelekeza kwa Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo na wa Viti Maalum yote kwa usawa. Sasa nasema namtakia kila la kheri na kazi zake nzuri. *(Makofi)*

Pia nampongeza jinsi anavyoangalia jinsi gani wanawake kuwashirikisha katika madaraka sehemu tofauti. Juzi hapa tumekuwa mashahidi, amewateua wanawake watatu kuwa Ma-*DC*. Kwa hiyo, namshukuru na bado tunamwomba asitusahau, asituache kama akinamama wale wenye uwezo, wale wenye elimu ya kutosha, basi asisite kuwachagua na kuwapa madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninampongeza pia kwa ule uchaguzi wa Viti Maalum. Ukisoma Katiba inasema kwamba, atakuwa tayari wawakilishi wanawake asilimia 30. Lakini mpaka sasa hivi tuko asilimia 20. Sasa ninachoshauri hapa Waziri asisite kuwa karibu sana na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, kumpa ushauri na kumkumbusha yale ambayo mwenyewe aliyaweka katika malengo yake.

Kwa hiyo, bado tuna matumaini kwamba, kwa mapenzi yake mwenyewe, jinsi alivyo makini kuwajali akinamama, asilimia 30 ataitekeleza kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitakuwa sina fadhila kama sijamtaja Mama Anna Mkapa, kwa jinsi anavyojitahidi katika shughuli za wanawake, kupitia Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote. Sisi hapa ni mashahidi, amekuwa akihangaika huyu mama mikoani kupeleka misaada ya kila aina kwa walemavu,

habagui, kwa akinamama, mashuleni kupeleka vitabu na hata kwenye Maonyesho haya ya Sabasaba yaliyofanyika nadhani ni yeye peke yake aliyejua kwamba wawepo wanawake moja kwa moja kutoka vijijini kwenda kufanya maonyesho Uwanja wa Sabasaba. Amekuwa akiwagharamia wanapokuja hapa na kuwasikiliza matatizo yao. Kwa hiyo, ninampongeza sana na ninaomba wale viongozi wengine, akina mama wengine wenye uwezo, wamuunge mkono huyu mama katika jitihada zile za kumkomboa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda kwenye maonyesho hakika inafurahisha kwamba, matumaini ya kumkomboa mwanamke yanakuja, lakini bado yanaonekana kwa mbali, pole pole. Kwa sababu wale akinamama walikuwa wanachangamka vizuri sana, wanajua kuwakaribisha wageni kwenye mabanda yao na vitu walivyotengeneza vilikuwa vizuri hata kama wengi wao hawakuuza wakavimaliza, lakini baadhi ya vitu vingine waliviuza na pia walijua kwamba, mimi kama mwanamke, lazima nitoe muda wa kutoa maonyesho ya vitu vyangu. Hayo yote yasingewezekana kama sio Mama Anna Mkapa, kwa hiyo, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti yetu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, naungana na wenzangu walioanza kuelezea huko nyuma na taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, imeeleza kwamba, Bajeti ni finyu, hata mimi nasema hivyo hivyo kwamba, kwa nini Serikali imeweka Bajeti ndogo kwenye Wizara hii ya Wanawake na Maendeleo. Wanawake tumekuwa tunazungumza katika sera mbalimbali kwamba, nchi hii itaangalia maslahi ya wanawake, tutaangalia jinsi gani kumkomboa mwanamke, sasa ni wapi tutakapomkomboa kama si kuipa uwezo hii Wizara. Tunapaswa kuipa hii Wizara. Serikali ione hilo kuipa uwezo ili iweze kuboresha mambo yake, kufanya mipango thabiti ya kuwafikia akinamama kule. Unapounganisha Maendeleo ya Jamii, una maana mambo yote yanaunganishwa katika maendeleo. Lakini maendeleo tunayozungumza hapa mimi naona ni nadharia, haijafika kwenye vitendo kwa kweli jinsi gani ya kumkomboa huyu mama. Serikali sasa ichukue hatua kwa makini kuwa Wizara hii ni nyeti kwa sababu wanawake hawa ndio wanaozalisha, ndio wanaoongeza pato la nchi hii. Kwa sababu haya mazao tunayozungumza hapa kwamba, asilimia fulani imechangia Pato la Taifa, iwe pamba, korosho na kadhalika, kote utakakokwenda katika nchi ya Tanzania, utakuta wanawake ndio wako mstari wa mbele wanazalisha. Kwa hiyo, hawa lazima tuwape kipaumbele ili tutimize azma ile ya kusema kwamba wanawake tutawainua kiuchumi, lakini hapa bado narudia kwa uchungu kwamba, Serikali haijawa makini katika kumwezesha huyu mwanamke kiuchumi ili apate kuwa na maendeleo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kumwangalia mwanamke tuanze kumwangalia tangu mama yule labda anavyokuwa mjamzito. Kwa mfano, juzi tumeuona unyanyasaji ule upo, mama mjamzito hatunzwi wala haangaliwi, lakini bado huyo huyo ndiye anayeweza kuwaweka wananchi walioko katika nchi hii. Kwa sababu kama huyu mama hatazaa basi hata nchi hii sensa kila tukifanya itakuwa inarudi nyuma. Lakini kutokana na sensa jinsi tunavyosema idadi ya watu iko jinsi kadhaa, ni nguvu ya hawa akinamama jinsi wanavyojitahidi kuwa makini. Sasa wakishabahatika wamezaa, tumwangalie huyu mtoto wa kike anatunzwaje? Ndio hao wanaopata janga la unyanyasaji. Leo utasikia mtoto mdogo wa miaka 6 au 7 amepatikana na janga, je, Serikali pamoja na kuzungumza kwamba wana uchungu, watoto wa kike wanabakwa hivi hatua zipi zinazochukuliwa? Bado huyu mtoto wa kike ana maisha magumu tu.

Anaendelea mpaka anakua maisha ni hayo anapambana na mambo mengi. Leo idadi ya watoto wa kike ambao wanakosa shule kwa ajili ya kupata mimba ni kubwa sana. Sera ya Taifa inasema elimu kwa wote, elimu kwa wote itakujaje wakati tunapata watoto kwa mkoa pengine 500 kwa mwaka hawakwenda shule kwa sababu eti wamepata mimba. Hiyo mimba wanaotoa mimba ni wanaume na wanaume wengine ni viongozi wa nchi, hata kama ni Balozi hata kama yuko kijijini kama baba mwenye kaya, yule ni kiongozi. Lakini je sasa hii sheria inamlinda huyu mtoto wa kike ambaye anapata mimba inamlindaje? Ni watoto wangapi wamepata matatizo hayo Serikali imechukua hatua kuwasaidia katika kuwabana wale wanaowaweka mimba, hakuna anayesimamia hii sheria! Sheria imekaa tu yenyewe inaning'inia au imekaa tu kwenye makaratasi lakini hakuna sheria iliyosimama jinsi gani ya kumbana, hata wote tukiulizana sasa kusema je, Serikali kwa mwaka au miaka fulani wangapi walishtakiwa, wangapi walihukumiwa, wangapi walifungwa. Tutakuta bado hakuna ambao wamechukuliwa hatua. Kwa hiyo, hili nalo ni tatizo, ningeishauri Serikali iangalie unyanyasaji wa mwanamke ambaye ndiyo huyo huyo tegemeo la Taifa kwa mambo mengi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la TAMISEMI wenzangu wamelizungumza. Ni kweli na mimi ninasisitiza kwamba, Wizara hizi mbili zipate muda ziketi, TAMISEMI pamoja na Maendeleo ya Jamii, waangalie ni mipaka ipi kila mmoja aifanye, kwa sababu leo utakuta kwa mfano fedha hizi unazotenga zinafikia mikononi mwa TAMISEMI, lakini bado Maendeleo ya Jamii inasikia baadaye kwamba, fedha zimetoka itafanya nini. Kwa sababu Idara yenyewe bado inanyanyasika hata kwenye Halmashauri zingine kila mara watasema punguza Idara, Idara ya kwanza ndiyo maendeleo wanayojadili kwamba tupunguze Idara. Wakati Idara ya Maendeleo ndiyo inayohudumia wananchi kwa karibu sana huko nyuma. Mifano ninayo leo akina baba wanauliza wanasema Idara yetu iko wapi, wanasema kaiambie Serikali tunataka Idara ya Maendeleo irudi tena madarakani, je, ni kweli Idara ya Maendeleo haipo?

Idara ya Maendeleo ipo lakini sana sana labda iko TAMISEMI, mikoani bado ni mashaka, hali kadhalika Wilayani, hali kadhalika vijijini ambako ndiko waliko walengwa wanawake, wenye kunyanyasika, wenye kuteseka, wenye matatizo, bado Idara kule haipo na ndio hawa wanaume wanauliza kwamba Idara yetu iko wapi. Kwa sababu kule nyuma ilikuwa inawasaidia Bibi Maendeleo, Bwana Maendeleo kuangalia usafi wa nyumba, kuangalia jinsi gani nyumba mazingira yake yako safi, nyumba imebomoka waijenge au waisilibe, lakini siku hizi utakuta nyumba hizo ni za kusikitisha, hazina vyoo. Nyumba utaikuta imebomoka ina miaka 10, 15 ina mbavu za mbwa, lakini wakati ule Idara ilipokuwepo ndiyo ilikuwa wahamasishaji, leo uhamasishaji ule haupo. Wale wachache waliopo utakuta wamekaa ofisini kazi ya kuandika muhtasari, je, ajira inamwelekeza hivyo kuwa yeye mwandishi. Huyu aende kwa watu. Kwa hiyo, naomba wizara hizi zione jinsi gani waungane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo nyongeza ya ile hali ya kwamba bado imekufa kule Vijijini au kwenye Kata. Utakuta hawana ofisi hawa. Mabibi na Mabwana Maendeleo, ofisi zao mpaka uzitafute huko vichakani ambako zilijengwa enzi ya wakoloni na hawana usafiri, hawana pikipiki, hawana baiskeli, lakini ukienda kwenye Idara zingine unakuta nyenzo wanazo, kwa nini Idara hii haitambuliki, kwa nini inakosa nyenzo. Kwa hiyo, Serikali mimi naiambia kwamba, kama haina mafungu ya kununua moja kwa moja kuwapelekea, basi watoe mikopo wawakopeshe na sasa hivi Idara iboreshwe, itupe nyenzo wananchi kama sawa na malengo yetu yanavyoelekeza kwamba watakuwa karibu na wananchi, sasa watakuwaje karibu kama hakuna nyenzo. Hiki kitendo cha kusema kwamba, Ofisi hawana labda nirudi nyuma kwamba, Waziri sisi ndio tunaokuelekeza hali ilivyo ngumu kule, watumishi hawana ofisi nzuri, mimi wamenipeleka kwenye ofisi zao nyingine inasikitisha kama *godown* haina viti wala nini. Kwa hiyo, hili suala nalo linatisha na bado naiuliza Serikali hivi Idara hii tunaifuta, Idara hii hatuihitaji na kwa nini hatuihitaji wakati wakulima wenyewe wanaitaka? Maana ya kuuliza kwamba iko wapi ni kwamba wanaihitaji Idara irudi kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha shughuli za wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini, ni lugha imekuwa ikuzungumzwa lakini hatutaondoa umaskini kama wanawake hawa hatukuwawekea mipango mizuri. Lazima tuwawekee mipango mizuri itakayokidhi haja na vile wanavyotengeneza tena akinamama wameitika wito vijijini, Sera hii wameitekeleza vizuri sana katika mazingira magumu. Utakuta wana miradi mbalimbali, lakini miradi ile imekuwa sasa ni majuto kwao. Kwa sababu vitu vile wametengeneza vimewazunguka hawajui wavipeleke wapi, hawajui soko liko wapi na wafanye nini na sisi wenyewe ndio tuliwahamasisha. Kwa hiyo, tuhakikishe kuanzia angalau Bajeti inayokuja iwe inajieleza kuwa wanawake wakishapata miradi yao wameitengeneza kutoka kijijini wataipeleka wapi mpaka wapi tayari wawe wameshauza. Suala la kutegemea kwamba, wanakwenda Saba Saba kuonyesha maonyesho. Ndiyo anakwenda kuonyesha maonyesho na baadaye akishamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nami sina budi kukushukuru wewe kwa umahiri wako, kwa kukikalia hicho kiti kwanza. *(Makofi)*

Lakini katika hatua yangu inayofuata, naomba pia niishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jami, Jinsia na Watoto, kwa shughuli nzuri ambayo kwa leo mimi sitokuwa na mengi sana katika Wizara hii kwa sababu mengi miongoni mwa niliyotaka kuyazungumzia, naona wameyaeleza wenyewe na wameyaweka sawa. Sasa hapa ninachoomba ni kutoa shukrani zangu tu za dhati kwao, kwa shughuli nzuri waliyoifanya kwa kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Makatibu na wote wanaohusika na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitakuwa na madogo madogo tu nayo naomba niende katika suala zima la Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kweli nimekuwa nikifuatilia sana shughuli nyingi ambazo zinafanywa na Wizara hii pamoja na ziara tulizozifanya wakati tuko katika Kamati pale Dar es Salaam na sehemu nyinginezo, mimi niseme tu kwamba, Wizara hii imejitahidi sana. Sasa kuna maeneo madogo madogo naomba niyazungumze kwa kuanzia kwamba, tulipotembelea Kisarawe kule kwa kweli tuliona baadhi ya shughuli zinakwenda vizuri lakini nyingine hazikuwa zikienda vizuri na hapa namwomba Mheshimiwa Waziri, asiwe na wasi wasi sana. Hapa nitataka kusema kidogo kidogo tu kwa sababu kuna mambo madogo madogo ambayo tulimshauri na katika hii hotuba yake sikuyasikia, sasa nitamwomba na hayo baadaye ayazingatie na atueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulipokwenda pale kile chuo mpaka tunaondoka sisi hakina hatimiliki, hakina uzio yaani hawajui maeneo yao yepi, sisi walituonyesha onyesha sijui mpaka hapa mpaka hapa. Sasa Mheshimiwa Waziri, sisi kwa pamoja tukakubaliana kwamba, nalo hili lizingatiwe ili wale waliopo pale nao wawe wana uhakika na wanachokifanya kwa sababu ardhi ni mali kila mtu anaihitaji. Sasa ni jambo zuri kama hao vijana wetu au hii Taasisi yetu ikiwa inaelewa maeneo yake rasmi. Lakini pia tuliona pale kwamba, ule utendaji kwa wale walimu na viongozi walioko pale kidogo ulikuwa una mashaka mashaka. Sasa mimi naomba tu Mheshimiwa Waziri, kama bado hujachukua hatua basi ufanye haraka kwa sababu wanaopata tabu pale ni wale vijana wetu na sisi tulikuwa mashahidi wa shida hizo wanazozipata sasa si busara kuona bado wanaendelea na shida hizo kwa sababu wale ni miongoni mwetu na tunawategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa shughuli tulizozifanya pale wakati wa Kamati, tulitembelea vikundi vya Baba Lishe na Mama Lishe. Tulikuta mambo mazuri kidogo lakini kukawa kuna malalamiko sasa sijui hili nalo Waziri ameliweka katika fungu gani. Kwa sababu tumekwenda sehemu fulani tukawakuta wale wanaoshughulika wamepewa vibanda vizuri tu. Lakini sasa vibanda vile baada ya kuwasaidia vimekuwa vinawadhalilisha na vinawapa mashaka. Vibanda hivi hawa vijana wanasema wamekodishwa kila mwezi wanalipa shilingi 15,000/=, hizi hazina mwisho wanalipa shilingi 15,000/= mpaka watakapoacha hii shughuli. Sasa hili sisi tuliliona si jambo zuri kwa sababu unapomkodisha kitu ambacho ungemweleza tu kwamba, hiki ninakuuzia kwa kiasi kadhaa utalipa baada ya miaka miwili kinakuwa chako, lakini wanakodishwa kwa shilingi 15,000/= kila mwezi na ukiangalia biashara zenyewe hazifanani na hali halisi ya wakati wetu kwa sababu sote tunaelewa kwamba, kwa kipindi tulichonacho hiki, biashara zimekuwa ngumu, wateja wamekuwa wana usumbufu kidogo. Sasa hapa sisi tulishauri tukasema hivi vibanda vizuri vinastahili kuwepo, lakini sasa viangaliwe wapunguziwe bei ya kukodisha au wauziwe, aambiwe mtu utalipa kama shilingi 100,000/= au 150,000/=, ulipe kidogo kidogo ukimaliza kibanda kiwe chako. Tulifikiria iwe hivyo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema awali kwamba, leo sitokuwa na mengi sana kwa sababu kwanza hii hotuba mimi naona imejijibu karibu maeneo yote. Lakini ninachotaka kusema katika hotuba hii kuna kitu kimoja sikukiona nacho ni suala zima la walemavu kwamba, msisitizo gani umewekwa kuhusiana na ndugu zetu, wenzetu miongoni mwetu ( walemavu). Kwa sababu ninachotaka kusema hapa labda hatukifahamu vizuri sisi sote ni walemavu watarajiwa, wakati wowote, saa yoyote miongoni mwetu anaweza akatokezea mtu kama huyo. Sasa tusipoliweka kabisa hili kwa kuwa labda mimi Yussuf najiona sasa hivi niko kamili baadaye nitakuwa sina pa kukamata wala sina wa kumlilia. Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba, suala la ulemavu liandaliwe utaratibu maalum na isiwe wa kujaliza jaliza tu, uwe maalum kwa maana hata kama kwenye Katiba yetu labda kipengele hicho hakimo basi tukiingize kiwe rasmi na katika shughuli zetu za Wizara au Idara zinaohusika basi iwe kuna utaratibu maalum ambao unawashughulikia walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nizungumzie UKIMWI na niseme tu kwamba, kwa kweli hili tatizo hakuna asiyelijua. Lakini mimi nashangaa kwamba, pamoja na kulijua kwetu bado tunalidharau. Tunasema tunalidharau kwa sababu, sababu za kuenea kwa UKIMWI sote tunazijua. Vishawishi vinavyosababisha UKIMWI sote tunavijua, lakini utashangaa watu wanavikimbilia wanavishangilia na hatimaye wamezama huko na kila siku imekuwa tunalalamika UKIMWI utatumaliza, UKIMWI utatumaliza. Mimi nafikiri labda nitoe rai moja. Inapotokea labda imebainika miongoni mwa

wale watu wawili ambao wanafanya hayo mambo yao, labda mmoja anavyo virusi na ikagundulika labda kwa makusudi amesababisha mwenziwe apate, mimi nadhani tungekuwa tuna jambo hili ambalo nitalisema ingekuwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo itakuwa tunakuja hapa tunaimba tunaondoka tunapiga mabao, tunaondoka lakini kama itathibitika miongoni mwa wawili hawa mmoja anamwambukiza mwenziwe kwa makusudi, basi kwanza yeye huyo adhabu yake iwe kifo. Ndiyo, sasa nyinyi mnataka kuondoa tatizo halafu mnasema huyu, huyu, nini? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ongea na Spika. Zungumza na Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa wakweli katika jambo tunalotaka kulipiga vita, mimi siamini kama tutalimaliza na si hivi tu kana mengineyo yapo, lakini kwa hili tukianza hapo basi mwenye virusi atakwenda kwa mwenye vurusi mwenziwe, itakuwa mchezo umekwisha na wale wazima watatafutana wenyewe. Lakini kama tutabaki kusema tu sijui tumia mipira, tumia nini, tutaishia hivi hivi na kuja hapa kupiga mabao hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, naunga mkono hoja hii kwa sababu imenifurahisha sana na baada ya hayo nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Awali ya yote, niseme kabisa kwamba, ninaiunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu katika kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote, walioko Makao Makuu ya Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa ushirikiano mkubwa wanaouonyesha katika *team work* yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu juzi Mheshimiwa Waziri, alikuwa Nitu Singh na Naibu Waziri Amrisha Patel na wamefanya onesho zuri kabisa la kuvutia. Maafisa wa Wizara yao kwa kundi wamekuja kuwashangilia. Kama wasingekuwa na umoja Wakuu wa Idara hawa wasingekuja, lakini nawapongeza Nitu Singh na Amrisha Patel, kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano walioujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia katika maeneo yafuatayo. La kwanza ni Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi viko karibu katika kila Mkoa. Kule kwetu Lindi kipo Chuo cha Chilala na Chuo cha Kilwa, kipo Kilwa Masoko. Baadhi ya vyuo hivi sasa hivi mimi naona kama vinasinzia havionyeshi cheche zake kama pale awali. Vyuo hivi viko maeneo ambapo kuna wananchi wanaohitaji elimu, ujuzi na ushauri. Mimi nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 14 ameonyesha kwamba, kila Halmashauri ilipewa shilingi 4,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ili wakopeshwe waweze kufanya shughuli za kibiashara ambazo zitawasaidia kujikwamua kiuchumi, ambazo zitawasaidia kupunguza kiwango cha umaskini ambacho kimezagaa kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nyingi hazijarejesha fedha. Katika orodha hii, pamoja na Halmashauri ya kwetu Lindi. Inawezekana kabisa pamoja na nia nzuri ya Serikali, tatizo linakuja kwa sababu wanawake au vikundi vinavyopewa mikopo, hawana taaluma ya kuendesha biashara, hawana *entrepreneurship skill.* Vyuo hivi vipo na kwa kuwa shilingi 4,000,000 zinatolewa katika kila Halmashauri, nashauri Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha kila anayechukua mkopo anapata kwanza *entrepreneurship skill* badala ya kugawa fedha na kuwapa mikopo ambayo watashindwa kurejesha.

Kwa sababu wakipata taaluma ya namna ya kuendesha biashara na wakaelekezwa kabisa kwamba, umekopa hakikisha unarudisha watakuwa na uwezo wa kurejesha na fedha zile zitazunguka. Ama sivyo tutabaki kudaiana hatimaye tutakwama. Taaluma hii inaweza ikatolewa katika Vyuo vyetu vya Wananchi.

Wakaoenda pale wachangie kwa kiasi ili waweze kupata elimu hiyo, hivyo wakipewa mikopo watajua uendeshaji mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia hizi fedha, nimekuta kwamba, kuna Halmashauri ambao vikundi vilivyoandikishwa wamepewa Sh.200,000/= na kuambiwa haya nendeni mkagawane, mtarudisha kwa wakati wenu. Hawajafuatiliwa wanafanya biashara gani, hawajafuatiliwa wana malengo gani au watarejesha vipi! Katika hali hii, hatusaidii kuwakwamua Wanawake, tuwasaidie kwa kuwapa taaluma na waelewe ili zile fedha wazitumie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, napenda nishauri kwamba, kwa sababu vyuo hivi viko karibu katika kila Mikoa, viandae mitaala kufuatana na mazingira ya Mkoa husika. Kwa mfano, kwetu (Lindi), wanapotaka kufundisha masuala ya kilimo cha kisasa, basi wafundishe kilimo cha ufuta, kilimo cha mtama na kilimo cha korosho, lakini wakienda *generally* haifai! Hiyo natoa mfano tu, lakini yapo mazao mengi ambayo yapo na yanahusika katika Mkoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mitaala iwe kwa ajili ya eneo husika ili chuo kiwe kinatoa taaluma kwa vijana wanaotoka katika eneo lile. Ama sivyo vyuo vyetu vitakuwa vinasinzia, haviendeshi shughuli zao vizuri. Mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Chuo cha Chilala, lakini kwa kweli sijaona *impact* yangu katika kuhakikisha shughuli za chuo zinaenda vizuri.

Eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu suala la UKIMWI. UKIMWI ni janga na sasa hivi unanyemelea hasa Vijijini kwa sababu huko Wananchi wengi ni maskini. Vijijini ndio kuna asilimia 80 ya wakazi wa Tanzania na tumeona katika sensa ya mwaka 2002 kwamba, zaidi ya asilimia 51 ya Watanzania ni Wanawake. Hii asilimia 51 ya Wanawake ndio nguvukazi ya Tanzania, hawa ndio wazalishaji, lakini kwa jinsi kasi ya UKIMWI inavyokwenda, nina hofu hasa kwa sababu ya umaskini uliokithiri kule Vijijini, nguvu kazi hii itaangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu nilieleza hapa siku moja kwamba, mgeni akija Kijijini akimpa mtu Sh.1,000/= anaona amepata milioni! Lakini njia moja ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeainisha katika suala la kupambana na UKIMWI na suala la kupambana na kuondoa umaskini ni elimu. Utakuta pamoja na nia nzuri iliyopo, maeneo mengine watoto hawaendi shule kwa sababu hali ya familia ni duni mno, hawana chakula! Kwa hiyo, mtoto anaenda kufanya kibarua ili angalau alete Sh.200/= waweze kula au mtoto anaenda kuuza maandazi angalau wapate chakula! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunapata fedha za misaada ya kupambana na UKIMWI. Lakini ukifuatilia fedha nyingi zinaenda kwenye semina na kwenye warsha. Wanaopewa semina na warsha hizo wengi wamefuzu, wako Mjini na wana uwezo wa kutosha! Naomba tuige wanavyofanya nchi nyingine katika Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mahali kwenye *curia* moja, katika kuhamasisha watoto waende shule na kuhakikisha kweli wanajiandikisha na wanahudhuria, kila mtoto kila siku anayohudhuria anapewa Sh.500/=. Mtoto wa Biti Selemani akirudi na Sh.500/= na kumpa Mama yake, jirani yake Mama George atamwuliza: "Umepata wapi hii Sh.500/=?" Atajibu: "Mwanangu ameenda shule ndio akapewa." Utaona mmoja kila siku anavyokwenda anapata hela, basi na jirani anavutiwa mtoto wake aende shule, anajua akitoka huko atarudi na hela ya chumvi. Kuliko kuzitumia fedha hizi kwenye warsha na semina zisizoisha kwa ajili ya watu ambao kwa kweli wamepevuka. Hebu ziende zikasaidie Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna watoto wengi wa mitaani tunawasaidia. Hivi ni wangapi tumekaa nao kuwahoji wanatoka wapi, wazazi wao wako wapi na kwa nini wamekimbia? Tunaweza kupata sababu ya msingi. Inawezekana wengine wamekimbia kwa sababu ya kila siku kutumwa nenda, nenda, badala ya kwenda shule aende akahangaike ili alete chakula nyumbani. Ninaomba suala hilo tuliangalie. Tutapiga vita UKIMWI na tutapiga vita umaskini kwa sababu mtoto akipata elimu anaweza kuwasaidia wazazi wake vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni kwamba, napenda kuungana na wenzangu wote waliozungumzia Idara ya Maendeleo ya Jamii. Idara hii ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya

Wananchi Vijijini. Nchi hii toka tumepata uhuru Maafisa Maendeleo ya Jamii ndio walikuwa wahamasishaji wakubwa wa kampeni zote za Kitaifa. Walikuwa wanaenda Vijijini kuhamasisha kilimo cha kufa na kupona, wanaenda kuhamasisha elimu ya watu wazima, uchimbaji wa vyoo, uandikishaji wa watoto na kadhalika. Wao walikuwa wanaandaa njia ili wahusika wa kampeni ile wanapokuja, wanakuta Wananchi wameandaliwa, hivyo kazi yao inakuwa rahisi. Lakini sasa cha kusikitisha, Maafisa Maendeleo ya Jamii, huwakuti Vijijini! *(Makofi)*

Ninaishauri Serikali iangalie muundo wake ili tuhakikishe kwamba, tunakuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya kila Kata katika nchi hii. Tufanye kazi, bado tuna kazi kubwa katika nchi hii ya kuhakikisha Wananchi wetu wanalima inavyotakiwa na tunayo kazi kubwa ya kuhakikisha Wananchi wetu wanakuwa na afya nzuri, lakini wahamasishaji hawatoshi. Tukienda na rungu la Sheria tu bila kuandaa, ndio inapotokea migogoro tunayoisikia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa ananisimulia Mheshimiwa mmoja ndugu yangu, jinsi Wananchi walivyokataa hifadhi ya mwambao! Lakini tungepata Afisa Maendeleo ya Jamii, akawaandaa, akawaelimisha na akawahamasisha Wananchi hao vizuri, kwa mwezi au miezi, kazi ile isingekuwa ngumu. Ninaishauri Serikali iingalie Idara hii kwa jicho la pekee, kwa sababu pamoja na maendeleo tunayoyaona Mijini, bado tunayo kazi kubwa Vijijini ambapo Wananchi wetu wengi wako kule na wengi bado ni maskini. Siyo maskini kwa sababu wanautaka umaskini, lakini ni maskini kwa sababu nyenzo wanazozipata ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ambalo napenda kuchangia ni kuhusu nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya nchi yetu. Kama nilivyosema, Wanawake ni zaidi ya asilimia 51 katika nchi hii na wanafanya kazi kubwa sana kule Vijijini, ndio wakulima wakubwa na ndio wanaotulisha katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *NGOs* nyingi zinazoshughulikia Wanawake, lakini hebu tujiulize *NGOs* hizi ziko wapi? *NGOs* hizi ziko Mijini, zinaendesha semina, makongamano na warsha. Lakini yule mwanamke anayevaa kaniki kule Kijijini, anayenyanyaswa na mume wake akiwa mjamzito nani anamkumbuka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ndio tunaowapigania, walio Mijini wameona mwanga, wanajua nini haki yao na wanajua namna ya kupambana, lakini kule Vijijini bado. Kwa hiyo, natoa wito kwamba, *NGOs* zetu zisiishie Mijini tu, hebu twende Vijijini tukawahamasishe, kwa sababu katika baadhi ya maeneo, Wanawake wananyanyaswa kutokana na mila na desturi zetu, hata ukiwaelimisha vipi, anakaa mnyonge, anasema hawezi kusema neno, anajifunika. Lakini mwanamke si mnyonge bwana, mwanamke ana uwezo na tumeona hapa Wizara zinazoongozwa na Wanawake jinsi zinavyofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache. Kwa bahati mbaya ukiwa wa mwisho raha yote ya kuchangia inakuwa haipo, kwa sababu mengi yanakuwa yamechangiwa na wenzako, lakini nami nina maeneo muhimu ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri na ninampongeza sana kwa kazi nzito anazozifanya, pamoja na Naibu wake na watendaji wote, kwa kuifikisha Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuchangia katika suala zima la kuanzishwa kwa Chombo cha Wanawake kupitia Wizara yake kwa awamu ya pili. Nasema kwa awamu ya pili, kwa sababu chombo hiki kiliwahi kuundwa kupitia madaraka ya UWT (Wanawake wa CCM), kwa wazo la Marehemu Mama Sophia Kawawa. Mara baada ya kuona kwamba, tunaelekea kwenye mfumo wa Vyama Vingi alisema: "Sasa lazima Wanawake wawe na chombo chao bila kubagua Vyama vyao vya kisiasa." Ndipo ukaitishwa Mkutano Mkuu kule Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwa mapendekezo ya Uenyekiti, akateuliwa dada yetu Anna Tibaijuka. Lakini napenda kusema kwamba, kutokana na kutokuwa na utoaji wa elimu kwa

Wanawake na kwa Viongozi wao, chombo kile cha awali kilileta matatizo na nyie wenyewe ni mashahidi, hakikutumika ilivyotarajiwa, kikatumika vibaya hatimaye msajili akakifutia usajili wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo basi, ili tusije tukatokewa na tatizo la aina ile ile, basi Waziri afanye utaratibu wa makusudi wa kutoa elimu katika vyombo vya habari, kila mtu ajue madhumuni ya chombo hiki kwa mara ya pili, vinginevyo Wanawake watadhani kwamba, wanasumbuliwa tu kwa sababu kilikwishaundwa na sasa wanarudia tena, labda wanafanya hivyo kwa maslahi yao. Kumbe sio hivyo, madhumuni na nia ya Waziri ni nzuri na itakuwa na maslahi makubwa hapo baadaye. Kwa hiyo, kitu kikubwa ni kuzingatia elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, alikwishatueleza hapa wakati anasoma hotuba yake kwamba, wamekwishafanya kikao hapa Dodoma, nampongeza sana kwa hatua hiyo pamoja na wenzake akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ni jambo la kushangaza kwa sababu baadhi ya Wabunge hatukualikwa kwenye kikao kile, ni Wanawake wachache waliohudhuria! Binafsi nina hofu kwamba, kwa mtindo huo, tunaweza tukapoteza mwelekeo tunaoukusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwomba radhi Mheshimiwa Waziri, asifikirie kwamba, namkosoa katika hili, ila ni katika kushauriana na kukumbushana. Kutokana na kwamba, shughuli zao ni nyingi, basi naomba walijue hilo, wafanye utaratibu wa kutoa semina kwa Wabunge wote ili tupate kulielewa, kwa sababu sisi tukielewa vizuri tutasaidia sana kuwaelimisha wapigakura wetu katika Majimbo yetu na kazi yake itakuwa rahisi kuliko itakavyokuwa bila sisi kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Wanawake na Wanaume huko Vijijini, Wilayani na Mikoani waandaliwe semina zitakazotolewa na watumishi wake wa Maendeleo ya Jamii, ambao wako Mikoani. Shughuli hii ya kufanya semina peke yake kila kona haiwezi, lakini akitoa nyenzo basi Wizara husika katika ngazi ya Wilaya na Mkoa wataweza kutoa elimu hiyo na chombo hiki kitakuwa cha kudumu, hakuna mtu atakayekuja kukiyumbisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiendelee kuzungumza sana, mwisho nitakuja kuishiwa muda halafu nishindwe kuunga hoja mkono. Naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja halafu ndio niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie katika eneo lingine linalohusu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Binafsi ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Bodi mara mbili mfululizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna matatizo katika Vyuo vyetu ya Maendeleo ya Jamii. Inadhihirika wazi kwamba, hawana uwezo wa kifedha wa kuendesha Vyuo hivyo. Kwa misingi hiyo, Wakurugenzi wa Vyuo hivyo wanaendesha shughuli zao bila kuitisha Vikao vya Bodi. Kuna Mbunge mwenzangu amechangia hilo, nadhani hii itakuwa ni kwa Vyuo vyote. Kwa misingi hiyo, kama tunataka Vyuo hivi vifanye kazi vizuri na viweze kutoa elimu kwa Wananchi, naiomba Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii ili iweze kutoa ruzuku kwenye Vyuo kuendesha shughuli zao vizuri. Kwa sababu kama nilivyosema nimeteuliwa, ni Mjumbe wa Bodi, lakini wanashindwa kuitisha vikao, wanafanya shughuli zao kienyeji bila sisi kufahamu na Mheshimiwa Waziri, atakapotuuliza tutashindwa kumueleza. Nimekwishamuandikia barua Mheshimiwa Waziri, kumuelezea juu ya tatizo hili. Lakini hao Wakuu wa Vyuo siyo makusudi yao, watafanyaje? Ndio sababu wanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Fedha, lakini simuoni hapa nadhani yuko kwenye shughuli zingine, basi kukiwa na uwezekano tunaomba waongeze Bajeti Maalum baadaye au kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 ili kuweka nguvu ya kuendesha Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kuhusu soko la bidhaa zinazotengenezwa na Wanawake nchini kote ukiwemo na Mkoa wangu wa Shinyanga. Kwa hakika Wanawake wanajitahidi sana kujiondoa katika umaskini, lakini tatizo kubwa ambalo lipo na ambalo mpaka hivi sasa linalojitokeza mara kwa mara ni kukosa soko la kuuza bidhaa zao. Kwa misingi hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, arudishe utaratibu ule wa zamani uliokuwa unaandaliwa na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na

Watoto, kufanya mashindano katika ngazi za Wilaya na Mkoa na kwa hiyo, kule kule Wilayani wanaweza wakapata soko, Mkoani wakapata soko na hatimaye wale ambao bidhaa zao zitakuwa nzuri waende kwenye maonyesho ya Saba Saba kutafuta soko la Kitaifa kuliko ilivyo hivi sasa, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba, Wanawake hao hawana uwezo wa kujiwezesha kufika Dar es Salaam kushiriki maonyesho ya Saba Saba. Kwa suala hili nilikuwa nimemuandikia Waziri wa Viwanda na Biashara wakati nachangia, kwa sababu nilichangia kwa maandishi, nikamwomba kwamba basi watafute uwezekano wa kuwawezesha Wanawake hawa wakiwa Dar es Salaam waweze kuishi vizuri na kwa usalama kuliko ilivyo hivi sasa. Waume zao wanakuwa hawana uhakika wa jinsi Wanawake hao watakavyoishi salama wakiwa Dar es Salaam, kwa hiyo, wengine wanakatazwa. Mtu anamwambia mkewe, wewe huna pesa utakwenda kuishi vipi huko! Utakwenda kuwa guo guo tu mitaani! Lakini kukiwa na uhakika kwamba watakula vizuri, wataishi vizuri, watakwenda kwenye maonyesho na watapata senti kidogo za kuwawezesha kununua hata soda, wataruhusiwa kwenda na hakutakuwa na matatizo ya suala hili zima la kutafuta soko kwa ajili ya shughuli zao. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kama kutakuwa na uwezekano, lakini nina uhakika uwezo wake ni mkubwa katika masuala ya Wizara hii, basi atafute linalowezekana ili kuwapa Wanawake uwezo wa kufika kwenye maonyesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, mara nyingi taarifa za Wanawake kushiriki katika maonyesho haya huwa zinapitia kwenye Halmashauri zetu za Wilaya au Manispaa. Tatizo kubwa ni kwamba, mawasiliano huwa hayaenezwi sawasawa kwa akina mama. Barua zingine zinafichwa na Wanawake hawajui! Watu hao wanazificha barua hizo kwa kukwepa tu kusumbuliwa au kuhakikisha ni namna gani Wanawake hao wanakwenda Dar es Salaam kuhudhuria maonyesho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, Wanawake wenyewe wangekuwa wanapewa taarifa moja kwa moja kwa sababu nadhani orodha ya Wanawake wanaoshiriki kila mwaka katika Wizara yake anaweza akaifahamu na kama hawezi kuifahamu, basi awasiliane na Mheshimiwa Mama yetu, Mama Anna Mkapa, ambaye kwa kweli tunamshukuru sana na tunampongeza kwa kazi nzito anayoifanya, kuwafadhili akina mama kwa chakula, malazi na usafiri wa kufikia kwenye maonyesho wakati wa kipindi cha Saba Saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa utaratibu wake wa kutupatia nakala Wabunge aendelee nao. Nampongeza sana kwa hilo kwa vile huwa anatupa taarifa. Lakini kwa vile mambo haya yanapitia kwenye Manispaa au kwenye Halmashauri, unaona kwamba wao wamekwishatekeleza suala hilo. Ukija kwenda kwenye mabanda unashangaa kwani hukuti Mkoa wako umeshiriki katika shughuli zile! Nimeona suala hilo safari hii, nimezunguka kwenye Saba Saba naangalia Mkoa wangu sikuuona, basi sikuuliza neno, nikarudi kwa aibu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, mwaka 2004 aibu hii nisiipate tena, atuwekee mambo vizuri ili tuweze kushirikiana kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu usajiri wa *SACCOS* hizi ambazo zinaanzishwa na Wanawake. Sheria inasema miezi mitatu ndipo isajiliwe. Naomba kama hakuna tatizo kubwa kwa chombo kile cha Wanawake kuchunguzwa miezi mitatu kisajiliwe mapema, sijui kinachunguzwa kitu gani sana mpaka wanacheleweshewa usajili! Wanawake wanakata tamaa katika utaratibu huo. Kuna Vyama ambavyo vinapaswa kuchunguzwa kwa miezi mitatu kutokana na utaratibu, lakini hizi *SACCOS* ambazo malengo yake ni kujipatia maendeleo ya kiuchumi kwa Wanawake, sioni sababu nzito ya kuchunguzwa muda wa miezi mitatu kwa ajili ya suala kama hilo na mpaka waandike maombi, wapeleke kwa wanaohusika ni karibu miezi minne, mitano, mpaka sita!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utekelezaji wa suala hili kwa sababu linatutokea na tunashuhudia jinsi linavyosababisha usajili wa Vyama hivi vya *SACCOS* kwa ajili ya Wanawake kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika suala la UKIMWI, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia, nami napenda nilizungumzie kwa maelezo machache tu kwamba, Wanawake wapo chini ya Wizara yake na mateso wanayoyapata ni wajibu wake Mheshimiwa Waziri, kujua wanateseka vipi na wakwamuliweje katika matatizo ya aina hii.

Namwomba ashirikiane pia na Wizara ya Afya kujua na kuona Wanawake hawa wanaoathirika wanasaidiwaje na kwa kiasi gani. Pia, anaweza akaweka mchango wake ili walau waweze kuwalea watoto wao na waweze kusogeza sogeza muda wa kuishi. Wanawake hao huwa wanachanganyikiwa kwa hilo, wanalia kila wakati kwamba, mimi nakufa, watoto wangu nani atawalea? Kwa hiyo, hayo yote namwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie kuweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, naunga mkono tena hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Wizara kwa juhudi zake. Lakini ninaomba nisaidiwe kupata maelezo ya kuweza kusaidia katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Tunashkuru kwa hatua za awali za uanzishwaji wa Benki hiyo. Mpango wa kuanza na *SACCOS* zake ni muafaka kabisa lakini nini mkakati wa makusudi wa Wizara wa kuzisaidia *SACCOS* za wanawake zilizokwishaanzishwa ili wanawake wengine wajifunze toka huko na kuharakisha kufikia azma hiyo.

Mfano *SACCOS* za Wanawake Mkoa wa Ruvuma na pia *SACCOS* za Wanawake Lushoto kwa Mheshimiwa Shekiffu, japo hata Wizara kuandika na kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu suala la watoto wadogo chini ya miaka mitano. Miongoni mwa *Millenium Development Goals (MGDs)* za kupambana na umaskini ni pamoja na suala zima la vifo vya watoto *under 5 years.* Ninaomba Wizara inisaidie kufahamu yafuatayo:-

(i) Nini hasa mkakati wa kuhakikisha vifo hivyo vya watoto vinaisha au kupungua na hasa kuchukua tahadhari ya kukinga. Tatizo kubwa ni la umaskini wa hali unaopelekea ongezeko la UKIMWI, lishe duni, kutoweza kuwa na uwezo wa kinga ya malaria na kadhalika.

(ii) Mheshimiwa Waziri wa Elimu, alipokuwa anajibu hoja yangu katika Wizara yake ya kujua nani ni mhusika zaidi wa kusaidia huduma ya makuzi ya watoto *under 5 years* alisema, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ndiye mhusika wa watoto hao. Ningetegemea kuona mpango wa Wizara wa makusudi wa kusaidia malezi na makuzi ya watoto hao, kwa kuzingatia umuhimu wa kisayansi wa kukua kwa ubongo wa *ratio* kubwa katika umri wa kuanzia 0 - 5 ukilinganisha na ukuaji wa miaka 5 mpaka utu uzima. Uko umuhimu wa kuangalia hilo.

(iii) Uwezeshaji wataalamu, kwa kuwa maendeleo ya jamii yanaenda na wakati, ninashauri sana Wizara ione umuhimu huu wa kuwafundisha wataalamu mbinu za maendeleo kulingana na wakati sasa.

(iv) Asilimia 10 ya vijana na wanawake iongezwe na zaidi Halmashauri zitoe hizo asilimia 10 za mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii iliyotoa mwelekeo wa maendeleo kwa walengwa hususan wanawake na makundi yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaipongeza Serikali kwa heshima kubwa iliyotupa Wana-Singida kuwa wenyeji wa Sherehe za Wanawake Duniani Kitaifa Mkoani Singida iliyofanyika tarehe 8 Machi, 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sherehe ilikuwa changamoto kubwa kwa wanawake na wananchi kwa ujumla kwani kutokana na maonyesho mbalimbali yaliyoonyeshwa kwa siku hizo, wanawake waliweza kujifunza aina mbalimbali za miradi, waliweza kuuza bidhaa zao na kuweza kujiongezea kipato hata mzunguko wa fedha kwa kipindi hicho ulikuwa mkubwa kwa wafanyabiashara wa Mji wa Singida na wa Mikoa mbalimbali walioshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina wawakilishi hadi ngazi ya Mkoa ambao ni Maafisa Maendeleo ya Jamii wakati Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya wapo chini ya TAMISEMI, hali ambayo inaleta mgongano. Naiomba Serikali iwaunganishe watendaji hawa wawe na mwajiri mmoja na Halmashauri ziwe zinasimamia tu, kwani kwa kufanya hivyo, itafanya Wizara hii kusimamia sera zake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kuwe na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata, ambao watakuwa karibu na walengwa kwa lengo la kutoa elimu ya uzalishaji mali, kuweka kumbukumbu za fedha sahihi na namna ya kubuni miradi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Maafisa Maendeleo wa Jamii, wanahitaji mafunzo ya mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya teknolojia ya kisasa kwani walio wengi wanashindwa hata kutoa elimu kwa wanawake ya uzalishaji mali kwa kutojifunza mbinu za kisasa. Je, nani inawajibika hapa ni TAMISEMI ama Wizara ya Maendeleo ya Jamii mwenye sera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwani imekuwa karibu na wanawake wanaojitahidi kuondokana na umaskini kwa kila mwaka kutoa fungu la kukopesha akina mama kwa mfano, mwaka 2002 kila Halmashauri ilipata shilingi 4,000,000/=, nina imani hata mwaka huu Wizara imeshapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Wizara hii hazitazaa matunda ama zitakuwa ngumu kama wanawake wataendelea kuendesha miradi bila kupewa elimu ya uendeshaji hawataweza kurudisha mikopo. Kwa hiyo, kuna kila sababu kutoa elimu kwa akina mama katika suala zima la uendeshaji vikundi vya uzalishaji mali na namna ya kubuni miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Tanzania, wakiwemo wa Mkoa wa Singida, pamoja na taaluma ndogo waliyokuwa nayo ya uzalishaji mali, wanajitahidi sana kutengeneza bidhaa mbalimbali tatizo ni soko la kuuzia bidhaa zao. Kwa kuwasaidia wanawake hawa, naziomba Wizara za Ushirika na Masoko, Wizara ya Viwanda na Biashara na Nishati na Madini, zishirikiane na Wizara hii ili kuhakikisha bidhaa za wanawake zinapata soko. Mfano, Singida wanawake wanasuka visonzu, wanafinyanga vyungu, wanasuka mikeka, vikapu lakini vipo tu havina soko. Je, Serikali haioni kuwa itakuwa haijamsaidia mwanamke? Wengine wanachimba madini na kupika chumvi hawana vifaa na soko pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza *NGOs* mbalimbali nchini zikiwemo *PRIDE, WEGCC, SEMA, TAMWA, CARITAS* na kadhalika, ambazo zimekuwa mstari wa mbele kuwawezesha wanawake ambao wamekuwa tayari kuondokana na umaskini, zikiwakopesha fedha na kutoa elimu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naziomba *NGOs* hizi zishirikiane na Wizara hii kwa sababu ndiyo yenye sera ambazo zimeainishwa kwa lengo la kumkomboa mwanamke. Vile vile niziombe *NGOs* hizi zipeleke huduma hadi vijijini kwani ndiko waliko wadau wakuu, kama ambavyo inafanya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitachoka kutoa pongezi kwani Wizara imejitahidi sana kukarabati Vyuo vingi vya Maendeleo, pamoja na ufinyu wa Bajeti kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi kilichopo Wilayani Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Wizara hii, bado Vyuo hivi vina upungufu mkubwa wa vifaa mfano vifaa vya vyerehani, ufundi uashi, useremala, fundi chuma, upishi na kompyuta kwani sasa hivi tuko katika teknolojia ya kisasa. Ni imani yangu kuwa wapo wakufunzi ambao tayari wameshachukua mafunzo ya kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tofauti iko wapi Vyuo vya *VETA* vina vifaa lakini Vyuo vya Maendeleo ya Jamii havina vifaa na Serikali ni hii hii au ndio unyanyaswaji wa kijinsia au kwa kuwa Wizara hii inaendeshwa na wanawake? Naomba Serikali iboreshe Vyuo vya Maendeleo ya Jamii haraka iwezekanavyo ili taaluma itolewayo iweze kukidhi haja kwa wanachuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kulipongeza Shirika lisilokuwa la Kiserikali *(AFNET),* kwa juhudi kubwa lililofanya kutokomeza mila potofu za ukeketaji Mkoani Singida. Naiomba Serikali iwe inatoa tuzo kwa mashirika yanayofanya vizuri kama hili la *(AFNET)* na mengine mengi kuwatia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu ambao naamini nitapewa majibu leo hii, nitamke rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii mia kwa mia.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi, kwa kutujaalia uzima na afya njema leo hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi na kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii ninayotoka, maendeleo ambalo ndio lengo la Serikali kuwaletea maendeleo wananchi wake, hivyo Serikali haina budi kupambana na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuendelea kutoa elimu vijijini ili kuweza kudhibiti maambukizo ya virusi vya UKIMWI ili visiongezeke katika jamii kwani waathirika wakiongezeka kutapunguza kazi ya uzalishaji kwani watu wenye nguvu hutoweka. Hivyo, Serikali itilie maanani suala zima la taaluma ya kupima UKIMWI kwa hiari kwa manufaa ya mtu/familia na Taifa kwa jumla. Hivyo, jamii ishauriwe kubadili tabia ya kufanya ngono, vinginevyo tusipobadili tabia, lengo la kupunguza umaskini Tanzania litakuwa ni ndoto tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukeketaji kwa jinsia ya akina mama au wanawake bado linakuwa likiendelezwa kwa kasi kubwa katika makabila mbalimbali Tanzania, ambapo mila, desturi na utamaduni huu wameshindwa kuacha wakiamini wanaboresha afya katika maumbile kumbe ni kinyume chake. Wanayatekeleza haya licha ya sheria iliyowekwa ya kudhibiti kero hii inayohatarisha maisha ya wanawake. Hivyo, Wizara hii iendelee kutoa elimu kwa wanaume na wanawake, kwa kushirikiana na Wizara nyingine, ili kuweza kukomesha kero hii kwa kutumia njia mbalimbali, mikutano ya hadhara, semina, kongamano, warsha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ipatiwe elimu kwa njia nilizozitaja kwa kutolewa mifano hai ya vifo ambavyo vimewapata waliokeketwa. Hili likifanywa jamii itapunguza kama si kuacha kabisa ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tumedhamiria kufuta/kuondoa ujinga, umaskini na maradhi, ninaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwapatia ajira wanafunzi waliomaliza mafunzo kutoka katika kada mbalimbali na kuwaajiri kulingana na fani zao za mafunzo waliyohitimu.

(ii) Serikali ihakikishe inaendelea na ujenzi wa nyumba za kisasa za kudumu zenye mkopo nafuu.

(iii) Serikali iendelee kutoa mikopo mdogo midogo kwa akina mama ili kuweza kujiwezesha na kupambana na umaskini.

(iv) Serikali kwa namna ya pekee ihakikishe inafikisha huduma za maji safi na salama vijijini licha ya Bajeti tegemezi, kwanza wanawake wengi vijijini wanatembea kilomita kadhaa kutafuta maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto lipewe umuhimu mkubwa katika Serikali kwa kuwajengea shule karibu na maeneo wanamoishi ili wasitembee kwa masafa marefu. Sambamba na hilo, Serikali ijenge vituo vya afya ili kupunguza usumbufu wa huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kwa namna ya pekee, ipange mikakati ya kuwatunza watoto yatima ambao hufiwa na wazazi wao kwa ugonjwa wa UKIMWI, kwani imebainika baadhi ya watoto baada ya vifo vya wazazi wao huacha shule na hatimaye kuanza kazi ya ombaomba na kufanya kazi za ajira ngumu kuliko umri wao kwani hutelekezwa na familia zao kutokana na umaskini, hili ni kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kwamba, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uwasilishaji mahiri wa hoja, akiwemo Naibu Waziri na Katibu wao Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara kwa kufanya utafiti wa kuweza kufikia maamuzi ya kuanzisha Benki ya Wanawake. Naipongeza Wizara kwa kukubaliana na mapendekezo ya Shirika la Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Jamii *(ESRF)* kwamba, uko umuhimu mkubwa wa kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* kama msingi wa kuanzisha Benki za Wanawake. Pamoja na wadau kuafiki uanzishwaji wa Benki hizo kupitia *SACCOS,* ninaamini kwamba, haitoshi wanawake kuhamasishwa kuunda Vyama hivyo na kuvimiliki wenyewe. Ushauri wangu ni kwamba, Wizara ifanye makusudi kuhakikisha mwaka huu utaratibu huu unatumika (baada ya Rais kukubali).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara izitambue *SACCOS* ambazo tayari zipo, ichukue baadhi yake ikiwa ni pamoja na Maafisa Maendeleo wa Wilaya zote nchini, wapewe mafunzo ya uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa mahesabu ya *SACCOS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi nchini hasa kule Muleba Kaskazini, wako tayari kuanzisha *SACCOS* lakini hawana utaalam wowote. Hivi sasa *SACCOS* zinaonekana zaidi ziko chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko. Ninapendekeza zoezi hili lisiendelee kuchelewa, nina imani kubwa Mheshimiwa Rais, atakubaliana na mapendekezo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalopenda kuchangia ni tahadhari juu ya UKIMWI, huduma na ushauri wanaopewa waathirika, wajane na watoto yatima wanaoachwa na wazazi waliokufa kwa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii isiyo na afya bora haiwezi kuchangia maendeleo ya jamii, kwa msingi huo UKIMWI ni tishio kubwa la maendeleo ya jamii. Hata hivyo, wanawake wanaopata UKIMWI wakiwa katika ndoa, hupata maisha mabaya kutoka kwa waume zao. Mara nyingi hupoteza mahusiano ya ndoa zao na hata kutalikiwa. Sina kumbukumbu yoyote ya mwanamke aliyeko katika ndoa aliyepata UKIMWI akaendelea kuishi pamoja na mumewe hadi mauti. Wakati huo huo wanaume wapatapo UKIMWI wakiwa na wake zao hao wanawake huvumilia, huwauguza waume zao na kuwapa huduma zote hadi mauti yanapowakuta. Hali hii inaonyesha ubaguzi unaojitokeza kwa watu walio katika ndoa mmojawao afikwapo na gonjwa la UKIMWI. Hapa bado mama hajakumbwa na matatizo ya mirathi ya marehemu mumewe, matusi na kejeli. Nashauri Wizara itafute namna bora ya kuiwezesha jamii kumwona mwanamke sawa na mwanaume kwa lolote katika ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo linalowapata waathirika, wanaugua malaria, mapele, vikohozi/*T.B*. na kadhalika ikiwa ni pamoja na watoto mashuleni na wafanyakazi, wanapata tabu ya huduma. Nashauri nalo hili kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza wajane na watoto wanaotokana na ugonjwa wa UKIMWI, watafutiwe namna nzuri ya kupata huduma. Hawa wanawake wajane wengi huwa pia wameathirika kwa hiyo, wasaidiwe ili waweze kumudu maisha yao. Hivyo basi, wajane wasinyanyaswe kwa namna yoyote na chombo chochote bali wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ushauri wangu uliotangulia upate utekelezaji unaostahiki, hapana budi Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kufanyiwa marekebisho bila kuchelewa. Sheria ya Ndoa imependelea zaidi upande mmoja na kuacha upande wa pili ukiwa unapata hisani. Wanaume wengi wamewatenga wake zao kwa miaka mingi, wameoa na wala hawapeleki hata matunzo kwa familia walizozitelekeza lakini akisikia mwanamke yule kapata mwenzi mwingine, basi kero huanzia hapo na vurugu nyingi. Huu sio usawa! Sheria iweke taratibu zilizo wazi kwa wanandoa ikiwa ni pamoja na haki ya mwanamke aliyetengwa na mumewe au vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa pia ije na mapendekezo mazuri ya mirathi, watoto wanaozaliwa bila wazazi kuwa na ndoa iliyosajiliwa nao watambulike katika mirathi, matunzo na mgawanyo wowote wa mali ulenge hali halisi. Wanawake, wanaume na watoto wote bila kubagua wapate haki zote sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuwatakia kazi njema kwa mwaka ujao, ahsante sana.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa akina mama ni Sera ya Serikali tangu Waziri Anne Makinda. Ni lazima iendelee mwaka hadi mwaka, siyo itolewe halafu iachwe kwa sababu ya ubadhirifu unaofanywa na Wakurugenzi wa Halmashauri husika. Wanawake wa vijijini hurudisha mikopo bila matatizo yoyote na hakuna njia nyingine ya kuwasaidia pasipo Wizara hii. Je, ni Halmashauri ngapi ambazo zimeshindwa kutoa taarifa sahihi ya utoaji wa mikopo na hatua zilizochukuliwa dhidi ya *DEDs* husika? Ni vema Taifa hili kupitia Wizara hii, lihakikishe juu ya upatikanaji wa mikopo. Kenya, Uganda na Afrika Kusini zimefaulu kutambua suala la mikopo ya wanawake hasa wale wanaojishughulisha na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuendeleza Vyuo vya Maendeleo ikiwa ni pamoja na utoaji wa vifaa katika Vyuo hivyo vya ufundi kwani vijana wengi wanaonekana kutopenda kujiunga na Vyuo hivyo kwa sababu ya upungufu wa vitendea kazi, *VETA* wana vifaa tosha.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia japo kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hotuba yake safi na yenye kutia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuzungumzia kuhusu mkopo wa akina mama. Mkopo huu unasaidia sana sasa lakini kutokana na hali ya maisha yalivyo, naomba mkopo huu uzidishwe kutoka Sh.50,000/= hadi Sh.100,000/=, ili waweze kufanya biashara zao bila ya matatizo. Pia mkopo huu uelekezwe zaidi vijijini ili kuwawezesha wanawake kujiajiri wenyewe kwa biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba Waziri, kama alivyotueleza kwenye hotuba yake kuwa Wizara hii ina ushirikiano mzuri na wa karibu na Zanzibar, basi ushirikiano huu uwe wa kweli na kusaidiana kwa hali na mali na hata kukutana kwa mikakati ya kufanikisha zaidi mipango ya kuwawezesha akina mama kibiashara na kuwapa taaluma juu ya mikopo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu UKIMWI, kutokana na maradhi haya, mimi naiomba Serikali iwe na mikakati zaidi ya kinga. Isaidie kikamilifu kutoa *condom* bure kwa sababu kuna baadhi ya vijiji hata hawajui nini *condom*. Kwa hiyo, elimu itolewe na *condom* zitolewe bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAMKUU M. KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake na mimi naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, napenda pia nimpongeze yeye na Naibu wake, kwa vazi la Kihindi waliloonesha juzi kwenye maonesho ya mavazi ya wanawake na zaidi nampongeza yeye Mheshimiwa Waziri, kwa namna alivyomudu vazi lile hasa tukizingatia kuwa yeye si asili yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jumla kitendo kile cha kufanya maonesho yale ni kitendo cha kuigwa na kizazi chetu ili tuweze kuachana kabisa na mavazi ya ajabu ajabu. Kwa hiyo, ningeshauri maonesho ya mavazi kama yale, tuendelee kuyaonesha kila baada ya wakati na hata kama tutatumia wasanii wetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie juu ya 30% ya nafasi au Viti Maalum vya Wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi. Kwanza, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa namna inavyojali mambo ya jinsia. Nashukuru kwa sababu miaka ya nyuma wanawake kupata nafasi za uongozi ilikuwa ngumu si kama tulipo leo. Kwa hiyo, ni lazima tuishukuru Serikali na tuipongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa kuanzia vijijini, Wilayani mpaka Taifa, wanawake tulikuwa hatupati nafasi za uongozi na hata wanawake wenyewe hapo miaka ya nyuma walikuwa hawawezi na hawaamini kuchukua nafasi za uongozi au kuchanganyika na wanaume kutokana na mila potofu tulizokuwanazo za kumfanya mwanamke awe hana hadhi mbele ya mwanaume. Kwa hiyo, iliwapa hadhi wanaume ya kujiona wao ndio viongozi bora na kumwona mwanamke hana sauti na hafai kuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuanzia miaka ya 1975 na kuendelea, Serikali yetu imekuwa ikilishughulikia suala hili la kuwaweka wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi. Kwa mfano, kuanzia mwaka 1980 wanawake walikuwa wakitengewa nafasi maalum katika Bunge na kwa kuwa siku zile ilikuwa ni mfumo wa Chama kimoja, basi nafasi zilitolewa kupitia Jumuiya zetu. Baada ya hapo kila kipindi kukawa kuna ongezeko la asilimia fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, naiomba Serikali iangalie sana suala la kuongeza nafasi maalum za wanawake ifikie 30%. Sasa hivi wakati umefika kabisa wa kuongeza idadi ya wanawake katika Bunge ifikie 30% na pia katika nafasi mbalimbali za uongozi iwe Madiwani Wanawake na wengineo, ili iweze kukidhi haja ya uwakilishi wa wanawake hasa tukizingatia matokeo ya sensa ya hivi karibuni juu ya ongezeko la idadi ya watu. Sasa hivi ndio wakati muafaka wa kuongeza nafasi kwa asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa tunaambiwa kuwa ukumbi ni mdogo, lakini sababu hii si sababu ya msingi hata kidogo, kwa sababu hatukuanza Bunge katika ukumbi huu, tumekuwa tukihamahama kumbi. Kwa hiyo, tusiwanyime haki wanawake kwa sababu ya ukumbi. Tukubali kuwa wakati umefika wa kuwa na 30% ya Viti Maalum kwa kila ngazi za uongozi. Kwa Bunge kama nafasi haitoshi, basi wanawake tuko tayari wengine wasimame au tukae kwa kupishana lakini tupate haki hii ili uwakilishi wa wanawake ulingane na ongezeko la idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kujua juu ya Benki ya wanawake. Napongeza na najua Wizara iko katika harakati za kutaka kufanikisha lakini pia ningeomba kujua harakati hizi zimefikia hatua gani mpaka sasa au kama kuna tatizo, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza wewe, Naibu Waziri na wataalam wako, kwa kazi nzuri mnayofanya kuinua hadhi ya Wizara yetu, hadhi yake ni kuweka utaratibu mzima wa kuweka mipango ya kuwaendeleza wananchi na kujenga umoja wa Wizara, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ningepewa nafasi ya kusema ningefurahi kwani umuhimu wa Wizara yako hauwezi kufumbiwa macho na mtu yeyote mpenda maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, aendelee kukazana kuiomba Serikali iongeze uwezo wa Mfuko wa *WDF* ili wanawake wengi waendelee kuelimishwa zaidi. Kazi mnayofanya kwa kutumia Mfuko huu ni nzuri, inaleta matunda mazuri, kwa hiyo, uendelezwe kwa kuongeza wanafunzi kwa mafunzo ya utaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maadhimisho ya Siku ya Familia, yatiliwe mkazo kwa kushirikisha watu wote hadi vijijini. Elimu ya wakati wa wiki hiyo ni nzuri kwa kujenga raia bora kwani uhamasishaji ukiwa mzuri, watu hujifunza kitu. Kama kauli mbiu ya mwaka huu "Uvivu katika Familia ni Adui wa Maendeleo," maneno ni mazuri yanaelimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uondoaji umaskini katika nchi hii una njia nyingi na *SACCOS* ni njia mojawapo ya msingi. Naomba muitilie mkazo sana kwa watu wa *grassroots* waeleweshwe wajue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, naipongeza Wizara kwa kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Naona bado vinatumika chini ya uwezo wake, Wizara nyingine zinatumiaje Vyuo hivi? Serikali iweke utaratibu wa kuvitumia Vyuo hivyo kwa mafunzo ya wananchi ili wapate elimu ya kuwawezesha kuzalisha chakula kingi, cha kutosha kula na ziada ya kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vipewe jukumu la kuelimisha Walimu wa EWW kwa sababu EWW ni pana iwe chini ya Wizara yako. Wizara ya Elimu na Utamaduni ishughulikie f*ormal education*, EWW mahali pake ni Wizarani kwako. Naiomba Wizara ilione hilo kusaidia EWW. Watumishi wengi wa Wizara yako waelimishwe ili kufanya kazi ya kuandaa watu kwa kazi mbalimbali za kuelimisha wananchi vijijini. Wizara hii ndio sauti ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna unyanyasaji wa aina nyingi wa wanawake. Kutaja kidogo tu:-

(a) Kupiga wanawake;

(b) Kuwaoza wakiwa wadogo kwa waume wasiowataka pengine hata wazee; na

(c) Kutopitisha Sheria ya Mirathi. Dini zisiingilie shughuli za Serikali isiyo na dini ila watu wake. Ndoa ya Wakristo ni mume mmoja na mke mmoja, sasa Mheshimiwa Waziri Wakristo wangapi wana zaidi ya mke mmoja wa agano? Si raia hao? Sheria itungwe ili wanaoitaka waitumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba elimu ya kuwaelimisha jinsia ya wanaume kwanza wajue maana ya jinsia sio wanawake peke yao na waelewe kwamba, uharibifu unaofanywa na mwanamke mmoja sio wa wanawake wote. Mheshimiwa Ngawaiya, aliposema Bungeni wanawake wakipewa madaraka huacha waume zao yalikuwa maneno mabaya mno. Mimi naona alitaka kuonesha unyanyasaji alionao moyoni mwake. Kusema wanawake wasipewe vyeo na wasichaguliwe Ubunge ni hali ya miaka ya zamani sana. Nakuomba uwaandalie semina wenzetu hao wajue kwamba katika maendeleo ya nchi hii, sisi ni wadau sawa kabisa katika nchi. Najua huna fedha za semina lakini omba hata kwa hao Waingereza anaosema wanajuta kuwapa vyeo wanawake ingawa siamini maneno yake basi Wabunge wajue ukweli wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Bajeti ni ndogo lakini tunaiomba Serikali ikuongezee Bajeti kwa 2004/2005 ili Chuo cha Tengeru, kiongeze wanafunzi tupate waragabishi wengi, *training* kwa Wizara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuimarisha Kitengo cha Elimu cha Wizara yako ni muhimu sana. Tengenezeni vijitabu vidogo vifike vijijini kwa sababu kazi ya vielelezo ni muhimu kwa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Wizara fufueni Kitengo cha Ujenzi, kitasaidia kuboresha makazi vijijini ili watu wapate mahali pazuri pa kulala. Kitengo cha Ujenzi ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninawapongeza sana.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo, ninayo machache ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi, kuna haja ya kuhamishia Idara ya Ustawi wa Jamii katika Wizara hii. Ikiwa itafanyika hivyo, suala la jinsia na watoto linaweza likashughulikiwa vizuri zaidi. Wanawake wengi wananyanyasika sana katika ndoa zao. Pia watoto, hasa yatima wanapata matatizo sana. Matatizo yao yanatakiwa yashughulikiwe na Idara ya Ustawi wa Jamii. Kuwepo kwa Idara hii katika Wizara ya Kazi kunaleta uwezekano wa hawa Maafisa Ustawi wa Jamii kukosa mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuachana na sheria na mila tulizorithi kuhusiana na watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Hawa watoto hawakuomba wazaliwe lakini wanapata adhabu badala ya wazazi wao. Sheria inawanyima haki ya kurithi hata pale ambapo wanatambulika. Pia hata kiwango cha Sh.150/= kilichowekwa na *Affiliation Ordinance,* kama ndicho stahili ya mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa kwa mwezi kama matunzo ni cha kushangaza. Kuna haja ya kupitia Sheria hii haraka sana ili kuongeza kiwango hicho na kuwapa watoto hawa haki ya kuwarithi baba zao kama watoto waliozaliwa kwenye ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watoto wa mitaani kwa sasa imeongezeka sana. Hii inaonyesha jinsi hali kifamilia ilivyokuwa na shida mpaka baadhi ya watoto kutoroka nyumbani na tatizo kubwa lililosababishwa na UKIMWI. Hali ya umaskini katika Taifa, inachangia pia kuwepo kwa ongezeko la tatizo hili. Kuna haja, kuiongezea Wizara hii fungu la kujenga asasi/vyuo vya kuwaweka watoto hawa ili waweze kupata yale matunzo muhimu pamoja na elimu muhimu kuwafanya raia wema baadaye. Tusipofanya hivyo, tunalea majambazi na watumiaji madawa ya kulevya wa kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinashughulika na kumwendeleza mtoto baada ya Darasa la Saba na pia Vyuo vya *VETA* vinafanya kazi kama hiyo. Hakuna Vyuo vya namna hiyo ambavyo vinamlenga huyu mtoto wa mitaani au yatima ambaye hana msaada wowote. Ninashauri Wizara ipewe jukumu hilo na nina uhakika kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, hili tatizo la watoto wa mitaani litapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili tatizo, wako pia wale watoto ambao badala ya kuzurura, wanaingia katika kazi ambazo ni za kuwadhalilisha na kuwaumiza. Si jambo la ajabu siku hizi kuona watoto wa mpaka miaka 11 wanafanya kazi ya ukahaba na wamewekwa kwenye madanguro. Pia, watoto wanaajiriwa katika kazi ngumu na hatari kwenye mashamba na majumbani. Wale wanaoajiriwa kwa kazi za majumbani wanateswa kwa kufanya kazi kwa saa nyingi sana kuanzia alfajiri mpaka kuibua usiku chakula. Kuna haja ya Wizara kufuatilia hili suala la ajira kwa watoto. Haitoshi Wizara ya kazi yenyewe kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi matukio ya talaka yameongezeka. Wanawake wanateseka sana baada ya talaka kwa sababu ya sheria zilizoko. Iko haja ya kurekebisha Sheria za Ndoa na Talaka ili kuhakikisha kuwa, mwanamke anayepewa talaka analindwa ipasavyo. Hii itaepusha wanaume kuwatumia vibaya wanawake na baadaye kuwaweka njia panda. Pia kuna haja ya kuongeza juhudi za Serikali katika kuwawezesha wanawake. Wakiweza kujitegemea kiuchumi, basi hata heshima yako ndani ya ndoa itakuwa

kubwa na unyanyasaji wa wanawake utapungua. Hili fungu la kuwawezesha wanawake liongezwe kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wanawake ambao tayari wanajishughulisha na biashara ndogo ndogo za usindikaji wa vyakula. Ninaishauri Wizara ishirikiane na *SIDO,* wanawake hawa wapate misaada ya kiutaalam, kutafutiwa masoko na mitaji. Huenda ikawa kwa kufanya hivyo, tunaweza kutatua pia tatizo la kuharibika kwa vyakula na matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto wengi kiasi, ambao wamefungiwa katika Magereza ya kawaida. Watoto hawa wanachanganywa na wahalifu waliokubuhu na wanafanyiwa vitendo vibaya sana huko jela. Wanajifunza tabia mbaya huko na wanapotoka wanakuwa wamejifunza mbinu za kutenda uhalifu kwa ufanisi zaidi badala ya kuwa wamerekebishwa. Wanatoka wakiwa na kinyongo dhidi ya jumuiya kwa hiyo, wanakuwa wanajumuiya wabaya zaidi. Ninashauri Wizara iingilie kati. Sheria ya *Children and Young Persons Ordinance* irekebishwe ili kuwalinda hawa watoto zaidi. Kuwe na ushirikiano kati ya Wizara hii, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Kazi, Vijana na Michezo, kuhakikisha kuwa watoto wahalifu wanapata adhabu katika mazingira ya kuwafanya wajirekebishe na sio wawe wahalifu mahiri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Naibu wake Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu, Mama Mary Mushi, pamoja na Maafisa wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwa kushirikisha Wizara ya Wanawake na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kutoa mafunzo ya stadi mbalimbali kwa Wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwa yafuatayo: -

(a) Juhudi inayofanya kwa kukomesha ukeketaji nchini;

(b) Kuanza utaratibu wa kuanzisha Benki ya Wanawake; na

(c) Kuendesha semina na mafunzo mbalimbali kuhusu masuala ya UKIMWI na kuhakikisha kwamba, zinaa (ngono nje ya ndoa) zinapigwa vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara imeomba fedha ambazo ni kidogo kwa kazi ambayo inatakiwa ifanye. Ninawapa pole Mawaziri na kuomba Hazina mwakani kuwazidishia ili wajisikie na kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *money is power* na *power* tukiwapa wanawake, basi watatusaidia sana. Wanaume hatukamiliki bila ya wanawake: *"Behind every successful man there is a woman".* Ni wajibu wetu tuwathamini na kuwaheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Shamim Khan, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Bibi Mary Mushi, Wakurugenzi na wataalam wote wa Wizara, kwa hotuba iliyoandaliwa vizuri na kueleweka kutokana na mpangilio wa maudhui yake, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, mchango wangu utajikita katika kutoa ushauri na kuomba kupata ufafanuzi wa hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuupongeza Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, unaoongozwa na Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, kwa kazi nzuri ya kuhamasisha Wanawake kuboresha bidhaa zao kupitia semina mbalimbali wakati wa Maonyesho ya Saba Saba Dar es Salaam, kwa vile akina mama toka Mikoa mbalimbali kupitia vikundi vya kiuchumi huweza kuonyesha na kuuza bidhaa zao kwa ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Biashara na Viwanda.

Pamoja na kazi hii nzuri, imejitokeza hali ya washiriki kuwa ni sura zile zile zinazokuja kushiriki katika maonyesho hayo. Hivyo, nashauri kuwa, utaratibu uwekwe wa kupata washiriki tofauti tofauti ili elimu na *experience* inayopatikana isihodhiwe na wanawake wanavikundi wachache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu mikopo toka Mfuko wa Wanawake, ambao huchangiwa kwa ubia kati ya Halmashauri na Wizara. Pamoja na kwamba, utaratibu mpya wa ukopeshaji ulioanza mwaka huu wa 2003, baada ya kusimamishwa kwa muda, ni mzuri sana kwa vile walengwa kupatiwa mafunzo kwanza. Lakini tatizo ni kwamba, bado Halmashauri nyingi hazichangii kikamilifu kwa visingizio mbalimbali na kusababisha mtaji kuwa mdogo hivyo kutosheleza kwa vikundi vichache tu. Kwa msingi huo, nakubaliana na ushauri wa Kamati kuwa Wizara ikishirikiana kwa karibu sana na TAMISEMI, ihimize Halmashauri zote kutimiza wajibu huo kwani mikopo hii ni njia mojawapo ya kuwapunguzia wanawake umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuwa Halmashauri zingine wala haziwaeleweshi wanawake vya kutosha kuhusu Mfuko huu kiasi kwamba, kuna uwezekano wa fedha hizo kutumika vibaya kinyume cha malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Wizara kwa kuzingatia ushauri wangu nilipouliza swali kuhusu mikopo kwa wanawake wenye ulemavu nchini Januari, 2002 humu Bungeni. Natumaini Wizara ilijitahidi kuweka utaratibu wa jinsi ya kuhamasisha wanawake walemavu kuunda vikundi ili waweze kukopeshwa katika Halmashauri zetu. Kwa msingi huo, nazipongeza Halmashauri ambazo zimetekeleza ushauri huo wa kukopesha vikundi vya wanawake vyenye ulemavu kwa mfano Halmashauri za Mtwara Vijijini, Newala, Kahama, Morogoro Manispaa na nyingine zote ambazo nitaomba Wizara itoe orodha yake hapo baadaye. Ombi langu ni kwamba, utaratibu huu au jitihada hizi zifanyike katika Halmashauri zote kwa sababu wanawake wenye ulemavu nao wanastahili kuwezeshwa kwa vile wengi wao ndio waliozungukwa na umaskini uliokithiri. Hivyo, mikopo hii itawasaidia kupunguza matatizo yanayowakumba kwa vile aina nyingine za mikopo hawawezi kukopa kutokana na masharti magumu yanayoambatana na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jina la Wizara sasa lina *element* ya wazi kabisa ya jinsia, ninawashauri kuwa katika suala la mikopo kutoka Mfuko wa Wanawake sasa hata vikundi vya wanaume maskini/fukara nao wakopeshwe ili nao waweze kujikwamua na umaskini walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa juhudi inazofanya katika kuhakikisha kuwa chombo cha Wanawake kinaundwa nchini bila kujali itikadi za wanawake hao. Hata hivyo, ninashauri kuwa, Kamati Teule iliyoundwa iwezeshwe kikamilifu na katika Tume itakayoundwa uwakilishi wa wanawake wenye ulemavu usisahauliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ilielezwa mwaka 2002 kuwa Sheria mbalimbali zinazohusu masuala ya wanawake na watoto zinafanyiwa mapitio kwa lengo la kurekebishwa, basi kasi ya mapitio hayo iongezwe ili ziletwe Bungeni kwani watoto na wanawake wanaendelea kuathirika kwa matumizi ya sheria zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, nawatakia wahusika wote utekelezaji mwema wa majukumu waliyojiwekea na naunga mkono hoja.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia japo kwa maandishi kuhusu Bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu ya 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninampongeza sana sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri mno, aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri kwa paragraph ya 25 ya hotuba yake kuhusu kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Benki ya Akiba na Mikopo *(SACCOS).* Vyama vya Ushirika *(SACCOS)* viko chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko, ambayo ndiyo yenye Mrajisi wa Taifa na katika Mikoa kuna Warajisi Wasaidizi. Kila Chama cha Benki ya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* kina *signatories* wake na Halmashauri ya *SACCOS.* Baada ya Wanachama kuweka fedha zao kwenye Benki hiyo, *signatories* wamekuwa na uwezo wa kuchukua fedha hizo *(withdrawing)* zaidi ya Sh.50,000/= bila kuitisha Halmashauri kupitisha hilo, matokeo yake *signatories* hawa wamefilisi Benki hizo za *SACCOS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *International Auditors (COASCO)* na *External Auditors* wanapogundua wizi huo hawachukui hatua yoyote ambapo ingekuwa Mrajisi kuwapelekea *surcharge* kufikishwa Mahakamani kufilisiwa, fedha kurudishwa *SACCOS* husika na hatimaye kufungwa kifungo stahili. Mrajisi kwa kuwalinda *signatories* hawa hachukui hatua yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo halifanyiki hata ukilia kwa Waziri, Mrajisi na Mamlaka yoyote ile hakuna hatua yoyote inayochukuliwa, viongozi hao wanasema ni juu ya waathirika kuwapeleka *signatories* hao Mahakamani huku wakijua kwamba, waathirika hawajui sheria. Akina mama wasaidiwe na Waziri kwa kila palipo na *NMB,* ndani pawe na dirisha litakaloandiwa *"Wanawake SACCOS"*, nasema kweli yamenipata, majuto ni mjukuu. Nimeshamfikishia hata Rais suala hili na hakuna hatua iliyochukuliwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chisalu kitafanyiwa ukarabati mkubwa, naishukuru sana Serikali. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Hivi sasa Chuo kinatumia umeme wa jenereta ambao ni gharama kubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvuta umeme wa Gridi ya Taifa, huo ndiyo umeme wa uhakika kutoka Mpwapwa Mjini kilomita 25. Gari ni bovu, kwa hiyo, linahitaji fedha za ukarabati pamoja na trekta ili liweze kufanya kazi ya kilimo na wanaweza kujitegemea kwa chakula kama litalimwa lote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeridhia Azimio la Beijing, ambalo linaitaka Serikali kutoa nafasi za kushirikisha wanawake katika ngazi zote za uamuzi. Serikali ya CCM imelitekeleza ila haijafikia asilimia thelathini ambayo imekubalika na *Beijing Declaration.*

Wabunge Wanawake wakifikia asilimia thelathini wataongeza changamoto kwa Wabunge maana hata michango yao ni makini. Hata hivyo, Tanzania inahitaji wanawake zaidi kwenye vyombo vya uamuzi kwa sababu idadi ni asilimia 51. Nashauri azimio tuliloridhia litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate asilimia thelathini kwenye ngazi zote za Wizara, Idara, Taasisi, Asasi na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake itaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupate mafunzo ya jinsia ili wanawake tuweze kuelewa kupangana kwenye nafasi za juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo, naomba mafunzo yatolewe kwa wanawake kuhusu haki zao za kuweza kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa ushirikiano mzuri.

**MHE. ESTHER NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wetu mpendwa, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Naibu Waziri mpendwa, Mheshimiwa Shamim Khan, kwa kazi nzuri wanazofanya kwa ajili ya kusimamia Wizara nyeti ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Wizara hii Serikali ikiiwezesha vizuri kifedha, umaskini, UKIMWI, unyanyasaji na ujinga, vitakwisha vyote. Hili naliweka hivi, sababu Watanzania wengi ni maskini, hawana maendeleo na hawana elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo yanaletwa kama mwanamke atawezeshwa kimkopo na mafunzo mbalimbali ataweza kuondoa umaskini kwa kuendesha biashara, atahakikisha watoto wanasoma kwa gharama yoyote.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kutoa kiasi cha shilingi 4,000,000/= kwa kila Wilaya. Nikiwa Mbunge wa Viti Maalum nitazifuatilia nihakikishe zimewafikia wanawake hadi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwepo uwiano wa kutoa maamuzi sawa, bado tunaomba Waziri amwombe Rais wetu aongeze asilimia ya Viti Maalum kwa Wabunge ifikie asilimia thelathini kabla ya mwaka 2005. Inapendeza kama wanawake wengi nao watashirikishwa katika maamuzi ya uongozi na kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuona haja ya kupandisha vyuo vingine kutoa Stashahada kwa Vyuo vyetu vya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa kuwa karibu sana na *MPs* Wanawake, tunashukuru kwa kututeua kuwa wajumbe katika Bodi za Vyuo vyetu, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana niwaombe viongozi wetu hususan Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, waendelee na moyo huu kwa kuwa karibu nasi, nawatakiwa kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono asilimia mia na waongezwe fedha kwani hizi hazitoshi, naomba Wizara hii ipewe fedha nyingi zaidi.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema wa malengo mliyojiwekea kwa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2003/2004. Mola awabariki na awajaalie afya njema watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hii sikuona fedha zilizotengwa kwa ajili ya Chuo cha Bahangija. Chuo kimeharibika sana na hakijapata matengenezo yoyote. Pamoja na kwamba, nimeona mwaka 2002 mlitenga shilingi milioni nne lakini mimi sijaona kama matengenezo hayo yalifanyika labda matengenezo yamefanyika mwezi wa Sita. Naomba sana Wizara itusaidie kutupatia fedha za matengenezo kama inavyofanya kwenye vyuo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba, wenye lishe duni wakiugua UKIMWI, hufa haraka sana kwa sababu hiyo ya lishe duni, naomba Serikali pia isaidie upatikanaji wa lishe kwa

walioathirika. Wataalam wanasema wadudu wa UKIMWI na aina ya UKIMWI hapa Afrika ni tofauti na wadudu wa UKIMWI na aina ya UKIMWI uliopo Ulaya. Je, dawa zinazofanyiwa utafiti Ulaya zitawasaidiaje Waafrika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro na Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu, Bibi Mary Mushi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inapongezwa sana kwa utendaji wake mzuri hasa kwa kusimamia tabia mbaya ya jamii kama vile ukeketaji ambalo ni tatizo kwa jamii. Haya ni mambo ambayo Wizara imekuwa mstari wa mbele kuyaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatakiwa itoe kipaumbele kwa mambo muhimu ya jadi na kutokubali mila potofu. Hii inatakiwa ili ijenge maadili kama yale yanayofundishwa kwenye jando na unyago. Lakini kwa kuangalia hali bora ya mila zetu sasa hivi, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aanze kushughulikia suala la mirathi kwa wanawake ili kuwepo usawa kati ya wanaume na wanawake hasa wanawake (wafiwa) ambao wao ndiyo wanatunza watoto na familia hasa pale baba anapokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuangalia upya Sheria za Mirathi. Hili nitapenda Mheshimiwa Waziri, atoe maelezo atakavyofuatilia suala hili kwani bado limekuwa ni tatizo kubwa kidogo kwa wananchi wa kipato cha chini na juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anatakiwa pia aangalie zile sheria za kudhalilisha wanawake. Kwa mfano, msichana wa sekondari au shule ya msingi anapopata mimba anafukuzwa shule na mwanaume hafukuzwi na ipo sheria au tamko la kumtia aibu mwenye mtoto kwa kupewa shilingi 10/=, naona hili ni suala la zamani sana. Naona sasa wakati umefika wa kurekebisha sheria hizi ili ziendane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kuadhibiwa basi inatakiwa wote wangepata adhabu kuliko kupewa wachache. Kwa hiyo, bado Wizara inapaswa kuangalia hali ya sasa hivi kwani siyo kama ile ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati umefika wa Wizara kuanzisha *centres* za makazi ya watoto yatima kwa kuzijenga na kuwapangisha wale wananchi wanaopenda kuziendesha. Pia *centres* hizo ziwe ndipo penye mikakati ya kuangalia matatizo mbalimbali ya jamii kama vile UKIMWI na kadhalika. Fedha nyingi zinazoshughulikia masuala ya UKIMWI zinapotea pasipo kuwepo *centres* hizi. Ni vema Wizara iangalie kuwepo kwa makazi hayo, vituo vya kulelea watoto wasio na makazi ni jukumu la jamii, lakini kama nilivyosema, inahitaji Serikali ijue bado ina kazi ya kusaidia kujenga *centres* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu na tatizo sugu la maradhi ya UKIMWI kwani sasa hivi wataalam wanatuambia kuwa wanandoa ndiyo wanaoathirika kwa wingi. Mimi nakubaliana na watafiti hao, kwani kuna wanawake wajane wengi ambao wana hali duni sana, wanapofiwa na waume zao hujikuta wanaathirika kisaikolojia kwani hupata tabu sana katika kufuatilia urithi, kuna mlolongo mrefu wa kufuatilia urithi na ndio wengine hukata tamaa na kujikuta wanachanganyikiwa na kuanza kufanya vitendo vya ngono bila kujali kuwa wanaeneza UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri Serikali itenge fungu la fedha kwa ajili ya kuwakopesha wajane hawa kupitia Wizarani na mkopo huo uwe na riba nafuu ili wajane hawa na watoto waweze kuishi kwa matumaini na maendeleo ya kukuza na kuendeleza watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie upya sheria hii ya mirathi kwani inamkatisha tamaa mwanamke kufuatilia kwa milolongo wa sheria hii ilivyo mirefu na mbaya zaidi mwanamke anapopandishwa kizimbani kama mhalifu mwingine wa kosa la jinai, hii kwa mwanamke huona kama ni unyanyasaji. Kwa hiyo, ndiyo maana wanawake wengi wanashindwa kudai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pale inapotokea misaada ya UKIMWI basi iwafikie wanawake wote wa Mijini na Vijijini kwani kuna wanawake wengi walioathirika na hawapati misaada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Mheshimiwa Dk. Asha-Rose Migiro, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyofanya katika mwaka 2003/2004. Bila shaka wataongeza jitihada katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba Wizara izingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji wa vyuo. Serikali iongeze fedha za Bajeti ya Vyuo ili viweze kutekeleza majukumu ya kuwaendeleza vijana na kupambana na umaskini. Wahitimu wa Vyuo hivi hawahangaiki kupata ajira kwani mara baada ya kumaliza vyuoni hapo Jumuiya huwaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuelekea zaidi Vijijini kuliko Mijini. Walengwa wa Wizara hii siyo watu wa Mijini tu kama hali ilivyo hivi sasa, bali wale walioko Vijijini kwani hao ni wengi zaidi. Mikopo mingi inatolewa kwa wakazi wa Mijini na ni mikopo michache tu inapelekwa Vijijini. Shughuli za Wizara hii zipanuliwe na kuenezwa toka Mijini kuelekea Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile kuzungumzia kuhusu mikopo kwa wanaume na wazee. Serikali huwalenga akina mama na vijana tu lakini wanaume au wazee hawaongelewi katika kupewa mikopo ingawa nao ni sehemu ya jamii tena wale ambao wamelitumikia Taifa hili muda mrefu. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuwa na sera ya namna ya kuwahudumia wanaume au wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imetolewa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naipongeza Wizara hii kwa utendaji wa hali ya juu na wenye ufanisi mkubwa, ambao umeanza kujitokeza kwa kasi kubwa hasa katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kuikumbushia Wizara ili iweze kutoa mikopo zaidi kwa akina mama waishio katika Jimbo la Siha ambao kama Waziri na Naibu wake wajuavyo wameonyesha ari kubwa katika kuunda vikundi mbalimbali ili wajiletee maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata nafasi hii kuchangia hoja iliyokuwepo mezani hivi sasa. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wake Wakuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia maendeleo ya wanawake na watoto. Aidha, ninawapongeza pia kwa kuandaa Bajeti nzuri yenye mwelekeo wa kumkomboa mwanamke na mtoto wa nchi hii.

Mchango wangu kwa leo nitauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, unyanyasaji wa wanawake na waume zao. Mbali na jitihada zinazofanywa na Serikali na *NGOs* mbalimbali, bado wanaume wanawanyanyasa na kuwaonea wake zao kwa kuwatukana matusi ya nguoni na kuwapiga viboko, mateke, magumi, wakielewa kuwa akina mama hawana uwezo na nguvu za kujihami. Imekuwa ni kitu cha kawaida hapa nchini kwetu kusikia kuwa mwanamke ameuliwa na mumewe kwa tuhuma tu za uzinifu, wengine humwagiwa maji ya moto sehemu za siri na wengine kukatwa au kumenywa kabisa sehemu za siri kwa tuhuma hizo hizo ambazo mara nyingi zinakuwa hazina ukweli wowote. Hapo ni suala la kujiuliza hawa wanaume wanaofanya hivi wamepata wapi ujasiri wa maamuzi yao, je, ni mila au utaratibu mbaya wa kushughulikia kesi kama hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai wa mke aliyeteswa na mumewe, kupigwa hadi kung'oka meno yote na kubakia kibogoyo. Nilipomwuliza baada ya matukio hayo ya kudundwa kama pweza, alichukua hatua gani? Alisema alikwenda kushtaki kwa wazee wake ambao walimtaka aendelee tu kuishi na mumewe kwa sababu watoto watapata taabu. Kwa vile mama yule alikuwa hana ajira na hajui namna gani ataweza kuishi kwa kujitegemea ingawa alikuwa na uwezo wa kulima na kufanya biashara ndogo ndogo na hata kubwa kwani alikuwa na elimu ya kidato cha tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanaopata mateso haya mara nyingi kesi zao wanazipeleka kwa viongozi wa kijamii au vijiji ambao wengi wao ni wanaume na kesi hazishughulikiwi ipasavyo. Mfano kule Zanzibar, viongozi wa jamii ni Masheha na takribani asilimia 97 ni wanaume, hivyo kesi zinababaishwa ili wawanusuru wanaume wenzao au kwa nia ya kuilinda ndoa isivunjike.

Ushauri wangu ni kuwa Serikali iangalie na kuandaa utaratibu bora wa kushughulikia jambo hili ili haki itendeke. Aidha, suala la elimu liendelezwe kwa nguvu zote ili wanaume wajue na wabadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili biashara ya ngono inafanyika katika madanguro ambayo yanamilikiwa mara nyingi na wanawake watu wazima na akili zao, ambao wanatumia watoto wadogo wa kike wa miaka 12 hadi 15. Huu ni uonevu na uvunjaji wa sheria, watoto hawa hawajui hata namna ya kujikinga na maradhi ya ngono ukiwemo UKIMWI. Adhabu kali itolewe ili mambo haya yakomeshwe kabisa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya ngono za kujitembeza barabarani na kwenye majumba ya starehe, mambo haya hayamo kabisa katika mila zetu za Kitanzania na ninaamini tunaweza kupambana nayo. Hapa nina mfano hai, mfanyabiashara ya ngono mmoja nilimsikia akilalamika na kulia alfajiri moja alipokuwa akirudi kazini ninamnukuu maneno aliyoyasema: "Baba yangu amenifukuza nyumbani, mama yangu simjui hata alipo, walimwengu hawanikubali na wananidharau kutokana na biashara ya kuuza mwili wangu na hata kile nilichokichuma usiku wa jana wenzangu wameniibia nitaishi vipi mimi"?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilimhurumia na kuona kuwa kwa kuandaa mkakati wa makusudi wa Serikali, watu kama hawa wanaweza kubadilika. Ni kuwapatia ushauri nasaha na kuwaelimisha njia nyingine za kupatia kipato na kumpatia nyenzo, ninaamini kwa asilimia kubwa wataachana na suala la kuuza miili yao.

Tatu, asilimia 30 ya wanawake kuwa katika nafasi za uongozi, katika hili naiomba Wizara isimamie ipasavyo ili litekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wake, kwa hotuba nzuri na mikakati bora yenye lengo la kuiboresha Wizara hii na kuboresha hali ya mwanamke na mtoto wa Tanzania. Ningependa sasa kutoa ushauri ufuatao kwa Wizara hii:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza utekelezaji wa Sheria ya Kupinga Ajira kwa Watoto. Sheria husika imekwishapitishwa na Bunge na kukubaliwa rasmi na Mheshimiwa Rais na hivyo inapaswa kutumika kikamilifu. Hata hivyo, sheria bado ni mpya na katika maeneo mengi bado haijaanza kutumika. Bado watoto wengi wanaajiriwa katika mashamba ya chai, biashara za bidhaa za kilimo ikiwa ni pamoja na kuchuma machungwa na matunda, ajira za majumbani ndani na nje ya nchi na kadhalika. Ni wajibu wa Wizara kuona sheria hii inatumika. Hivyo basi, ipeleke nakala moja ya sheria yenyewe kwa Wakuu wa Wilaya na kuagiza Serikali ngazi ya Wilaya, ikiwemo Idara ya Polisi, kuwasaka na kuwafikisha Mahakamani wote wanaojihusisha na ajira ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa sheria hii ukiachwa kutegemea viongozi wa Serikali za Vijiji kuwashtaki wale wanaoajiri watoto, haitakuwa vema kwa sababu baadhi ya watoto ni wa viongozi wao na wao wanashabikia kipato kidogo wanachopata watoto hao huku wao kama wazazi, wakikwepa majukumu ya kuwasomesha watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Halmashauri nyingi hazichangii katika mifuko ya maendeleo ya wanawake na vijana, hivyo lengo la Wizara kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana linadumazwa. Wizara lazima ibuni mbinu za kisheria zitakazobana Halmashauri zote kuwajibika katika utekelezaji wa mpango wa Serikali katika kutenga fedha kutokana na mapato ili kuunga mkono uboreshaji wa mifuko hii inayolenga kuinua maendeleo ya wanawake na watoto. Wizara lazima itambue kwamba, kushindwa kutekelezwa kwa mpango ambao ni sehemu ya sera ya Wizara, ni sawa na kushindwa kwa sera yenyewe na hivyo Wizara isitarajie kufikia lengo la kiwango cha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu na mwisho, Wizara isaidie vikundi vya wanawake na vijana kuviandikia michanganuo ya miradi wanayobuni wenyewe ili waweze kupata mikopo na kuitumia mikopo hiyo kwa mpango sahihi na utakaowawezesha kupata faida na kulipa madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli wapo Maofisa wa Ustawi wa Jamii ndani ya Halmashauri nyingi, lakini kwa kiwango kikubwa maofisa hao wameshindwa kuwasaidia wananchi katika kuandaa miradi na kuandika michanganuo. Wizara inapaswa kulizingatia hili na kuwa na Maafisa wake watakaosaidia kuongoza utekelezaji wa mpango huu ikiwa ni pamoja na kuwavuta na kuwahamasisha Viongozi wa Halmashauri, Idara ya Ustawi wa Jamii kutoa mchango wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JINA KHATIB HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kuipata nafasi ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ninalolichangia ni kuhusu unyanyaswaji wa watoto. Ninaomba Wizara ichukue bidii ya makusudi kuwaelimisha wanawake wenzetu. Taaluma niisemayo ni kwa wanawake wanaoajiri wafanyakazi wa majumbani. Baadhi ya wanawake wanaowaajiri wafanyakazi wa majumbani wanawanyanyasa sana. Mayanyaso makubwa ya watu hawa ni kama haya yafuatayo: Kupigwa na waajiri wao, kutukanwa matusi makubwa. Maoni yangu, ningeshauri Wizara hii ikafungua kitengo kidogo cha kusikiliza matatizo kama hayo. Mara nyingi matatizo yanapopelekwa Polisi, hatua inayochukuliwa inakuwa ni nyepesi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ahsante sana.

**MHE. OMAR JUMA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunatambua kwamba, wanawake ndiyo tegemeo kubwa la Taifa kwani bila ya wanawake Taifa haliwezi kutoa viongozi wazuri, wataalamu na washauri wazuri wa Serikali, kwa hiyo, bila ya kuwatunza basi na kuwapatia pembejeo tutafika mahali pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada ambayo hupatiwa wanawake haiwezi kukidhi haja yoyote, ipo haja ya kupewa mikopo mikubwa yenye kukidhi haja kwani mkopo wa biashara ya maandazi hauwezi kumwendeleza mwanamke kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malezi vile vile yanachangia kuleta ama familia kuwa nzuri au mbaya ikiwa malezi hayo hayafanani na malezi ambayo tumerithi kutoka kwa wazazi wetu au malezi ya kimila kwani tukifuata malezi ya Kizungu, malezi hayo yanaleta matatizo kwa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Gonjwa la UKIMWI, taasisi nyingi zinahamasisha kuhusu ugonjwa huo, lakini kuhamasisha siyo suluhisho la kuondoa hilo gonjwa bali dawa pekee ya UKIMWI ni kujizuia na uasherati au uzinifu tu wala siyo kuhamasisha utumiaji wa kondomu kwani kondomu ni biashara za wajanja tu watu waathirike na UKIMWI, yeye anapata pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umaskini uliokithiri hapa nchini, ndiyo kitu pekee ambacho husababisha vijana wengi kukimbilia Mijini kwa ajili ya kutafuta kazi. Kwa hiyo, hurundikana katika Miji bila ya kupata kazi na ndiyo huamua kujiingiza katika vitendo vya kihuni kama kuvuta bangi, unga au madawa ya kulevya, kwa wanawake na wanaume. Vile vile wanawake hujiingiza katika biashara mbovu ya ukahaba na uasherati kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za watoto bado ni nyingi katika Miji, kwa hiyo, waajiri huwaajiri watoto hao kwa sababu watoto hao huwa hawana mawazo ya kudai mishahara kulingana na kazi zao bali kupata kula yao na hivyo kula ndiyo malipo yao tu.

Vile vile wanawake ambao hutoka Vijijini kwa ajili ya kwenda Mijini kutafuta kazi, huajiriwa na waajiri ambao imani zao ni ndogo na kuwapa mishahara midogo ambayo hailingani na kazi ambazo wasichana hao hufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto yatima, hupata taabu sana hasa ukilinganisha kwamba wasimamizi wa maisha yao wameshatoweka.

Kwa hiyo, huishi katika maisha ya kubahatisha tu na wengi huishia katika maisha ya ombaomba na hatimaye kuwa wahuni, wezi na waporaji na wengine hupoteza maisha kwa vitendo vya uporaji.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ili nami nitoe mawazo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa ushirikiano waliouonyesha na kuleta taarifa/hotuba hii nzuri. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyofanyika mwaka 2002/2003 ukweli inaonekana na inapunguza kelele toka kwa jamii. Hii ni kutokana na utendaji ulio ndani ya Wizara hii hasa katika mgao wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF),* pesa ilitolewa bila upendeleo. Hii ni picha inayopaswa Wizara nyingine ziige mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kazi nzuri inapunguza maswali mfano mwingine ni eneo la Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa mgao mzuri kwa vyuo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla ni kuona Chuo cha Misungwi kinaimarishwa ili kitoe elimu nzuri. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 28 - 29 aya ya 48. Kulipatia ufumbuzi tatizo lao la kubadilisha Programu ya Mafunzo toka Cheti cha Kawaida kwenda Cheti cha Ufundi *(FTC).* Naipongeza sana Wizara.

Hotuba ya Wizara hii imejibu hoja za wananchi wa Misungwi hivyo naomba sana Mheshimiwa Waziri akipata nafasi katika ziara zake za kukagua shughuli zihusuzo Wizara yake, namkaribisha Wilayani Misungwi ili aje aone maendeleo ya wananchi wa Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na namtakia Mheshimiwa Waziri kazi njema.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim P. Khan, Katibu Mkuu na Maafisa wa Wizara hii kwa kazi nzuri za Wizara. Tulikuwa pamoja katika Kamati ya Bunge katika muda wa miaka sita (6) mfululizo. Ninafahamu juhudi zenu, matatizo ya kijamii nchini. Karibuni sana Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo. Wizara inashauriwa kutoa fedha ili kukarabati Vyuo hivi kwa sababu ni vichakavu sana. Tunaomba Wizara izingatie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitengo vya Jinsia Wizara Nyeti. Kuwe na Idara ya Jinsia katika maeneo ya Wizara za Afya, Ulinzi, Viwanda, Fedha, Mipango*, PMO,* Ofisi ya Rais, Mambo ya Ndani na Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Asilimia Kumi kutoka Halmashauri. Iundwe timu maalum toka Wizarani kufuatilia Wizara au Halmashauri ambazo hazitoi asilimia 10 ili zichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo wa Kamati ya Mikopo ya Wilaya. Madiwani wanalalamikia muundo wa Kamati ya Wajumbe kwamba ishirikishe Madiwani wanawake, hawamo. Wanaomba Wajumbe waongezwe.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Hotuba imewasilishwa kwa ufasaha na maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa hongera kwa Tamasha la Wanawake la tarehe 26 Julai, 2003 usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa Serikali kwa kutenga fedha za ukarabati wa Vyuo vya Mafunzo hususan Chuo cha Mabughai Lushoto. Naomba suala la madeni ya chuo hicho lichukuliwe hatua ya kulipwa. Ikiwa deni la umeme na kadhalika halitalipwa itakuwa kazi bure kukarabati chuo wakati umeme hautarejeshwa. Naomba Wizara itoe kauli juu ya suala la madeni sugu ya Vyuo vya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya akina mama (wanawake) hususan wale wa Vijijini lipewe kipaumbele. Utaratibu mzuri wa utoaji mikopo hiyo ubuniwe. Utaratibu wa sasa haufai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umaskini hususan kwa wanawake ni budi liangaliwe kwa undani. Vitendo vya kunyanyaswa wanawake zaidi husababishwa na umaskini. Wasichana wengi wamejiingiza katika matendo ya kufedheheshwa kutokana na hali duni ya maisha. Huko Vijijini maisha ni magumu sana umaskini umekithiri. Nashauri kwa dhati kabisa jitihada za makusudi zichukuliwe katika kumkomboa mwanamke kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Mikopo yenye masharti nafuu sana isambazwe Vijijini.
(b) Elimu ya biashara, kilimo na kadhalika ipewe umuhimu sana kwa wanawake.
(c) Iundwe Benki ya Wanawake kuratibu mikopo na elimu kwa wanawake.
(d) Kiasi kilichotengwa na Serikali kwa mikopo ya wanawake kiongezwe maradufu. Elimu ya kurejesha mikopo hii itolewe kwa kina.
(e) Makongamano na semina yapunguzwe ili fedha ziende Vijijini.

**MHE. MWANAIDI HASSAN MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wataalam wote kwa kuandaa hotuba hii ambayo ni nzuri na inayoeleza mambo mengi kwa kina na ufafanuzi unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara kuangalia uwezekano wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuandikishwa na *VETA* ili vyeti vyake viweze kutambulika. Hii itasaidia kuondosha usumbufu wanaoupata wahitimu wa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuyafanyia ukarabati majengo ya Vyuo vya Maendeleo nchini ni muhimu sana. Kwa hivyo, Wizara ipange utaratibu wa kulishughulikia suala hilo awamu kwa awamu hadi yamalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukeketaji wa wanawake linadhoofisha na kumdhalilisha mwanamke. Kwa hivyo, Wizara ichukue jukumu la kuhamasisha zaidi na kutoa elimu kwa wanaohusika. Pia ichukue fursa hiyo kwa kuwachukulia hatua wanaofanya uhalifu huo kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha ubakaji wa watoto kimeshamiri sana miaka ya hivi karibuni. Serikali kupitia Wizara ichukue hatua kali zaidi kwa watu wanaofanya vitendo hivyo haramu kwa watoto kuliko hatua inayochukua sasa. Hiyo itasaidia kukomesha udhalilishaji wa watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Ofisi ya Wizara ijengwe Dodoma na Serikali iiongezee Wizara fungu la fedha ili kuanza ujenzi huo badala ya kila mwaka kutenga fedha za ukarabati wa jengo la Dar es Salaam. Katika ujenzi Wizara izingatie watu walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara yako ifanye ushirikiano na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ili kuunganisha Vyuo vya Wananchi na Vyuo vya *VETA* katika maeneo yaliyo na *VETA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iongeze walimu katika Chuo cha Wananchi Mwanhala (Nzega) hasa katika fani za makenika na umeme, seremala na uashi na ushonaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hakuna kabisa walimu na wanafunzi ni wengi.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya hususan katika kuleta maendeleo ya jamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mafunzo yatolewayo yanawanufaisha siyo tu wale ambao hupata mafunzo hapo bali ni pamoja na wananchi wanaokaa katika maeneo ambako wahitimu hao wanakopelekwa kufanya kazi. Kwa kuwa baadhi ya vyuo hivi vilikuwa vimejengwa mahususi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima kwa mfano, Msinge na Mwanhala; na kwa vile mafunzo hayo yalisitishwa baada ya mabadiliko hayo; na kwa kuwa sasa Serikali inatoa msukumo mkubwa katika kuendeleza Sekta ya Kilimo, ninashauri kuwa mchanganyiko wa masomo uzibe pengo hilo kwa kutoa mafunzo maalum ya kilimo from time to time. Hili lifanywe kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hali ya majengo katika vyuo hivyo ni mbaya. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweka utaratibu wa kukarabati majengo hayo kama anavyoonyesha katika hotuba yake. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF).* Naipongeza Wizara kwa kuuendeleza Mfuko huu ambao unaonyesha mafanikio katika kuwapatia wanawake mtaji wa kuanzisha shughuli za kibiashara kwa vikundi. Katika Wilaya ya Ruangwa Mfuko huu unaweza kuleta hamasa katika uanzishwaji wa Viwanda vya Kubagua Korosho Vijijini, mradi ambao umeanza vizuri Wilayani humo.

Ombi langu ni kuwa Waheshimiwa Wabunge wawe wanafahamishwa kila fedha za Mfuko huo zinapopelekwa Wilayani ili waweze kufuatilia na kuhakikisha ufanisi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii moja kwa moja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa inayofanya katika kuleta maendeleo ya jamii, jinsia na watoto. Na kwa hiyo basi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuchangia hotuba hii katika upande wa watoto yatima ambao wazazi wao wote wamekufa kwa Ukimwi na wao wakawa ndio viongozi wa nyumba zao. Kwa kweli watoto hawa wanasikitisha sana kwa sababu wengi wao huwa viongozi wa kuwahudumia wadogo zao kwa kutafuta chakula, nguo na malazi. Wakati ambapo watoto hao hawana wa kuwasaidia, watoto hao hulazimika kwenda shule kwa matatizo sana maana huwa hawana msaada wa hata vifaa vya shule au malipo ya shule. Hali hiyo inawasababisha wengi wao kukosa kwenda shule na kukosa masomo na pia kukosa upendo kutoka kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza Wizara ifanye kazi ya utafiti wa kuwaelewa watoto hawa yatima ili kuwatafutia msaada wa kuwalea na kuwasaidia maana na wao ni miongoni mwa jamii hii ya Kitanzania, wasidharauliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia katika suala la watoto wanaofanya kazi majumbani. Watoto wengi husababishwa kupata Ukimwi kutokana na kubakwa na wale waliowachelewesha kuwafanyia kazi. Watu kama hao wakorofi huwalazimisha watoto wanaofanya kazi kufanya vitendo vya ngono bila wao kutaka. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweke Maafisa kila Kijiji wa kushughulika au kufuatilia nyendo halisi za watoto hao na wale waliowachukuwa kwa ajili ya kazi. Maafisa hawa wawe wanatoa ushauri kwa jamii kuacha kufanya vitendo vya kikatili kwa watoto wa majumbani (wanaofanya kazi) na endapo yatatokea mateso hayo kwa watoto hao basi Maafisa hao wawe wanatambua na kusimamia kesi zao maana wao peke yao (watoto) hawawezi kusimamia kesi hizo endapo litatokea tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, ni kwamba naomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (Mahakama) ili kuweza kubadilisha mfumo wa kuwaweka jela watoto kwa kuwachanganya na wafungwa watu wazima. Hali hii ya kuwachanganya watoto na wafungwa watu wazima si kuwatendea haki wafungwa hao watoto kwa sababu huko ndani wanafanyiwa vitendo vya kinyama sana na mwisho kuambukizwa Ukimwi bila ya huruma. Je, huo ni uungwana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii ilifuatilie suala hili la wafungwa watoto ili iwatetee watoto hao kwa kuwaweka (kuwajengea) watoto hao katika jela za watoto. Naomba sana Wizara iishauri Wizara husika iondokane na mfumo huo wa kikatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga tena mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yako ni muhimu sana kwa masuala ya maendeleo ya nchi. Lakini tembelea Wilaya uzione Ofisi zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sisitiza mikopo kwa wanawake ili kuwakomboa na jamii itaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wataalam walioko huko Wilayani watembelee sana maeneo husika, wakitoa elimu katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wako katika ngazi ya Wilaya wale ambao hawajapandishwa vyao wapandishwe vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana ya Wizara yake. Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ushirikiano mzuri anaoutoa kwa Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijitahidi kufuatilia utendaji kazi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto walioko Mikoani ili kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa karibu na wananchi ili kuhakikisha kuwa Wizara inapata picha ya aina ya Miradi ya Kiuchumi inayofanyika katika Wilaya mbalimbali. Wizara hii ni waratibu Wakuu wa Maendeleo mbalimbali yanayohusu watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iendelee kujenga hoja Wizara ya Utumishi ili ajira ya watumishi wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto waajiriwe katika ngazi kuanzia Vijijini kama ilivyo kwa Watendaji wa Vijiji. Unapozungumzia tu Sera ya Kujitegemea katika maendeleo ni lazima uwe na watumishi hao ambao kimsingi ndio wahamasishaji Wakuu. Serikali kwa ujumla wake ni lazima ilielewe hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale walio kazini, kuna haja ya kuwa na mipango mizuri ya muda mrefu na muda mfupi ya mafunzo kazini ambayo yatawasaidia watumishi hawa washiriki kikamilifu katika mabadiliko ya kijamii yanayoendelea hivi sasa. Wizara hii iwe na jukumu pia la kufahamu idadi ya wanawake kwa majina na nafasi walizonazo katika nafasi za uongozi ili kufahamu mafanikio yao na matatizo yao ili kama kuna namna ya kuwasaidia waweze kusaidiwa. Wizara pia iwe na *Data Bank* ya Wanawake wenye uwezo ili iweze kuisaidia Serikali katika utoaji madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuiongoza Wizara na kutatua matatizo yaliyokuwa yanakabili Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, naishukuru Wizara kwa kutenga fedha za kufanya ukarabati mkubwa katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa nia yake ya kuanzisha Benki ya Wanawake. Aidha, kwa kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa kutasaidia sana kuweka msingi wa kuanzisha Benki ya Wanawake. Wanawake wengi Vijijini wana mwamko mkubwa wa kutumia mikopo kwa ajili ya kuzalisha mali. Naomba Serikali iongeze kasi ya kuanzishwa Benki hiyo ya kuwahudumia wanawake.

Aidha, kwa kuwa Halmashauri nyingi hadi leo hazichangii asilimia 10 kwenye Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana; na kwa kuwa Serikali iliziagiza Halmashauri kutoa fedha hizo, nashauri Serikali ichukue hatua za kuwakumbusha wahusika ili fedha hizo (asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri ziweze kutolewa). Wale watakaokiuka au kuendelea kukaidi kutekeleza uamuzi wa Serikali basi wachukuliwe hatua za Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri inayoonekana kufanyika. Jitihada zao bila shaka zimezaa matunda kutokana na ushiriki mzuri wa Watendaji na wataalam kuanzia kwa mfano na Wakurugenzi na watumishi wote ambao kwa ufahamu wangu wa Wizara ni watumishi wenye bidii. Hivyo nawapongeza vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa Wilaya ya Hanang niliambiwa kuwa baada ya fedha za *WDF* kukusanywa zinarudishwa kwanza Makao Makuu ili zigawiwe tena. Utaratibu huu unaonekana kuchelewesha kutoa mikopo na vile vile ni risk ya fedha kupotea kwa wizi lakini lilo kubwa ni kuwa kutokana na muda unaotumika kuzirudisha na hatimaye kupewa tena Halmashauri mbalimbali, turnover ya utoaji mikopo itakuwa imepunguzwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa, ikiwa suala ni kuhakiki urejeshwaji wa mikopo, ni vyema Maofisa kutoka Wizarani wakaweka utaratibu mzuri wa *follow up,* ukawekwa. Wizara inapaswa kuwa waangalifu ikitumia *auditors,* kwani auditors huwa wanaangalia *situation* ya siku moja. Kwa mfano wakikuta fedha ziligawiwa kama mikopo wiki iliyopita wakakuta katika *Account* ya Halmashauri husika ni kidogo, ni rahisi kwa taaluma kuona kuwa mikopo haijereshwi na hii ndiyo taarifa inayotumiwa na kutoa *general statement,* hali ya urejeshwaji wa mikopo ya akina mama. Hali kadhalika ikitokea kuwa audit inafanyika siku ambazo fedha zimerejeshwa basi itaonekana kuwa wanawake ni hodari katika kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ni vema kufanya tathmini kamili baada ya *normal audit* ili kuona hali halisi ya mikopo hii. Kwa uelewa wangu kwa Halmashauri zinazojitahidi kufuatilia mikopo kwa utaratibu uliowekwa, urejeshaji wa mikopo ni mzuri kuliko hata Mabenki mengi wanavyofanya. Hii aina maana kwamba ni kila Halmashauri kwani kuna chache ambazo haziifuatilii mikopo na hivyo siyo haki kutoa *general statement* na kuonyesha kuwa utaratibu uliopo siyo mzuri au akina mama hawalipi mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kuwepo kwa Bajeti finyu kwa mahitaji ya Wizara kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 42 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hivyo ningeshauri Wizara iongeze Makadirio yake miaka ijayo hasa kwenye Vyuo vya Maendeleo kama vile *FDC - Ifakara.* Ada ya Sh.50,000/= kwa mwaka kwa kila mwanafunzi ambaye anahudumiwa malazi na chakula ni kiasi kidogo mno, hivyo kuathiri ubora wa mafunzo na kupunguza umakini wa walimu katika kuwahudumia wanafunzi kwa kukerwa na matatizo ya uendeshaji vyuo. Ni kweli vyuo hivyo vinapaswa kuchangia mapato mengine kwa kuuza huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujihusisha na kilimo. Lakini ni muhimu fedha zinazotolewa na Wizara zikidhi haja yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jedwali namba 5, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha mgao wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* kwenye Wilaya mbalimbali nchini. Ningeshauri Mfuko huu ungeongezwa na kujumuisha pia jamii nzima. Mfuko ungebadilika na kuitwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Jamii *(Women Development and Community Fund - WDACF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya badiliko hilo Mfuko huu uongezewe kiwango zaidi na utumike zaidi kwenye kusomesha jamii kwenye vyuo vyetu vya kuwakopesha wanafunzi wenye kuweza kujiandikisha masomo maalum ya kuwawezesha kujitegemea baada ya kuhitimu. Mikopo hiyo iwe ikirudishwa baada ya muda mrefu.

Baada ya hapo inabidi ada kwenye vyuo hivyo zipandiswe angalau kufikia Sh. 150,000/= kwa mwaka badala ya Sh.50,000/=. Aidha, Wizara ingeungana pia na Wizara ya Elimu na Utamaduni kwenye suala zima la elimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim P. Khan, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi mazuri ya hoja ya Wizara hii na bila kuisahau Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii adhimu. Kwanza, napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kuchora dira ya mwelekeo wa Wizara hii ambayo kabla ya hapo ilikuwa haieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu ni moja. Nashauri Vyuo vya Maendeleo katika Wilaya viwe vituo vya kiuchumi kwa hasa akina mama. Maendeleo ya kiuchumi kwa akina mama yana mustakabali mpana sana.

Lakini nafikiri kama kweli tunaazimia kuwaondoa akina mama katika umaskini basi katika kila Wilaya ni lazima tuwatafutie kituo ambapo *comprehensively;* mustakabali mzima wa maendeleo yao utasimama. Kwa mfano: -

(i) Akina mama wataelimishwa kuhusu miradi gani inafaa katika kuwainua kiuchumi.

(ii) Mchanganuo utafanywa na wataelimishwa vilivyo mpaka waelewe wanachokifanya.

(iii) Viwe vituo vya usimamizi wa kuratibu maendeleo ya miradi ya jinsi gani watazalisha fedha za mikopo na kuweza kurejesha.

(iv) *Record* yao, maendeleo yao na masoko yao yatakuwa *monitored.*

(v) Patakuwa ni mahali maalum pa kuwafundishia na kuwabadilisha ili waweze kujiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo Urambo kinahitaji msaada wa ukarabati wa majengo na mitambo na pia kufufua josho na mashamba ya majaribio ambayo yangetumika vizuri kwa mafunzo ya vitendo ambavyo ni muhimu sana kuwabadilisha kimaendeleo.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja isipokuwa nina swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Wilaya mpya hazikupewa mgao wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Halmashauri kutochukua fedha za mkopo, lakini fedha hizo hazikutengwa kabisa, ni kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu juu ya hoja hii nzito ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba nikiri kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wametuandikia michango yao na wengine wametoa michango yao kwa kauli. Kwa sababu ya ufinyu wa muda hatutaweza kujibu hoja zote hapa, lakini hii haina maana kwamba tunawapuuza, bali tunawaahidi kwamba tutawajibu kwa maandishi hoja zao kabla ya kikao hiki kuahirishwa. Lakini napenda kusema kwamba mawazo yao ni mazuri na yatatusaidia sana katika kutekeleza kazi zetu za siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuzungumzia suala la mikopo kwa Wanawake. Mheshimiwa Salama Islam, Mheshimiwa Aziza Ally pamoja na Mheshimiwa Maria Watondoha aliyemaliza kuzungumza sasa hivi, wamezungumzia kiwango cha mikopo kwamba ni kidogo, pia wamezungumzia Wanawake kupewa taaluma ya kuendesha mikopo. Naafikiana na Waheshimiwa Wabunge wote kuhusu suala hili, lakini kwa upande wa kiwango cha fedha kinachotolewa huzingatia ukubwa wa Mfuko na jinsi mikopo iliyokopeshwa itakavyorejeshwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa Wanawake wengi wanapata mikopo

hasa Vijijini. Aidha, ugawaji wa mikopo haubagui, inatakiwa Wanawake wote wapewe ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Margareth Mkanga, ametuandikia kwamba tusiwabague watu wenye ulemavu maana Mikoa kama Morogoro, Mtwara na Lindi tayari wameanza kuwakopesha hao akina mama. Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Ponsiano Nyami nao wamezungumzia kwamba, tuelekeze mikopo Vijijini. Nashukuru sana kwa mawazo yao, ni kweli tunafanya hivyo kwa sababu mkiangalia jedwali mtaona kwamba tayari tumepeleka mikopo hii katika Mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, anasema hivi, utaratibu uliopo wa kufuatilia mikopo uboreshwe na kushauri kwamba, badala yake wataalam wa Wizara wafuatilie kwa upana zaidi. Utaratibu mpya ulianza mwaka 2002/2003, huu ni muda mfupi wa kuweza kujua matatizo na mafanikio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itazingatia ushauri wake wakati wa kuboresha utaratibu uliowekwa ambao ulikuwa wa majaribio. Nakushuru Mheshimiwa Dr. Mary Nagu. Mheshimiwa Philip Magani, amesema Wabunge wawe wanajulishwa fedha za *WDF.* Wabunge ni Wajumbe wa Kamati ya Mikopo.

Sasa yeye Mheshimiwa Mbunge, ni Mjumbe wa Kamati ya Mikopo na ana haki ya kujua fedha hizi zinakopelekwa. Kwa hiyo, naomba tuwe pamoja kufuatilia kwa Wakurugenzi wetu na sisi kama mlivyotuomba tutakuwa tayari kuwaletea nakala za barua hizo.

Vile vile Mheshimiwa Semindu Pawa, anasema kamati iundwe ya kufuatilia michango ya Halmashauri kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Wizara itaandaa utaratibu kwa kushirikiana na TAMISEMI kuhusu ufuatiliaji wa michango hiyo.

Pia amesema kwamba madiwani wanalalamikia kuachwa kwenye Kamati ya Mikopo ya *WDF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hizi ziwe ndogo kwa sababu tukiwa wengi sokomoko ndiyo linaanzia hapo. Lakini pia naomba niseme kwamba sisi pia kama ni Wabunge ni Madiwani na tunaweza kusimamia mifuko hii. Lakini bado katika kuborasha mfuko huu wazo la Mheshimiwa Mbunge litazingatiwa.

Pia Mheshimiwa Henry Shekiffu amesema utaratibu wa sasa wa kutoa mikopo ufike vijijini. Ni kweli kabisa mikopo tayari tumefikisha vijijini, lakini tatizo ni kwamba mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wetu. Isipokuwa bado napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, agizo la Waziri Mkuu bado liko pale pale na kwamba kila Halmashauri iendelee kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Mifuko hii miwili ya Wanawake na Vijana.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Paul Makolo ameuliza kwa nini Wilaya mpya hazikupewa mikopo? Ni kweli Wilaya Mpya hazikupewa mikopo kwa sababu wakati huo walipewa mikopo katika Wilaya zao za zamani. Naomba niseme kwamba mikopo yao iko tayari na kwamba wanaweza kumtuma Afisa Maendeleo ya Jamii, ili aje aweze kukamilisha taratibu. Katika kukamilisha taratibu waanze kufungua akauti huko waliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, amezungumzia kwamba mfuko huu utumike kwa kuwakopesha wanafunzi wasiyo na uwezo. Lengo la mfuko ni kukopesha kwa ajili ya kuzalisha. Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji nao wamezungumzia hilo hilo.

Pia Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, anasema fedha zitengwe kwa ajili ya kuwakopesha wajane kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mimi naona tufuate ushauri wa Mheshimiwa Margareth Mkanga kwamba tusiwatenge akina mama, akina mama wote waingie chini ya mfuko huu. Kwa hiyo pia na Wajane waombe na wapewe kutoka mfuko huu wa WDF. Mheshimiwa Margareth Mkanga ameshukuru Wizara zilizotoa mikopo kwa wanawake wenye ulemavu. Mheshimiwa Halimenshi Mayonga ameuliza je, ni Halmashauri ngapi zimeshindwa kutoa taarifa sahihi na hatua zilizochukuliwa ni zipi? Halmashauri 29 hazijakiri mapokezi ya fedha walizopewa. Katika jedwali ukurasa wa 64 na 65 utakuta Halmashauri 29 hazijakiri mapokezi ingawaje wamechukua fedha hizo. Hatua ya kwanza tumewakumbusha kukiri mapokezi.

Aidha mkataba tuliowekeana unawabana kwa mfano hawawezi kupelekewa fedha nyingine mpaka wamekiri na kurejesha. Sasa kwa bahati mbaya Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma hazijakiri. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Halimenshi Mayonga afuatilie ili waweze kupewa mkupuo unaofuata. Lakini hapa pia naomba niwapongeze tena Mtwara Mikindani na Bagamoyo ni Wilaya mbili tu zilizokiri na kurejesha mikopo hiyo, maana mkataba ulisema kwamba by 30th June wawe angalau wamefanya hivyo. Kwa hiyo, kati ya Wilaya hizo zote ni Wilaya mbili tu zimefanya hivyo. Ninawapongeza. *(Makofi)*

Vile vile Mheshimiwa Aggrey Mwanri, amesema Wizara itoe mikopo zaidi kwa wanawake wa Siha kwa juhudi walizoonyesha za kuunda vikundi. Naafikiana naye lakini hii ipo mikononi mwake kwa sababu yeye ni Mjumbe katika Kamati hiyo na ana uwezo huo wa kujua nani apate na nani asipate. Mheshimiwa Aggrey Mwanri endelea na msimamo wako huo. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala wamesema Maafisa Maendeleo ya Jamii wapewe elimu zaidi ili waweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao. Nakubaliana na hoja hii kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Wizara yetu, inaendelea kutoa mafunzo ya rejea kwa wataalam hao.

Aidha Wizara imetenga asilimia 60 ya nafasi za kujiunga na Stashahada ya Juu ya Maendeleo ya Jamii kwa Watumishi wa Maendeleo ya Jamii walio katika Halmashauri. Nia ni kuimarisha taaluma za wataalam hao ili waweze kutekeleza kazi zao barabara. *In other words* kwanza miaka ya nyuma tulikuwa tunawachukua wanachuo 70 lakini kwa mwaka huu tumeongeze idadi ya wanachuo hadi 210 yaani mara tatu zaidi. Kati ya hao 210 asilimia 60 ni wale Maafisa Maendeleo wetu walioko watachukuliwa. Asilimia 40 ni wale pre service waliomaliza form six. Kwa hiyo, Wizara imeongeza kutoka wanachuo nafasi 70 hadi 210. (Makofi)

Pia Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Halmenshi Mayonga, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, wamezungumzia hali duni katika vyuo vyetu kutokana na ufinyu wa bajeti.

Wizara inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, kuwa hali katika vyuo vyetu inahitaji kuimarishwa kimajengo na kimiundo mbinu, kitaaluma, kinyenzo na kadhalika. Serikali kupitia Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuziimarisha huduma na hali ya vyuo hivi.

Aidha nakubaliana na maoni kuwa, hali katika vyuo vya *VETA* ni nzuri zaidi kuliko wenye vyuo vya maendeleo. Hii inatokana na ukweli kuwa *VETA* wanavyo vyanzo vingi vya mapato vikiwemo *vet levy.* Bajeti ya Serikali na wafadhali ukilinganisha na Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi ambavyo vyanzo vyake vya fedha ni Bajeti ya Serikali, michango ya wananchi na miradi ya vyuo vya kujitegemea. Maana kila chuo kina miradi ya elimu ya kujitegemea *(EK).* Sasa kwa kutambua hali duni katika utoaji elimu na mafunzo katika shule na taasisi zake, Serikali imeandaa mpango wa kuimarisha elimu ya msingi na hivi sasa inaendelea na maandalizi ya mpango wa kuimarisha elimu ya mafunzo katika vyuo na taasisi nyingine. Baada ya elimu ya msingi naamini hali ya vyuo hivi itaendelea kuimarika katika jitihada hizo za Serikali. Aidha ninaziomba Halmashauri na wananchi nao kuendelea kujitoa zaidi katika kuviendeleza na kuvitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Halmashauri zinasaidia sana vyuo vyao, kama vile Anatoglo, Ifakara, Kasulu, Kibondo, Kilosa, Mbinga, Isingi, Mwanza, Newala, Rubondo, Nandembo. Kwa upande wa Wabunge nao tusimsahau Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kapeleka *computer* mbili kwenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Handeni. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Nimemaliza masuala ya *WDF* sasa naingia kwenye maonyesho ya biashara. Mheshimiwa Margareth Mkanga anasema kwamba washiriki wa maonyesho ni wale wale mwaka hadi mwaka, anashauri utaratibu uwekwe wa kupata washiriki tofauti tofauti. Hili pia limezungumzwa na Mheshimiwa Esha Stima. Wizara imewasiliana na Wilaya kuhusu suala la kuleta washiriki tofauti kila mwaka. Hata hivyo, tutawasiliana na Halmashauri kusisitiza hilo. Ni kweli kabisa unapofika pale Saba Saba unakuta nyuso zile zile. Je, wengine hawana kiu? Naona itabidi turekebishe. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Salama Khamis Islam, amempongeza sana Mheshimiwa Mama Anna Mkapa kwa kufadhili ushiriki wa wanawake katika maonyesho haya na kumwomba aendelee kutuunganisha wanawake. Hata hivyo amesisitiza haja ya Serikali kusaidia wanawake kupata masoko baada ya maonyesho. Ameshauri Wizara zote mbili za Bara na Zanzibar zishirikiane kuhusu suala hili. Hili pia limezungumzwa na Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Diana Chilolo. Ni kweli kabisa na sisi pia tunampongeza sana Mama Anna Mkapa kwa jitihada zake kuwasaidia akina mama. Lakini sasa lililojitokeza ni idadi ya washiriki kama alivyozungumza Mheshimiwa Esha Stima ni kwamba idadi kidogo inaanza ku-drop na ukitazama katika kitabu hiki kwenye jedwali ukurasa wa 62 utakuta kwamba idadi haipo stable imeanza ku-*drop* na hii imetokana hapa tulipoanza tu masuala haya ni Mama Anna Mkapa pamoja na Serikali *(Central Government)* Serikali Kuu na baadhi ya wadau tu walikuwa wanawagharimia hawa washiriki kikamilifu. Lakini baada ya ku-*introduce cost sharing* basi idadi imeanza kupungua. Kwa mfano mwaka 2002 washiriki walikuwa 145 na kwa mwaka huu washiriki wakawa 125. Naafikiana na Wabunge wenzangu kwamba kuna haja ya kulitazama hili ili tuweze kulitatua la sivyo tutakuwa reduced to zero ambacho siyo kitu kizuri. *(Makofi)*

Vile vile Mheshimiwa Mariam Mfaki amempongeza mama Anna Mkapa na pia amehimiza Halmashauri, kuwasaidia wanawake waweze kushiriki. Ni kweli kabisa kuna Halmashauri ambazo zinawasaidia wanawake lakini Halmashauri zingine kwa kweli ni sugu. Wakisikia tu wanawake wanataka kwenda kushiriki kwa kweli vichwa vinawauma. Sasa mimi sielewi kwa ni nini? Lakini katika utafiti wetu tutawajua hawa ili tupate dawa yao. Vile vile Mheshimiwa Diana Chilolo amesema hawana masoko ya bidhaa. Ni kweli kabisa naafikiana na Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba tatizo ni soko la bidhaa. Mheshimiwa Mwenyekiti naomba unilinde. Kwa hiyo, tutashirikiana na wadau kama vile *EOTF, FAWATA,* Wizara ya Viwanda na Biashara, kutafuta soko pamoja na *NGOs. (Makofi/Kicheko)*

Pia Mheshimiwa Salama Khamis Islam amezungumzia mafunzo, haya yanaingia kwenye mikopo, ninaafikiana naye kwamba bila mafunzo tatizo lipo la marejesho na hili litatazamwa upya na Wizara yangu pamoja na Wizara zinazohusika kama vile TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, maana Wizara ya Viwanda na Biashara mikopo yao inarejeshwa vizuri kupitia mfuko wa wafanyabiashara *(NEDF) National and Enterprenership Development Fund* . Kwa hiyo, kuna haja kukaa pamoja na kujadili.

Pia Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Juma Sereweji, Mheshimiwa Masoud Abdallah wamezungumzia kudhibiti maambukizi ya virusi vya ukimwi na athari za ukimwi wenyewe pamoja na kama nimemsikia vizuri Mheshimiwa Maria Watondoha. Ukimwi kama Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alivyotangaza ni janga la taifa. Katika mazingira haya kila aina ya nyenzo inayoweza kutusaidia kushinda vita dhidi ya ukimwi na athari zake hatuna budi kuzitumia. Napenda kukubalina na michango mbalimbali kuhusiana na mapambano yetu dhidi ya balaa la ukimwi. Aidha nawaomba Waheshimiwa Wabunge, elimu tunayoendelea kuipata kuhusiana na tatizo hili tufikishe kwa wapiga kura wetu. Ukimwi ni tatizo la kijamii, ufumbuzi wake uko kwenye jamii kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia kwa kauli na maandishi. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Diana Chilolo amezungumzia suala la Wizara inahusianaje na Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye ngazi ya Halmashauri na Kata, elimu ya Watalaam hao haitoshelezi, hawana vitendea kazi. Wizara inatoa maelekezo ya kisera, Wizara ina jukumu la kuwaendeleza kitaaluma, Wizara inashirikiana na mamlaka husika kuhakikisha wanakuwepo wataalamu wa kutosha katika ngazi hizo kwa kuzingatia sheria. Wizara inatoa mafunzo ya rejea na imeongeza nafasi zaidi za kujiunga na mafunzo ya stashahada ya juu kama nilivyozungumza. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri hizo kuwatafutia vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haroub Said Masoud ameelezea kuhusu unyanyasaji alioushuhudia pale Ubungo tarehe 22/7/2003. Ameshauri vibanda vijengwe kama Halmashauri ya Wilaya ya Ilala. Aidha kodi ya vibanda shilingi 15,000 ni kubwa wapunguziwe. Kuna vitendo vinafanyika ambavyo Serikali haijui, lakini tunashukuru kuwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwa upande wa Dar es Saalam jitihada zimefanyika ya kujenga vibanda hapa ni mwanzo. Ninaamini Halmashauri nyingine zitajitahidi. Hapa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Yussuf Makamba kwa kazi nzuri anayofanya kuwatetea hawa akina mama, mama lishe na baba lishe. Lakini pia kwa upande wa vibanda vya *Cococala* ambavyo vinawatoza shilingi ya 15,000/= tumelichukulia na kwa bahati nzuri siku hiyo walikuwepo Wabunge wa Dar es Salaam wameahidi ku-take up maana wao pia ni Madiwani. Kwa hiyo, tutaendelea kufuatilia suala hili. *(Makofi)*

Vile vile Mheshimiwa Salama Khamis Islam anasema wanawake huathirika zaidi kutokana na mila potofu, kurithiwa na ukeketaji. Wizara imelipa suala la mila potofu kupigwa vita katika sera zake, sheria, hakuna mila potofu ambayo inakubali hayo yote. Mheshimiwa Haroub Said Masoud anasema kutosheka kuweka mazingira yanayovutia pale kwako unapoishi ili kupunguza vishawishi nje ya nyumba yako, amesisitiza kila mtu awe na mpenzi mmoja. Tumepokea ushauri wake. *(Makofi)*

Kwa upande wa ukeketaji Mheshimiwa Haroub Said Masoud ametoa ushauri mzuri kwa wale wote wasio keketwa wanaume wasaidie kukomesha hiyo tabia. Tunashukuru kuwa Mheshimiwa Mbunge ameona umuhimu wake. Mheshimiwa Ponsiano Nyami, amesema taarifa ya Mkutano wa Bagamoyo ilishitusha Wabunge kuogopa kukemea hiyo tabia ili wasikose kura, kadhalika akashauri Madiwani tuwaelimishe, tunapokea ushauri wake Wizara itaendelea kuimarisha mkakati wa kijamii wa kuwakinga wanawake dhidi ya ukimwi kupitia Vyuo vya Maendeleo nakadhlika. Ushauri wake tumeupokea. Mheshimiwa Aziza Ali, ametoa ushauri wa kuwalea watoto yatima, jamii ielimishwe kuwa na mapenzi kwa watoto kwanza kabla ya kufikiria kupeleka watoto kulelewa katika vituo vya kulelea watoto.

Kwa kuzingatia mila na desturi zetu bado tunazingatia mfumo wa kuwalea watoto yatima katika familia, kaya na jamii. Hatua ya kuwalea watoto hawa katika vituo vya watoto liwe ni hatua ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi mazuri yamezungumzwa kama nilivyosema hata Mheshimiwa Jina Khatib Haji amezungumzia masuala ya unyanyasaji wa watoto, wanaoajiriwa, Mheshimiwa James Mntangi naye amezungumzia masuala ya utekelezaji wa sheria ya kupinga ajira ya watoto, Mheshimiwa Henry Shekiffu amezungumzia Wizara ilipe madeni Handeni Chuo cha Magughai. Serikali inakubali kulipa madeni ni wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabla sijagongewa kengele naomba Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kwamba wote tumepewa vitabu kama hivi na vina majedwali. Sasa naomba tukirudi tukayafanyie kazi majedwali haya kwa sababu kuna mapengo mengi tu. Sasa naomba mkirudi tukashirikiane na watendaji wetu ili mapengo haya yasiwepo mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza kwa nusu saa nasema naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, ushauri na hoja walizozitoa wakati wakichangia hoja yangu. Orodha ya Wabunge waliochangia kwa kauli hapa Bungeni ni 14, waliochangia kwa maandishi ni 39. Naomba kabla sijajibu hoja hizo niweze kuwatambua na kuwashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa wale waliochangia kwa kauli nao ni Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Maria Watondoha,

Mheshimiwa Esha Stima na Mwisho lakini siyo mwisho kwa kutokukuwa muhimu ni, Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na ambaye pia amenisaidia kwa kiasi kikubwa sana kujibu hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Hassan Makame, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Kidawa Hamis Saleh na Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Wengine ni Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmael, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Cnythia Ngoye, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Fatma Said Ali ( Mchumo). Napenda tena kuwashukuru wote waliochangia kwa kauli, kwa maandishi na pia kwa kutuunga mkono kwa makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nichukue fursa hii kupitia hoja kwa ujumla baadhi ya zile zilizotolewa hapa. Naomba nikiri kwamba kwa ajili ya muda tunaweza tukashindwa kujibu zote hapa sasa hivi, lakini tunaahidi kwamba tutazijibu kwa maandishi kabla ya kikao hiki kumalizika. Kwanza tunashukuru sana Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushauri waliotupa na ningependa kujibu baadhi ya yale waliyotuambia ili kuwathibishia kwamba tutaendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wamezungumzia suala la uandikishaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *VETA* ili wahitimu wake watambulike. Napenda kuihakikishia Kamati kwa kweli hivi sasa tuna ushirikiano wa karibu sana na *VETA* na kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, tunafanyia tathmini mpango mzima wa elimu ya ufundi baada ya mafunzo ya elimu ya msingi. *VETA* pamoja na Wizara yangu tunaunda kamati ya pamoja katika mpango wa kuboresha elimu na mafunzo. Kwa hiyo, tutaendelea kuangalia ni namna gani tuweze kuchukua uzoefu wa wenzetu. Lakini napenda kusema kwamba maeneo yote yale ambayo yatabainishwa na ushirikiano huu na utafiti huu yatasaidia sana kuboresha kazi za Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa pia suala la ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hili limezungumzwa na Kamati, limezungumzwa pia na Waheshimiwa Wabunge. Naomba niseme kwamba kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, Wizara inaendelea kufanya ukarabati. Mpango huu tuliuanza mwaka 2001/2002 kwa kufanya kwanza matengenezo madogo madogo kwa kuzingatia wakati ule uwezo wa kibajeti wa Wizara. Mpaka kufikia mwisho wa mwaka 2003/2004, Wizara itakuwa imekamilisha ukarabati mdogo mdogo wa vyuo vyote. Lakini kama nilivyosema hivi sasa tumeanza awamu nyingine ya kufanya ukarabati mkubwa. Lakini kama tulivyoanza na ukarabati mdogo mdogo pia tutakwenda kwa kadri ya uwezo wa kibajeti, lakini sisi ndani ya Wizara tunatiwa moyo kwamba tuliweza kufanya ukarabati mdogo mdogo na hivi sasa tutakamilisha karibu vyuo vyote mpaka kufikia mwisho wa mwaka 2003/2004 na hivi sasa tuko katika kufanyia ukarabati mkubwa baadhi ya vyuo kimiundo mbinu na kimajengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ushauri hapa kupitia kwa Kamati na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwamba Wabunge wanawake wote wawe Wajumbe wa Bodi za Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika Mikoa yao. Kimsingi Wizara inateua Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa Viti Maalum, Wabunge wa Kuteuliwa wote kuwa katika Bodi hizi, endapo wapo katika maeneo ambayo vyuo hivyo vipo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tumefanya hivyo na tunategemea sana kwamba tutapata mchango wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa ushauri kwamba tuhimize Halmashauri kuwapatia kazi wahitimu wa vyuo kulingana na ujuzi waliosomea na tumepewa ushauri pia kwamba tuhamasishe Halmashauri hizi katika kuchangia vyuo. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amezitaja Halmashauri zile ambazo zimekuwa zikituchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kutoa rai tena kwamba Halmashauri nyingine ziendelee kuchangia Vyuo hivi kwani ni Taasisi ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na jamii zinazowakilishwa katika Halmashauri hizo.

Lakini lingine ambalo ningependa niliseme ni kwamba, Vyuo hivi tunawatayarisha vijana hawa kujiajiri wao wenyewe. Kwa hiyo tunategemea kwamba ingawaje wanaweza wakapata ajira katika maeneo mengine, lakini kimsingi tunawapa taaluma, tunawapa stadi ili waweze kujiajiri na hivyo kupunguza msongamano katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa ushauri hususan na Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba tuangalie utaratibu wa kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hapa Dodoma. Kimsingi sisi hatuna tatizo kwa sababu ni uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma, lakini tungependa tu kusema kwamba ukarabati tunaoufanya ni kwa ajili ya kuzingatia matatizo yanayojitokeza hivi sasa kikazi. Nadhani Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mnafahamu kwamba Wizara yetu hivi sasa imepata Idara mpya ya Watoto. Hilo tayari ni jambo ambalo linatufanya tuangalie nafasi finyu tuliyonayo, lakini vile vile kupitia miradi mbalimbali na kadri tunavyoboresha utendaji kazi tunakuwa na zana kama vile *computer, printers* na kadhalika vitu ambayo vinahitaji kuwekwa katika Ofisi zenye nafasi. Kwa hiyo, kwa kweli tunachokifanya ni upanuzi mdogo na kuongeza samani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshauriwa Vyuo vyetu viruhusiwe kutumia fedha zilizokusanywa katika kuboresha Vyuo na hali ya maisha ya wanafunzi Chuoni. Tunapenda kuishukuru Kamati kwa ushauri huu na napenda tu niseme kwamba tutaangalia kwa kadri taratibu za fedha zinavyoruhusu tuweze kuona ni nini tunafanya. Lakini labda niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge na hasa kwa sababu nyinyi mko kwenye Bodi za Vyuo vyetu kwamba katika baadhi ya Vyuo kuna miradi ya Elimu ya Kujitegemea. Miradi ile pia inachangia nguvu ya Serikali katika kuendesha Vyuo. Kwa hiyo tutakachowaomba kupitia Bodi hizi na kupitia uongozi wenu, muweze kuhakikisha kwamba vile Vyuo ambavyo vina Elimu ya Kujitegemea kweli vinatumia fedha zile kwa manufaa ya Vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauriwa pia na Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba Wizara hii ina majukumu mengi makubwa lakini Bajeti haitoshelezi. Hilo ni suala ambalo ningependa kusema kwamba, kwa ujumla sio rahisi kwa bajeti ya Serikali kukidhi mahitaji halisi ya kila Wizara, lakini hata hivyo sisi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tunatambua jitihada zinazofanyika kwa ujumla wake na kwa mwaka huu wa fedha Serikali imeweza kuongeza kiasi cha Shilingi milioni 600 katika Bajeti ya Wizara. Nina imani kabisa kadri nchi yetu itakavyokuwa inaimarisha uchumi wake na viwango vya Bajeti vitaweza kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya masuala ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyazungumzia hususan kuhusu mafunzo kabla ya kupewa mikopo. Hilo sitalirejea, kuna suala la Halmashauri kuhakikisha zinatoa mchango wao. Hili limepigiwa kelele sana lakini ningependa kusema kwamba sisi kama Wizara tutaendelea kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba Halmashauri zinatoa michango yao.

Kamati pia imetushauri tuongeze fungu kwa ajili ya kununulia vifaa na zana mbalimbali katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi. Napenda nami niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza kuzipongeza zile Halmashauri, lakini kuwapongeza Wabunge na viongozi wengine mmoja mmoja ambao wamekuwa wakichangia hasa eneo la vitendea kazi. Amemtaja Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, labda nadhani nimtaje pia Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge; kwa kuweza kusaidia sana Chuo cha Kilala. Amekipa msaada mkubwa na tunapenda kushukuru kwa kweli kwamba ameweza kuona tatizo hilo na ninadhani kwa kweli ni mfano wa kuigwa kwa maana Waheshimiwa Wabunge Vyuo hivi ni vya kwetu viko ndani ya Majimbo yetu, vinasaidia wananchi wetu na pale hali inaporuhusu, tutashukuru

sana kama mtaendelea kufanya hivyo. Ninavyokumbuka Mheshimiwa Mudhihir alituchangia kiasi hakipungui milioni kumi hivi, kumi na saba kitu kama hicho. *(Makofi)*

Lakini nina habari pia Mheshimiwa Ponsiano Nyami sijui kama yupo na yeye amekuwa akitoa mchango kwenye Chuo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa ushauri pia Wizara yetu iwasaidie Wakuu wa Vyuo kupata mafunzo zaidi ya namna ya kuendesha Vyuo na kuwafanya wawe wabunifu katika kuendesha Vyuo hivyo. Ni kweli huu ni ushauri mzuri tunauchukua, lakini labda nitoe taarifa kwamba kwa hivi sasa tuna mpango na tumekuwa tukifanya hivyo, tumekuwa tukitoa mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuwaimarisha kiuongozi na pia kuwapatia mbinu zitakazowawezesha kuwa wabunifu zaidi kwa sababu tunaamini kwamba tukiwa na Wakuu wa Vyuo wabunifu basi na wao wataweza kuvifanya Vyuo vile vipanue utendaji wake wa kazi na viwe imara zaidi.

Kuna suala limezungumziwa hapa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu vikao vya Bodi kutoitishwa. Hili ni jambo na sisi tumeliona pia Waheshimiwa Wabunge na tumekuwa mara kwa mara tukikumbusha. Lakini kama ambavyo tumefanya kama tulivyoeleza katika hotuba yetu, tumeweza kuonyesha Vyuo mbalimbali, tumeweza kuonesha utendaji kazi wao na ninadhani katika baadhi ya yale majedwali mtakuwa mmeona ni maeneo gani ya kuyaimarisha. Eneo mojawapo ni eneo hili la kufanya mikutano ya Bodi kwa sababu Bodi ndio zitakuwa zinazimamia Vyuo hivi na zitakuwa zinaongoza Vyuo hivi. Kwa hiyo, tutaendelea kuwakumbusha na kuwaagiza Wakuu wa Vyuo ili waweze kuhakikisha vikao vinafanyika kwa sababu wao ndio Makatibu wa Bodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kujielekeza kwenye baadhi ya hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Sasa labda niseme tu kwa ujumla wake kwamba picha inayojaribu kujengwa na hotuba ile siyo sahihi. Inaonyesha kana kwamba nchi yetu bado imegubikwa na umaskini uliokithiri, miaka 40 hakuna maendeleo yoyote, hakuna nyumba bora, Serikali imeshindwa kumaliza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu, kwa kweli hiyo sio picha halisi ya Tanzania ya leo. Ukitazama sio tu kwa macho lakini hata kwa taarifa ambazo hazifungamani na upande wa Serikali, taarifa kama ya Benki ya Dunia, taarifa kama za Mashirika ya Kimataifa ambazo zinaweza zikapatikana kwa urahisi sana kwenye mtandao wa *Internet* lakini pia zinaweza zikapatikana katika Ofisi za Benki ya Dunia zilizoko Dar es Salaam, ripoti hizo zote zinaonyesha kwamba kiwango cha umaskini kimepungua toka asilimia 49 katika miaka ya katikati ya 1990 hadi kufikia asilimia 36 kwa mwaka wa 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kusema kwamba kwa kweli hatua imepigwa. Hatusemi kwamba kuwa na kiwango kidogo basi turidhike, lakini ni lazima tukubali kama Watanzania, kama Wazalendo wa kweli kwamba hatua imepigwa na hata ukiangalia maeneo, ukiangalia eneo moja moja, kwa mfano eneo la elimu ni juzi tu hapa tulikuwa tumemsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, tulikuwa tumepata pia semina na tulipata taarifa kamili na tulipata *figures,* hazikuwa hadithi, zikionesha ni namna gani uandikishaji wa watoto umekua. Hilo kwa kweli nadhani ni jambo linaloashiria vizuri sana kwamba nchi yetu inapiga hatua. *(Makofi)*

Lakini hata ukiangalia katika eneo la afya, hivi sasa wananchi wetu wana huduma bora zaidi kuliko hata miaka mitano tu iliyopita. Kwa hiyo siyo kweli kwamba hakuna kitu ambacho Serikali inafanya. Lakini labda nimalizie kwa kusema kwamba hivi sasa imekubalika kila mahali na inafahamika kwamba sisi Tanzania kama nchi tumefanikiwa kujenga uchumi tulivu. Huwezi kujenga uchumi tulivu kama nchi yako haina maendeleo. Sasa kitu kilichofanyika, kuwepo kwa uchumi tulivu ni kielelezo tosha cha jinsi hali inavyokuwa nzuri na changamoto yetu kwa kweli ni kutumia hali hiyo sasa kupiga hatua zaidi katika eneo hili la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa ni la ujumla, lakini pia tumeulizwa hapa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanapatikanaje, wanaandaliwa ndani au nje ya nchi, kuna mitaala gani. Je, Wizara ndiyo inawaajiri? Ningependa kusema kwamba Wizara yangu kama nilivyosema katika hotuba yangu ni kwamba tunavyo Vyuo vinne vya Maendeleo ya Jamii na hivi

kwa kweli ndiyo vinatumika kwa kiasi kikubwa kuwatayarisha wataalam hawa wa maendeleo ya jamii katika ngazi ya Cheti na Stashahada ya Juu. Lakini mitaala inayotumika katika Vyuo hivyo hupitishwa na Mamlaka mahususi Serikalini yaani Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, hili ndilo linaloangalia mitaala na mitaala hii inazingatia mahitaji ya kitaaluma katika eneo la maendeleo ya jamii kwa wakati huu tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Wizara hii ndiyo inawaajiri wataalam hawa. Katika Wizara tunao wataalam wa Maendeleo ya Jamii, lakini pia wataalam hawa huajiriwa na Serikali za Mitaa, huajiriwa pia na wadau mbalimbali, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, yote haya huwachukua wataalam hawa wa Maendeleo ya Jamii. Lakini pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani ametutaka tuangalie uchakavu wa majengo na miundombinu, nadhani hili tayari tumeshalizungumza, kama tulivyosema tulianza ukarabati mdogo mdogo 2001, tumekuwa tukiendelea hadi hivi sasa tumefikia ukarabati mkubwa katika baadhi ya majengo ya Vyuo hivi na tutaendelea kufanya hivyo kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hotuba yangu nimeeleza hususan kwenye Ibara ya 53 kwamba tutaendelea na kuimarisha sio miundombinu peke yake lakini pia kuimarisha utendaji kazi kwa maana ya kutoa mafunzo kwa walimu na kutoa mafunzo kwa waendeshaji wengine, halikadhalika kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi.

Kumetolewa hoja pia kuhusu kuanzishwa kwa Benki za Wanawake na chombo cha wanawake. Napenda kusema kwamba kwa kweli kuhusiana na Benki ya Wanawake sasa hivi tumefikia katika hatua ya juu kabisa na tunamshukuru sana Mheshimiwa Haroub Said Masoud maana yake yeye alitoa ushuhuda kwamba ni siku chache zilizopita tu alikuwa ameshirikiana na wataalam wa Wizara yetu katika kuendeleza mchakato huu wa kuundwa kwa Benki ya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chombo, Serikali imeendelea kuwezesha uanzishaji wa chombo hiki na tunachukua ushauri wa Mheshimiwa Esha Stima kwamba tuwashirikishe Waheshimiwa Wabunge. Napenda niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tuliwahusisha kupitia iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii na tulipata uwakilishi wa Wabunge kadhaa lakini uwakilishi ambao ulitusisimua sana ni kuwepo kwa Mheshimiwa Bakari Mbonde, ambaye alikuwa na heshima ya kuwa Mbunge mwanaume peke yake aliyeweza kufika. *(Makofi)*

Kwa hiyo tutaendelea, lakini huo siyo mwisho kwa hatua zozote zile tutakazopitia itabidi tushirikiane na Waheshimiwa Wabunge kuwafahamisha kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Esha Stima, uzoefu ule wa Chombo kile cha mwanzo utakuwa ni muhimu sana katika kuona chombo hiki kinaundwa vipi ili kuepuka yale yaliyotupata kwa wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema jambo moja ambalo limeongelewa na Msemaji wa Upinzani kuhusu suala la mikopo. Kwenye hotuba yake Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema kwamba mikopo haiwezi kumkomboa Mwanamke. Huo siyo ukweli kamili. Mikopo ni sehemu ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Kwa hiyo tukisema kwamba mikopo haimkomboi mwanamke siyo kweli, utafiti tulioufanya wa kisayansi kabisa unaonyesha ni namna gani wanawake wanafaidika na mikopo na tunachosema ni kwamba mikopo ni mojawapo ya vyanzo vya

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda pia kuangalia hoja iliyotolewa kuhusu wanawake kuteuliwa katika nafasi za uongozi. Tunashukuru kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wameipongeza Serikali na hususan Mheshimiwa Rais Mkapa kwa jinsi ambavyo amekuwa akijitahidi kutoa fursa mbalimbali za uongozi kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya Chama cha Mapinduzi ya kuwawezesha wanawake kushika madaraka katika ngazi mbalimbali na hadi sasa ni Chama cha Mapinduzi pekee kilichotenga nafasi maalum na kuongeza idadi yake kwa ajili ya uongozi na hivyo basi Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi itaendelea kuwapa wanawake nafasi za uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa niweke sawa suala moja ambalo limezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu suala zima la maendeleo, lakini hapa kulikuwa na Wilaya

maalum iliyotajwa, ni Wilaya ya Ngorongoro na taarifa ile inasema kwamba Ngorongoro haina hospitali ya Wilaya. Labda kwa ajili tu ya kumbukumbu sahihi niweze kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Ngorongoro kuna Hospitali ya Kanisa Katoliki inayoitwa Waso na ni Hospitali Teule ya Wilaya. Kwa hiyo, inapata uangalizi wote unaostahili Hospitali ya Wilaya na inatoa huduma zote za Hospitali ya Wilaya na ni moja ya Hospitali zenye huduma nzuri sana ikiwa ni pamoja na huduma ya Madaktari ambao wanaitwa *Flying Doctors* au Madaktari wanaoruka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hivi sasa katika nchi yetu bado tuko nyuma kwa sababu wananchi hawapati maji, hilo nalo siyo kweli. Hivi sasa hali ya maji nchini inaonyesha kwamba asilimia 73 ya wakazi wa Mijini wanapata maji safi na salama. Tuna imani kabisa chini ya uaskari wa mwavuli wa Mheshimiwa Edward Lowassa tutaendelea kuongeza asilimia hii ili ifikie katika ngazi ya juu zaidi, lakini ningependa kusisitiza kwamba asilimia 73 ya kupata maji safi na salama sio ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakazi wa Vijijini tuna asilimia 53 ya wanaopata maji safi na salama. Hiyo nayo ni hatua ya kuridhisha lakini tunafahamu kwamba bado inahitajika kufanyika jitihada ya ziada, lakini la msingi ni kutambua kwamba kazi inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala kuhusu wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shuleni. Napenda niseme kwamba ipo Sheria ya Elimu inayoshughulika na suala hili, lakini vile vile nadhani wakati Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba akijibu baadhi ya hoja aliweza kuzungumzia pia Sheria ya Makosa ya Kujamiiana na umri ule ambao unaweza ukamfanya mtu akaingia hatiani na ujauzito itakuwa ni sehemu ya ushahidi kama mtu amefanya kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kujibu baadhi ya hoja ambazo nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri hakuweza kuzijibu, lakini mojawapo ambalo limechangiwa ni kuhusu mila potofu amezungumzia lakini pia kulikuwa na mambo ya mirathi. Napenda niseme kwamba hivi sasa Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba inalishughulikia suala hili na kama ambavyo Mheshimiwa Bakari Mwapachu aliweza kutueleza ni kwamba tumefikia mahali pazuri na labda katika muda siyo mrefu sana tutaweza kuja na sheria Bungeni ambayo itaangalia maeneo yote yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza ikiwa ni mirathi, matunzo ya watoto na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya hoja kama nilivyosema tutazijibu kwa maandishi, lakini labda niseme pia kulikuwa na wazo hapa kwamba Wizara yetu hivi sasa iangalie uanzishwaji wa Vituo vya Makazi ya Watoto Wadogo au Watoto Ambao Hawana Makazi. Labda niseme kwamba sera ya Serikali ni kuhakikisha kwamba watoto hawa wanakuwa katika jamii zao. Kuwepo kwa Vituo vya kuwalea watoto wadogo au kuwepo kwa Vituo vya kuwalea watoto wa Mitaani ni hatua ya mpito tu, kwa sababu tunaamini kwamba mtoto anakuwa vizuri zaidi akiwa katika mazingira ya familia. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na wadau na hivi sasa tunayashukuru sana Mashirika yasiyo ya kiserikali na Taasisi za Kidini ambazo zinaisaidia sana Serikali katika kuendesha Vituo hivi. Lakini kama nilivyosema, tunaamini kwamba hilo ni suala la muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia ningependa kujibu hoja moja ambayo aliizungumza Mheshimiwa Haroub Masoud kwamba tuweze kuwa na Madreva wa kike na alikuwa anataka apate taarifa itakuwaje. Nilikuwa nimemwuliza Mheshimiwa Mwapachu na kwa kuwa mimi ni Mwanasheria, alikuwepo shahidi Mheshimiwa Prof. Mwandosya na Mheshimiwa Mwapachu alisema kwamba kwa kweli yeye haafiki sana suala la kuwa na *Driver* wa kike. Sababu ni kwamba anapotoka Dar es Salaam akifika Mlandizi anapumzika, akifika Chalinze anapumzika, akifika Morogoro anapumzika, sasa hiyo inaweza ikaleta utata kidogo. Kwa hiyo, amesema kwamba yeye hataajiri *Driver* wa kike. Kwa upande wangu, nilipotoka hapa kwa kweli nilimkuta Dereva wangu amenyong'onyea sana, akaniambia kwamba sasa Mheshimiwa Waziri, ubaguzi wa kijinsia unaupiga vita ndani ya Bunge, ukitoka nje unataka kuniondoa, sasa itakuwaje? Kwa hiyo, suala hilo bado naendelea kulitafakari Mheshimiwa Haroub. Lakini nazingatia pia hofu inayompata Mheshimiwa Mwapachu, lakini kwangu bado haijaniletea mtafaruku. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... Sh. 500,927,326/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... " 50,586,640/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... " 116,715,144/=
Kif. 2001 - *Training and Folk Development Colleges* .." 1,653,069,023/=
Kif. 2002 - *Community Development* ... ... ... ... ... " 609,626,795/=
Kif. 3001 - *Gender Development* ... ... ... ... ... ... " 800,361,272/=
Kif. 3002 - *Children Development* ... ... .... ... ... ... " 162,000,000/=

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ....... .... Sh. 200,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*... ... ... ... ... ...... ....Sh. 793,079,400/=
Kif. 2001 - *Training and Fold*
*Development Colleges* ........... ..... ......... Sh. 180,000,000/=
Kif. 2002 - *Community Development*... ... ... ....... .......Sh. 200,000,000/=

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio ya Matumizi hayo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto Kwa Mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 21(6), naomba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa dakika 47 kabla ya muda wake hadi kesho saa 3.00 Asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu nitoe maelezo yangu binafsi chini ya Kifungu cha Kanuni za Bunge Namba 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kutoa maelezo yangu binafsi kuhusu mgawanyo usioridhisha wa fedha za *STABEX* kiasi cha *Euro* milioni 38 au fedha za Kitanzania Shilingi bilioni 42 na kumwomba Waziri wa Kilimo na Chakula atoe majibu ya *order* zilizomo katika maelezo haya. Tangu Bunge lako Tukufu lianze uhai wake mnamo Novemba 2000 hadi Juni, 2003 jumla ya maswali ya msingi 34 na 43 ya nyongeza yameshaulizwa na Waheshimiwa Wabunge kutoka Vyama vya Siasa mbalimbali na kutoa Mikoa mbalimbali ya Tanzania inayolima kahawa kuhusu kutoa sehemu ya fedha za *STABEX* kwa wakulima wa kahawa ili kufidia hasara waliyoipata kutokana na kuanguka kwa bei ya kahawa katika Soko la Dunia pamoja na sababu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati wote majibu ya Serikali yamekuwa hayaridhishi na yanayojikanganya kila mara. Lakini pamoja na majibu ya kujikanganya, Serikali imekiri kuwepo kwa fedha hizo za *STABEX* ya kahawa. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa sababu kubwa mbili kwa nini wakulima wa kahawa hawapaswi kupewa sehemu ya fedha hizo za *STABEX* moja kwa moja, nazo ni:-

(i) Kuwa Jumuiya ya Nchi za Ulaya imekataa kutumika kwa fedha ya *STABEX* kuwalipa wakulima wa kahawa kwa sababu ya kuwepo kwa soko huria;

(ii) Kwamba Serikali inataka kutumia fedha hizo katika viwanda vya kukoboa kahawa katika Vyuo vya Utafiti na ujenzi wa miundombinu.

Nitazijadili na kuzichambua sababu hizo mbili hapo baadaye. Kwanza nitoe maelezo mafupi kuhusu historia ya fedha hizi za *STABEX.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *STABEX* zinatokana na makubaliano kati ya nchi 77 za Afrika, *Caribbean and Pacific, ACP* kwa upande mmoja na nchi za Jumuiya ya Ulaya, *EU* kwa upande mwingine. Makubaliano ya kwanza yaliitwa *Rome Cooperation Agreement.* Lakini Mkataba wa Rome uliisha mwaka 2000 na ndipo mnamo mwezi Juni, 2000 yaliposainiwa makubaliano mengine yaitwayo *The Cotonou Agreement* yanayoanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2020. Ukiwa na makualiano yaliyofanyiwa marekebisho ili kutoa misaada ya kimaendeleo na kupunguza umaskini, mpango mpya kwa ajili ya ushirikiano wa kikanda, utaratibu mpya wa kibiashara na usafi wa kisiasa wa kuimarisha utawala bora na utengamano wa kijamii. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2000 hadi 2005 nchi za *ACP* zimetengewa jumla ya *Euro* bilioni 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ikumbukwe kuwa madhumuni makubwa ya mfuko wa *STABEX* ni kupunguza madhara yatokanayo na hasara kubwa kutokana na upungufu wa bei ya bidhaa zitokazo nchi za *ACP* katika Soko la Dunia. Kwa Kiingereza wanasema *The general purpose of the STABEX System is to listen the effects of loses of commodity, export earnings by ACP States when there is a fall in work places or in exports.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima nikiri kuwa fedha za *STABEX* zinatolewa kwa ajili ya mazao mbalimbali kama vile kahawa, pamba, chai, katani, karafuu na kadhalika. Ila sina uhakika kama hawa wa karafuu na wengine wamepewa. Tangu mwaka wa 1985 hadi 2002 Tanzania imewahi kupata fedha za *STABEX* kwa kila zao lililotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2002 Kamishna Nelson wa *The European Commission* alitiliana saini makubaliano na Serikali ya Tanzania kututumia *Euro* milioni 38 au bilioni 42 kwa ajili ya kuendeleza kilimo ikiwa ni pamoja na kuongeza mapato ya mkulima wa kahawa. Taarifa ya *Union Commission* inasema, *in December, 2002 Commissioner Nelson sent a new claim of a Committee obligations for the intervention of Euro 38 million made available to Tanzania for coffee export, lost mainly in 1994 and 1999.* Ni dhahiri kuwa Jumuiya ya Ulaya inajua kuwa kulikuweko na ankara ya bei ya kahawa katika soko la dunia kuanzia mwaka wa 1994 hadi 2003 na ni ukweli na uwazi kuwa Serikali ya Tanzania inajua kuwa mwaka 1999 hadi 2002 bei ya kahawa kwa mkulima ilianguka vibaya sana kuliko ilivyowahi kutokea katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, wakati kwa upande wa Serikali kipindi cha tangu 1999 hadi 2002 mapato ya Serikali na pato la Taifa kwa ujumla ilikuwa likiongeka kwa wastani wa asilimia

tano kwa mwaka, basi pato la mkulima wa kahawa ilikuwa linapungua kwa zaidi ya asilimia 70. Kwa hiyo, wakulima wa Tanzania na hususan wakulima wa kahawa waliathirika vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nimkumbushe Mheshimiwa Waziri takwimu jinsi hali ilivyokuwa. Hapa kuna takwimu za tangu mwaka 1994 hadi 2002-2003. Nitasoma za miaka mitatu. Kwa mwaka wa 1994/1995 Mkoa wa Kilimanjaro bei ya kahawa *milled coffee,* kilo moja ilikuwa shilingi 1,200/=. Mkoa wa Mbeya 1,200/=, Mkoa wa Ruvuma 1,200. Mkoa wa Iringa na Rukwa 1,200/=. Mkoa wa Kagera ambayo ilikuwa 340/= na Ukerewe na Mara ilikuwa 340/=. 1995/96 Kilimanjaro ilikuwa 1,200/=, Mbeya 1,000/=, Ruvuma 1,000/=, Iringa na Rukwa 1,000/=. Kagera 340/=, Ukerewe na Mara 340/=.

Kwa mwaka 2001/2002 Kilimanjaro ilikuwa bei ya kilo ya kahawa ni sh.500/=, Mbeya sh.350/=, Ruvuma sh.300/=. Iringa sh.300/=. Kagera sh.50/=. Mara na Ukerewe sh.120/=. Mwaka 2002/2003, bei ya kahawa Kilimanjaro ilikuwa sh.500/=, Mbeya 300/=, Ruvuma 300/=, Rukwa 300/=, Kagera 90/=, Mara na Ukerewe 120/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa katika takwimu hizi, msimu wa 94/95 dola moja ya Kimarekani ilikuwa inabadilishwa kwa shilingi za Kitanzania 509.57, mkulima wa Kilimanjaro alipata kwa kilo moja sh.1,200/=. Lakini msimu wa 2002/2003 dola moja ilikuwa sh.120/= za Tanzania na mkulima wa Kilimanjaro alipata sh.500/= na mkulima wa Kagera alipata sh.60/= kwa kilo. Vile vile ikumbukwe kuwa bei ya kahawa katika soko la dunia mwaka 2003/2004 itakuwa pungufu kwa vile uzalishaji wa kahawa kwa dunia nzima ni magunia milioni 140, wakati kahawa inayotumika na kutosheleza mahitaji ni magunia milioni 110. Hivyo kutakuwa na ziada ya magunia milioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa nirudi katika hoja za Serikali za kukataa kumega angalau bilioni 5 kutoka bilioni 42 kuwalipa wakulima wa kahawa, pamoja na kwamba Jumuiya ya Ulaya imekataa sehemu ya pesa za *STABEX* isitolewe kwa wakulima wa kahawa siyo ya kweli. Hoja hiyo ni hoja ya Serikali ya Tanzania, kwa sababu nchi za Ulaya zinawapa wakulima wao hela ya *STEBEX* na kwa vyovyote vile kama Serikali ya Tanzania ingejenga hoja za kutosha na za kimsingi hoja hiyo ingekubalika, vinginevyo ni kwamba kulikuwa na udhaifu katika ujenzi wa hoja.

Katika barua ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba yenye Kumb. Na. Inaishia na 106 ya tarehe 8 mwezi wa saba 2002 kwenda kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Dr. Kabourou, Mbunge, aliyetaka kujua kama Jumuiya ya Ulaya itatoza fedha za *STEBEX* wasipewe wakulima wa kahawa. Mheshimiwa Mramba aliandika na ninamnukuu. *"As to whether the EU Commission has directed the fact that the STABEX funds should not be paid directly to farmers, I wish to assure you that, this have not been the case."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Jumuiya ya Ulaya katika madhumuni yake makuu katika kutoa fedha za *STABEX* ni katika kufidia hasara ya zao husika iliyotokana na kupungua kwa bei katika soko la dunia. Hivyo Jumuiya ya Ulaya inajua kuwa wakulima wa Tanzania na hususan wakulima wa zao la kahawa walipata hasara kubwa sana na Serikali ya Tanzania inalijua hilo. Kwa hiyo, kama Serikali ya Tanzania ingependelea na kupendekeza kuwa sehemu ya *STABEX* ya kahawa angalau asilimia 20 walipwe wakulima wa kahawa, Jumuiya ya Ulaya isingekuwa na kipingamizi na hata hivyo haina kipingamizi.

Hoja ya Serikali kuwa haiwezi kutoa *STABEX* kwa wakulima wa kahawa kwa vile waliuza katika vyama vya ushirika na wengine kwa makampuni binafsi. Ni hoja isiyokuwa na chembe yeyote ya uzito kwa sababu:-

Moja, makubaliano ya nchi za *APP and EU* ni pamoja na kuwa na mfumo wa soko huria. Mbili, Serikali ya Tanzania walipewa fedha za *STABEX* ya chai kwa wakulima wa chai kuanzia mwezi Juni, 2002 hadi Novemba, 2002, wakati na wao walishiriki katika mfumo wa soko huria. *(Makofi)*

Ninaipongeza Serikali na wakulima wa chai kwa kulipa angalau kidogo. Hoja ya Serikali kuwa inataka kutumia fedha ya STABEX katika kukarabati viwanda, haina msingi kwani Serikali inajitoa katika

kujenga viwanda na kuviendesha. Hata hivyo sisi hatukatai na ndiyo maana tunadai wakulima watengewe asilimia 20 ya bilioni 42 na zinazobaki zikafanye kazi ambazo Serikali inazipendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo hapo juu ninapenda kujenga hoja za namna mbili. Moja katika mfumo wa ushauri kwa Serikali na hoja katika mfumo wa maswali kwa Serikali.

(a) Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutaka fedha zote za *STABEX* kutumika katika ujenzi wa miundombinu, utafiti na kuimarisha Sekta ya Kilimo kwa ujumla, basi Serikali ifikirie kuwapa japo fedha kidogo wakulima wa kahawa.

Mkulima anahitaji fedha za kutunza shamba lake la kahawa kwa kuweka nyasi shambani, kununua pembejeo, kununua magunia ya kuhifadhia kahawa, kukodisha gari la kupeleka kahawa yake kwenye chama cha msingi au sokoni. Kuwalipa vibarua kwa kuvuna kahawa na mwisho, kupata fedha za kukidhi mahitaji ya familia yake kama vile elimu na afya kwa watoto wake.

(b) Kwa kuwa mkulima wa kahawa amekwishakufa moyo, kutokana na bei ya uzalishaji kuwa kubwa kuliko malipo anayoyapata kutokana na mauzo ya kahawa. Je, Serikali kumpa lishe bora ni sawa na usemi kuwa *even he takes the machine gun, when paid in the hands of the dead person, is as useless as a walking stick in hands of a baby. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie! Serikali inapaswa kuwalipa wakulima wa kahawa angalau fedha kidogo za *STABEX* kwani Serikali ikiweka utaratibu nzuri wa kuhesabu miche ya wakulima na kila mmoja akalipwa kufuatana na idadi ya mche bora aliyonayo, yafuatayo yakitekelezwa:

(a) Kila mkulima atahakikisha anaongeza idadi ya miche;

(b) Atahakikisha anatunza miche aliyoipanda;

(c) Hata wingi na ubora wa kahawa utategemea angetunza shamba lake;

(d) Kahawa haitaanikwa tena kwenye vumbi;

(e) Vijana wengi pia watajiunga katika kilimo cha kahawa kwa kuwa na faida kwani sasa wamekata tamaa.

Naomba Serikali ikumbuke msemo huu wa mwana saikolojia mmoja katika masuala ya Uchumi alisema kuwa: *"Money is the best motivator of the human behavior" ,* nitakutajia baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa upande wa hoja zilizoko katika mfumo wa maswali naomba Serikali nieleze yafuatayo:-

Katika suala la miundombinu hasa barabara, Wilaya ya Karagwe, hususan jimbo la Gewe, linazalisha nusu ya kahawa yote ya *Robster,* itapata fedha kiasi gani kwa barabara hii?

Kwa Mikoa ya Rukwa, Kigoma, Mara, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Morogoro, Ruvuma, Iringa, ni barabara ngapi za vijijini kabisa zitapata fedha za *STABEX* katika maeneo yanayolimwa kahawa.

Je, Serikali inakiri kuwa wakulima wa kahawa walipata hasara kubwa kwa miaka mitatu iliyopita? Na kama inakiri ni kwa nini inawanyima angalau fedha kidogo ili waweze kufutia machozi. Je, kama bei ya kahawa itaendelea kuporomoka katika soko la dunia na wakulima wataendelea kupata hasara, na Umoja wa Jumuiya ya Ulaya ukaendelea kuleta fedha ya *STABEX* kwa Serikali. Je, Serikali itaendelea kuwanyima fidia kidogo hawa wakulima?

Je, baada ya maelezo haya na kutokana na kilio cha Waheshimiwa Wabunge, cha kuomba wakulima wa kahawa wapewe fidia Serikali inakubaliana kutafuta uwezekano wa angalau shilingi bilioni tano ili kuwafidia wakulima wa kahawa?

Je, Serikali itakuwa tayari kwenda kwenye Wilaya zote na Mikoa yote inayolima kahawa kuwauliza wakulima ni kitu wanahitaji kuendeleza morali na hali ya kuendeleza zao la kahawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati nikichangia hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema yuko tayari kunipa hela niende Jumuiya ya Ulaya kuwauliza. Lakini na Waheshimiwa Wabunge wengine wako hapa. Tunaweza kwenda kwa hela zetu na tukajenga hoja na baadaye tukaja kumdai Mheshimiwa Waziri.

Baada ya kuyasema hayo, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe majibu ya uhakika kwa hoja hizi. Naomba kuwasilisha na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ambayo haiko kwenye *Order Paper,* ya siku hiyo haijadiliwi. Kwa hiyo, nitawahoji hoja ya awali ya kuahirisha Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01.11 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 29 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*